**22 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 22 Mei, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, Kikao cha Thelathini na Moja.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 405

**Ujenzi wa Zahanati ya Mtego wa Simba – Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kuendeleza ujenzi wa Zahanati ya Mtego wa Simba katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024, Serikali ilipeleka shilingi bilioni 4.9 katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Vituo vya Afya vya Kakero na Mkukazi pamoja ukamilishaji wa maboma 16 ya zahanti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro itatenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kukamilishaji ujenzi wa zahanati ya Mtego wa Simba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba

amwagize mkurugenzi kwa sababu ni fedha kidogo, aweze kuzitafuta kusudi wananchi waweze kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; Zahanati ya Fulwe katika Kata ya Mikese ni muhimu sana inahudumia hasa majeruhi na iko barabarani na wananchi wanaitumia sana hasa wanawake kwa kujifungulia, lakini unakuta wodi hiyo ni ndogo sana na wanaume wanaoumwa na wenyewe wanasubiria humo humo wakati wanatibiwa. Kwa hiyo, wananchi wamejenga wodi yao ambayo imechukua muda mrefu. Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia hiyo wodi ambayo wananchi wameweza kujenga kwa nguvu yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Zahanati ya Magadu inahudumia mitaa kama minne lakini inahitaji ukarabati. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kusudi iweze kukarabatiwa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma kwa namna ambavyo ameendelea kufuatilia huduma za afya kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Morogoro na katika Halmashauri ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu kwamba tumeshakubaliana na mkurugenzi watafute fedha milioni 50 mapema iwezekanavyo ili waende kukamilisha lile jengo ambalo wananchi wa Kijiji cha Fulwe wamechangishana kuanza ujenzi. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumsisitiza mkurugenzi kwamba pamoja na kwamba tuna mpango wa kuweka kwenye bajeti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 waangalie uwezekano wa kufanya *reallocation* na kupeleka fedha mapema iwezekanavyo ili kuepusha utaratibu wa kuweka wanaume katika wodi ambayo akinamama wanajifungulia. Suala hili halikubaliki na ni lazima lichukuliwe hatua mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wodi ya wanawake ya kujifungua lazima itumike kwa ajili ya wanawake peke yake. Sasa ikishatokea kuna wanaume wanatumia wodi hiyo maana yake ni suala la dharura lazima jengo likamilishwe ili wanaume wapate nafasi na wanawake wapate nafasi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na Zahanati ya Magadu ambayo imechakaa, inahitaji ukarabati, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutawasiliana na Halmashauri ya Morogoro tuweze kuona kiasi cha fedha ambacho kinahitajika na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tuone uwezekano wa kupata fedha hiyo pia kwa kushirikiana na mapato ya ndani ya halmashauri ili zahanati iweze kukarabatiwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Vijiji vya Mgansa, Isubangala, Kabanga ni vijiji ambavyo vimejenga zahanati kwa kutumia nguvu za wananchi na wamefikia hatua ya maboma. Je, lini Serikali itaweza kuwasaidia kuwapatia fedha wamalizie hizo zahanati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutambua maboma ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na imeendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma yale ili zahanati ziweze kutoa huduma na katika kipindi cha miaka mitatu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshapeleka zaidi ya bilioni 89.9 na maboma zaidi ya 1,789 yamekamilishwa yakiwemo maboma katika Halmashauri hii ya Wilaya ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso kwamba zahanati hizo tatu alizozitaja

tutaendelea kuzipelekea fedha ili zikamilishwe na wananchi wapate huduma katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha katika Kata ya Mahurunga, Kijiji cha Kivava kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ambayo nguvu kubwa ya wananchi imetumika hapo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba tunaendelea kupeleka fedha kwenye zahanati kwenye maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa kijiji hicho kwa kutoa nguvu zao kuchangia kujenga zahanati na niwahakikishie tu kwamba Serikali aidha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri au Serikali Kuu tutahakikisha tunapeleka fedha kukamilisha boma hilo ili wananchi waanze kupata huduma katika eneo hilo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kwa niaba ya Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 406

**Ujenzi wa Stendi ya Mabasi na Soko Kuu Makambako**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Stendi ya Mabasi na Soko Kuu Makambako Mjini kupitia Mradi wa kuboresha Miji 45 nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa stendi ya Mji wa Makambako ipo kwenye Mradi wa kupendezesha Majiji, Manispaa na Miji *(Tanzania Cities Transforming Infrastructures and Competitiveness - TACTIC)* ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa katika awamu tatu; awamu ya kwanza imeanza kutekelezwa katika Halmashauri 12, awamu ya pili imeanza kwa usanifu mwezi Januari, 2024 na zabuni inategemewa kutangazwa ifikapo Agosti, 2024 kwa halmashauri 15 na awamu ya tatu itakuwa na halmashauri 18 ambazo utekelezaji wake utaanza katika mwaka 2024/2025 ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya miradi itakayotekelezwa katika Halmashauri ya Mji wa Makambako ni pamoja na ujenzi wa soko na stendi ya kisasa. Hivyo, mradi huo utakapoanza, utekelezaji wa miradi hiyo utatekelezwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru Serikali kwa majibu mazuri, kwa maana ya wananchi wa Makambo wanaona mwanga sasa wa huu mradi ambao Watanzania wengi wanausubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja, Halmashauri ya Wilaya ya Makete ni moja kati ya halmashauri ambazo zinakuwa kwa kasi sana na mmetujengea barabara kutoka Njombe hadi Makete na Mheshimiwa Rais mwaka huu ametoa fedha tunajenga kutoka Makete kuelekea Mbeya, barabara hii inaenda kuunganisha miwili wa Njombe na Mbeya. Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusu Stendi ya Wilaya ya Makete na ni lini itaanza kujengwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Sanga, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga amefuatilia kwa karibu sana kuhusiana na ahadi ambayo yeye kama Mbunge alitoa kwa wananchi wa Mji wa Makambako lakini amekuwa akifuatilia kwa karibu sana Serikalini kuona stendi hiyo inajengwa na barabara zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwahakikishia wananchi wa Mji wa Makambo, Serikali iko kazini, taratibu zipo mwishoni na watapata stendi yao mpya, soko pamoja na barabara ambazo waliahidiwa na Serikali hii inaendelea kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na Makete nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, tuna mpango mzuri wa kuhakikisha kila halmashauri zinakuwa na stendi za kisasa kwa ajili ya huduma kwa wananchi. Makete itawekwa kwenye kipaumbele waandae eneo, andiko tuweze kuona gharama ni kiasi gani ili tuone namna ya kupata fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kama ilivyo katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, Mafinga pia ipo katika Mradi huu wa *TACTIC* na tayari wananchi wa Kinyanambo tumeshatenga eneo kwa ajili ya kujenga stendi. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga stendi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mji wa Mafinga ni miongoni mwa

miji ambayo ipo kwenye mpango wa *TACTIC* wa miji 45 na niwapongeze wananchi na Mheshimiwa Mbunge kwa kutenga eneo la ujenzi wa stendi katika eneo la Kinyanambo. Niwahakikishie katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huo utaanza kutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ni moja ya halmashauri zenye mapato madogo sana na jambo hili linapelekea wakati mwingine kushindwa kuanza ujenzi wa masoko kwa ajili ya uzalishaji na kuongeza mapato ya ndani; na Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tayari halmashauri imeandaa andiko kwa ajili ya kupata fedha, je, ni lini fedha hii itakwenda kwa ajili ya ujenzi wa masoko ya bidhaa wanazozalisha Halmashauri ya Wilaya ya Rorya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, maandiko haya ya miradi ya kimkakati yanawasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunayafanyia uchambuzi pia kuona *business plan* yake na baadaye tunawasilisha Hazina kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Chege kwamba kama Halmashauri ya Rorya wameshawasilisha tutalifuatilia baada ya hapa tuone limefikia hatua gani ili hatua zinazofuata zifanyike na kuona uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaingilia kati mazungumzo kati ya Mkandarasi na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ili kuhakikisha Stendi ya Ngangamfumuni inakamilishwa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Halmashauri ya Moshi ni Serikali, lakini kama Halmashauri ya Moshi ina changamoto na mkandarasi ambao wameingia nao mkataba. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi kuona kwanza uwezekano wa kutatua changamoto hiyo ya kimkataba kati yao na mkandarasi katika ngazi ya halmashauri lakini kama suala hilo linahitaji ngazi ya Wizara walete taarifa rasmi ili Serikali iweze kuona namna ya kutumia wataalam wa wizara kushirikiana na Halmashauri ya Moshi kwa ajili ya kutatua mkwamo huo uliopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Geita ni sehemu ya Miradi ya *TACTIC* na tumekamilisha taratibu zote za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa stendi tangu mwezi Machi, lakini tunasubiri TAMISEMI wafanye maamuzi. Je, ni lini maamuzi hayo yatafikia mwisho ili mkandarasi aweze kuanza? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue hili suala la Mheshimiwa Kanyasu kuona sehemu gani mkandarasi amekwama kuanza kazi ili sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tushirikiane na Halmashauri ya Mji wa Geita kukwamua mkwamuo huo ili kazi iweze kuanza kama ilivyopangwa. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi nilikuona.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini soko la Kazima katika Manispaa ya Mpanda itaanza kujengwa kupitia miji 45? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Mpanda ni miongoni mwa manispaa zilizopo katika Mpango wa *TACTIC* wa Miji 45 na kwa sababu sina uhakika uko wa awamu ya kwanza, pili au ya tatu...

**MBUNGE FULANI:** Awamu ya pili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Iko awamu ya pili, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekii, awamu ya pili tayari tumeshaanza usanifu, watu wanaofanya usanifu kwa maana ya *consultancy* wanaendelea na mara tu usanifu utakapokamilika ile miradi itaanza. Kwa hiyo, Soko la Kazima ni miongoni mwa miradi ambayo itaanza kutekelezwa mapema katika mwaka ujao wa fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Manispaa ya Ilemela ni moja ya miji ambayo ipo katika Mradi wa *TACTIC* na kuna mpango wa kujenga soko pamoja na barabara zenye urefu wa kilomita 2.9, taratibu zote zimekamilika. Je, ni lini ujenzi huo utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwamba kwa kuwa tayari taratibu zote za kimkataba zimekamilika, mkandarasi amepatikana, kwa hiyo ni jukumu lao kuhakikisha kwamba anaanza utekelezaji wa mradi mapema iwezekanavyo ili mradi

uweze kutekelezwa kwa wakati na wananchi wa Ilemela waone manufaa ya Serikali yao kwa wakati. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 407

**Vijiji vya Kyerwa Kufikiwa na Umeme**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, lini vijiji na vitongoji vyote vya Wilaya ya Kyerwa vitafikiwa na umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Wazirim majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kyerwa ina jumla vijiji 99. Kati ya hivyo, vijiji 86 vimepatiwa umeme na vijiji 13 havina umeme. Vijiji hivi 13 vitapatiwa umeme hivi karibuni kupitia Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini. Aidha, Wilaya hiyo ina vitongoji 668 na kati ya hivyo 238 vina umeme na 430 havina umeme. Kazi ya kusambaza umeme katika vitongoji ambavyo havina umeme inaendelea katika Wilaya ya Kyerwa ambapo *REA* inaendelea kutekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji 59 kupitia Mradi wa Ujazilizi 2B na vitongoji 15 vipatapiwa umeme chini ya Mradi wa Vitongoji 15 kwa kila Jimbo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kwa vitongoji 356 vilivyosalia vitaendelea kupelekewa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha kupitia miradi mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua vitongoji vingi bado havijapatiwa umeme, lakini pamoja na uwepo huo wa umeme kumekuwa na changamoto kubwa sana ya kukatika kwa umeme ambao unatoka Uganda. Sasa nataka kujua baada ya kukamilika Mradi wa Rusumo ni lini tutaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa ili tuondokane na umeme ambao umekuwa kero kwa kukatika mara kwa mara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; pamoja na neema ya kupatiwa umeme kumekuwepo na changamoto wakati wa kusambaza nguzo na hasa *REA* wanapopita kwenye maeneo hukata migomba, miti, sambamba na mikahawa. Mfano mmoja ni mwananchi anayeitwa Josephat Buchadi amekatiwa zaidi ya miti yenye umri wa miaka 18, mia tatu bila kupewa fidia. Je, ni mkakati gani wa kuepusha kukata miti na mazao mengine wakati wakipitisha nguzo pia kupatiwa fidia au kuweka *component* ya fidia kwenye Mradi wa *REA* ili kuondoa adha zinazojitokeza kwa sasa? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kwanza kuhusiana na kupeleka umeme wa gridi katika Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kagera wote kasoro Wilaya za Ngara na Biharamulo, Wilaya zilizobakia za Bukoba Mjini, Bukoba Vijijini, Misenyi, Karagwe na Kyerwa zinapata umeme kupitia laini inayotoka Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumeshaanza kujipanga kupeleka Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Kagera katika wilaya hizi nne kupitia ujenzi wa laini kutoka Benako kwenda Kyaka. Tumeshapata fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo na tumeshasaini mkataba na mhandisi mshauri na sasa tuko katika hatua za kuweza kwenda kwenye zabuni ili kuweza kupata mkandarasi. Niwahakikishie wananchi wa Kyerwa na wananchi wote wa Mkoa wa Kagera, Serikali ya Awamu ya Sita imejizatiti kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Kagera na tumejipanga kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na fidia katika Miradi ya *REA,* miradi hii ni miradi ambayo inatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini. Ni miradi ambayo kwa kweli haina fidia na ndio maana wananchi wanapata umeme kwa kuunganishiwa kwa 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni wa fedha nyingi sana takribani trilioni 1.593 na umelenga kuwafikishia wananchi huduma na kwa hiyo *component* ya fidia haipo kabisa, lakini *specifically* kwa suala hili la mwananchi huyu Josephati Buchadi naomba nimpe pole sana na inaelekea kuna uzembe umefanyika kwa upande wa Mkandarasi, kwa sababu ndio ana wajibu wa kufanya *survey* kujua maeneo ya kupitisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namWelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *REA* walichukue suala hili, walifanyie utafiti kuona kama kulikuwa kuna uzembe katika kufanya *survey*. Ikibainika hivyo, basi tutaona ni hatua gani tunachukua, kwa ajili ya kumsaidia mwananchi huyu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga na baAdaye Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kupeleka umeme kwenye vijiji vyote vya Wilaya ya Simanjiro, kwa sababu, umbali kutoka kijiji hadi kijiji katika Wilaya ya Simanjiro ni mrefu, je, ni lini sasa Serikali itapeleka umeme, ili kuhakikisha jambo kubwa na jema la kupeleka umeme kila kijiji linaweza kuwafikia wananchi kwenye vitongoji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala ya Simanjiro. Pale Wilayani Simanjiro tuna miradi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji na hivi karibuni tumesaini mkataba na mkandarasi, *China Railway*, ambaye anapeleka umeme kwenye

vitongoji 159 vya Mkoa wa Manyara, ikiwemo Vitongoji vya Simanjiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishia Wananchi wa Manyara na Simanjiro pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala la kupeleka umeme katika vitongoji tumeanza kulifanyia kazi. Tutaendelea kulifanyia hivyo ili kuhakikisha umeme unafika kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Jimbo la Mbulu Vijijini, vijiji vyetu vimekaa mbali mbali. Mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliahidi kuwapelekea Wahadzabe umeme bila nguzo, yaani umeme wa *solar*. Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Waziri itatekelezwa ili Wahadzabe wapate umeme kama wananchi wengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maendeleo ya wananchi wake. Kuhusu kupeleka umeme wa *solar* kwa Wahadzabe; mradi huu tayari tumeanza kuufanyia kazi pamoja na ule wa kupeleka umeme wa jua katika visiwa. Mheshimiwa Mbunge, hili la kupeleka umeme huu wa jua kwa Wahadzabe tutalichukua na tutahakikisha linafanywa sambamba na miradi hii ya kupeleka umeme wa jua katika visiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, nilikuona.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kuna shida kubwa ya umeme katika eneo la wachimbaji wadogo, Kata ya Nyarukoba, Kijiji cha Msege; wamefunga *transformer* ambayo haiwezi kufanya kazi kwa hiyo, ipo kama pambo. Je, nini kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya wananchi wale ambao ni wachimbaji wadogo wapate umeme na wafanye kazi ya uchimbaji, ili wailipe Serikali kodi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Naomba nimsisitize meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Mara ahakikishe kwamba, anatembelea eneo hili la wachimbaji hawa wa mgodi na kuona uwezekano wa kuwawekea *transformer* ambayo inakidhi mahitaji yao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 408

**Sheria ya Ndoa Kuendana na Vita dhidi ya Ndoa za Utotoni**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ya Ndoa ili iendane sambamba na vita dhidi ya ndoa za utotoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maamuzi ya Mahakama ya Tanzania, Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa kupitia Tangazo Na.1. *Vol* 102, tarehe 5 Februari, 2021 kwa kupendekeza umri wa kuoa au kuolewa uwe ni miaka 18. Aidha, Bunge kupitia Kamati ya Uongozi iliielekeza Serikali kukusanya maoni ya wananchi

kuhusiana na suala hili. Baada ya maelekezo hayo, Serikali ilikusanya maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tarehe 26 Aprili, 2023, Serikali ilifanya Kongamano la Sheria ya Ndoa hapa Dodoma, ili kupata maoni zaidi kuhusu umri wa kuingia kwenye ndoa. Kongamano hilo lilikuwa na ushirikishwaji mpana wa wadau mbalimbali wakiwemo wazee wa kimila, viongozi wa kidini, wanataaluma, wanafunzi wa ngazi mbalimbali, watu mashuhuri na Waheshimiwa Wabunge. Kongamano hilo lilikuwa mubashara kupitia Televisheni ya Taifa na wananchi waliruhusiwa kupiga simu na kutuma ujumbe na maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha uandaaji wa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa na hivi sasa Muswada huo upo katika hatua za ndani ya Serikali. Mara hatua hizo zitakapokamilika, Muswada huo utawasilishwa Bungeni kwa utaratibu wa kawaida. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri sana yenye kuleta matumaini. Naomba hizo hatua sasa ziende kwa *speed* kama alivyojibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Edwin Maleko, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 409

**Kuimarisha Huduma za Usuluhishi Migogoro ya Ndoa**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa Serikali kuimarisha huduma za usuluhishi kwa migogoro ya ndoa na matumizi ya watoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 102 cha Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, Waziri mwenye dhamana na masuala ya Sheria amepewa mamlaka ya kuanzisha Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa katika kila kata au sehemu nyingine yoyote atakayoona inafaa. Aidha, mabaraza hayo yameanzishwa na yanafanya kazi katika kata zote nchini. Vilevile kifungu cha 101 cha Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, mgogoro wowote wa ndoa ni lazima upitie katika hatua za usuluhishi kabla ya kuwasilishwa Mahakamani. Mabaraza hayo yana mamlaka ya kusuluhisha migogoro ya ndoa ikiwemo matunzo ya watoto. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Maleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nataka kupata ufahamu, ni lini sasa Serikali itafanya maboresho ya Sheria hii? Maana gharama za maisha zimepanda na kiwango kilichokuwa kinatolewa zamani ni kidogo sana hakiwezi kukidhi matumizi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, nini Kauli ya Serikali kwa wale ambao wanashindwa kutekeleza yale majukumu ambayo wamekubaliana kwenye vile vikao vya usuluhishi na kusababisha watoto kupata shida? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Maleko kwa namna alivyofuatilia suala hili, amewasiliana na Waziri wangu na mimi mwenyewe kwa nyakati tofauti. Niseme tu kwamba, kuhusu uboreshaji wa Sheria ya Ndoa ambayo masuala ya matunzo ya watoto yamegusiwa; ni kweli sheria yenyewe ni ya mwaka 1971 hivyo, viwango vilivyowekwa wakati ule huenda ni kweli kwa sasa vimepitwa na wakati. Nadhani tuchukue pendekezo la Mheshimiwa Mbunge, tuielekeze Tume ya Marekebisho ya Sheria katika maboresho ya

Sheria ya Ndoa wanayoshughulikia sasa hivi wazingatie viwango hivi, ili viende na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu asiyetekeleza maelekezo au makubaliano yaliyofikiwa kwenye vikao vya usuluhishi, maelekezo yetu ni kwamba; mwananchi atakayeona halitekelezwi anaruhusiwa kwenda kwenye Mahakama kwa sababu, Mahakama ndiyo chombo chenye dhamana ya kutenga viwango vinavyopaswa kutolewa kwa ajili ya matunzo ya watoto. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero.

Na. 410

**Umuhimu wa Sheria ya *Plea-Bargaining***

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO K.n.y. MHE. ABUBAKAR D. ASENGA** aliuliza:-

Je, Serikali inaona bado kuna umuhimu wa Sheria ya *Plea-Bargaining*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20, kwa kuongeza vifungu vya 194A, 194B na 194C kwa kuanzisha utaratibu wa kukiri makosa kwa makubaliano maalum kati ya mshtakiwa na Serikali, ikiwa na lengo la kupunguza muda wa upelelezi na usikilizwaji wa mashauri, kupunguza mlundikano wa mahabusu, kuwezesha kubaini namna uhalifu ulivyotendeka pamoja na kubaini mitandao ya kiuhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanza kwa utaratibu huu mwaka 2019 hadi Juni, 2023 jumla ya mashauri 423 ambayo

yalihusisha watuhumiwa 1,040 yamemalizika kwa utaratibu wa *Plea-Bargaining*. Kiasi cha shilingi 54,643,730,080.13 zilirudishwa Serikalini kupitia utaratibu huu na shilingi 2,083,384,927.70 zilirejeshwa kwa wahanga wa uhalifu. Kutokana na faida hizo, Serikali bado inaona umuhimu wa kuwa na utaratibu huu wa kisheria katika mashauri ya jinai. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote walioipitisha sheria hii. Swali langu ni kwamba kwa kuwa, kumekuwa na malalamiko mengi tangu utekelezaji wa Sheria hii kuanza, je, Serikali haioni ipo haja ya kufanya utafiti na kubaini changamoto zinazotokana na utekelezaji wake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria yenyewe imetungwa mwaka 2019, mpaka leo ni miaka mitano tu. Hata hivyo, tunapokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge kwa msingi wa madai ya kuwepo kwa malalamiko, ili Tume ya Marekebisho ya Sheria iweze kuangalia kama kuna maeneo yanayohitaji kuboreshwa yaweze kuboreshwa ili yakidhi haja. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu unataka kuongezea? Karibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake na Mheshimiwa Chaurembo kwa swali lake. Pamoja na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala analoliulizia ni kati ya yale ambayo yalifanyiwa kazi na Tume ya Rais kuhusu maboresho ya

Haki Jinai. Kwa sasa linatengenezewa mkakati kupitia Kamati inayoendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri akaelewa pia kwamba, changamoto zile za awali kabisa zimeshatatuliwa baada ya Mheshimiwa Jaji Mkuu kutoa kanuni za kushughulika na mashauri yanayoisha kwa njia ya kukiri, ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi wa Mashtaka kutoa miongozo ya kuongoza Waendesha Mashtaka na Wapelelezi namna ya kushughulikia haya. Kwa hiyo mengine yanayoendelea kuibuka yataendelea kuangukia kwenye mkondo unaoendelea kufanyiwa kazi na Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mwanasheria Mkuu na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 411

**Mikopo ya Elimu ya Kati na Juu Kama Ruzuku kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. STELA I. ALEX** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani kutoa Mikopo ya Elimu ya Juu na ya Kati kama ruzuku kwa Watu wenye Ulemavu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi wote wa Kitanzania wenye uhitaji kwa kuzingatia Sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo, Sura 178 na Mwongozo wa Utoaji Mikopo kwa mwaka husika unavyoelekeza, ukiwalenga wanafunzi

wa Kitanzania wenye sifa za kitaaluma za kujiunga na taasisi za elimu ya juu, lakini wanashindwa kumudu gharama za ngazi hiyo ya elimu kutokana na hali ya kiuchumi na hivyo kuhitaji usaidizi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa utoaji mikopo unawapa ahueni wanafunzi wenye ulemavu au wenye wazazi wenye ulemavu kwa kuwapatia kipaumbele katika upangaji wa mikopo. Kwa upande wa ruzuku kupitia *Samia Scholarship,* tangu imeanza Mwaka wa masomo 2022/2023, jumla ya wanafunzi 23 wenye ulemavu wamenufaika na ruzuku hiyo. Vilevile, wanafunzi wenye ulemavu wanapewa kipaumbele kwa kupatiwa vifaa saidizi, ili kuwawezesha kumudu mazingira ya chuo katika kipindi cha masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Bodi ya Mikopo inaendelea kutumika kutoa mikopo ya elimu ya juu na kati kwa kuwajumuisha kwa usawa wanafunzi wote wenye sifa, wakiwemo wenye ulemavu ili watakapohitimu masomo yao waweze kurejesha na kuwasaidia Watanzania wengine wahitaji waweze kunufaika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa majibu haya mazuri. Pia, naomba niishukuru Serikali kwa hatua muhimu ambazo zimefikiwa kwa kundi hili la watu wenye ulemavu. Kipekee kabisa naomba niishukuru Serikali kwa uzingativu wa hoja ya utolewaji wa mikopo hii ya elimu ya juu kwa watu wenye ulemavu na uzingatiaji wa hoja hii kwamba, ulemavu ni kigezo wakati wa utoaji wa mikopo hii pia, kwa hilo naishukuru Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kufahamu, kwa hatua hii na kwa mambo haya mazuri yaliyofanyika, Serikali imefikia hatua gani kuifanya mikopo hii kuwa ruzuku kwa kundi hili la watu wenye ulemavu? Je, Serikali ina mpango wowote wa kuifanyia marekebisho Sheria hii ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili sasa kundi hili nalo liweze kunufaika? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, hivi sasa tunavyozungumza, Serikali imetengeneza kamati kupitia Wizara ya Elimu ambayo inafanya mapitio ya Sheria yetu ya Bodi ya Mikopo, ile Sura Na. 178, kuangalia namna gani Sheria hii itaweza kufanya kazi vizuri katika mazingira ya sasa. Ni kweli kumekuwa na malalamiko, *especially,* kwa wanafunzi ambao wanapata mikopo kwa kuzingatia sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuondoa wasiwasi, ipo kamati ambayo inapitia Sheria hii pamoja na zile Kanuni. Vile vile, Serikali imetengeneza tena Kamati ambayo inapitia Sheria ya Elimu. Sheria yetu ya Elimu ni ya Mwaka 1978 kwa hiyo, nadhani baada ya mapitio haya mambo mengi sana yanaweza kuingia kwenye utaratibu mzuri, ikiwa ni pamoja na wenzetu wenye ulemavu, huo ndiyo mpango wa Serikali. Namwondoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae, aulize swali lake; kwa niaba.

Na. 412

**Matumizi ya Magogo Kukatia Nyama**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza:-

Je, lini katazo la Bodi ya Nyama Tanzania la kuzuia matumizi ya magogo kukatia nyama litafanyiwa kazi ili kuwanusuru Watanzania kupata athari za kiafya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018, Bodi ya Nyama ilitoa tangazo kwa umma kuhusu katazo la matumizi ya magogo katika maduka ya nyama, yaani bucha. Kufuatia katazo hilo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilijulishwa na kuhimizwa kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia katazo hilo, matumizi ya magogo kwenye bucha hususan maeneo ya mjini umepungua, jambo linaloonesha wadau wameendelea kutekeleza katazo hilo la Bodi ya Nyama la matumizi ya magogo. Aidha, katika kuhakikisha katazo hilo linaendelea kutekelezwa Bodi ya Nyama imeendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye bucha, kutoa leseni za bucha kwa wafanyabiashara waliokidhi vigezo, ikiwa ni pamoja na kuwa na mashine ya kukatia nyama, kutoa mafunzo kwa wamiliki na wafanyakazi kwenye bucha kuhusu uendeshaji wa maduka ya nyama, matumizi sahihi ya vifaa vya buchani, uhifadhi wa nyama na madhara ya matumizi ya magogo katika kukatia nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Nyama kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu katazo la matumizi ya magogo na kusimamia utekelezaji wake, ili kuzalisha nyama yenye ubora na kulinda afya ya watumiaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa, tamko hilo lililotolewa na bodi bado halijatekelezwa katika baadhi ya maeneo na bado wanatumia hayo magogo ambayo yana madhara makubwa kwa maisha ya binadamu. Je, ni nini sasa Kauli ya Serikali kwa wale ambao wanaendelea kutumia magogo kuwaambia kwamba, waache mara moja na waendelee na taratibu nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, changamoto hizo za kukatia magogo maeneo ya mjini ni kweli inaonekana kuna mabadiliko, lakini vijijini kutokana na mazingira yao imekuwa ni vigumu sana watu kupata hivyo vikatia nyama vya kisasa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wale watu wa vijijini kuhakikisha na wao wanaweza kupatiwa vifaa hivyo hata kwa mkopo, ili waweze kuendesha biashara na kuepukana na madhara ya kukata nyama kwenye magogo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na hili la kwanza, kauli ya Serikali ni moja kwamba ni marufuku kutumia Magogo, kwa ajili ya kukatia nyama na tayari Serikali imeshatafuta *alternative* juu ya kifaa gani kinachoweza kutumika kwa ajili ya kukatia nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumewasiliana na wenzetu wa *SIDO* na wametoa *sample* ya mashine za bei rahisi kabisa ambazo zitaweza kutumika, kwa ajili ya kukatia nyama. Mashine hizi tayari zimeshaanza kusambaa katika Mikoa ya Arusha, Moshi, Manyara na maeneo mengine ili kuhakikisha kwamba, tunaondokana na hii teknolojia ya magogo na tunakwenda kwenye teknolojia ya kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuwahamasisha

*SIDO* waendelee kusambaza vifaa hivi mpaka vijijini ambako amesema Mheshimiwa Mbunge ili kurahisisha shughuli hii ya ukataji wa nyama, lakini Kauli ya Serikali ni moja kwamba, ni marufuku kutumia magogo kwenye bucha zetu, ni marufuku kutumia magogo kwenye ukataji wa nyama ambayo inaenda kutumiwa na wananchi wetu. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kusimamia na kuwasiliana na wenzetu wa Serikali za Mitaa, kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya mashine hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la mwisho ni kwamba, tutakapokuwa tumefanya uzalishaji wa kutosha kupitia *SIDO*, tutapeleka mpaka vijijini kwa bei nafuu. Kwa kipindi hiki ambacho *production* bado haijawa nzuri nawaomba wenzetu wa vijijini kujua madhara makubwa yanayotokana na matumizi ya magogo kwenye kukatia nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe Serikali za Mitaa kupitia Serikali za vijiji kuhakikisha kwamba wanasimamia jambo hili la kisheria na tayari tumeshatoa ufafanuzi wa jambo hili. Wenzetu wa Serikali za Mitaa tunaomba wasimamie ili iweze kukamilishwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba, Mheshimiwa Hussein Amar.

Na. 413

**Barabara ya Busisi – Buyagu – Nyang'wale hadi Kahama**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR K.n.y. MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Busisi kupitia Buyagu – Nyang'wale hadi Kahama kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya *Nyangh'wale Junction* (Busisi) – Wing3 – Nyangh'wale – Nyangh'olongo – Nyambula (Kahama) yenye urefu wa kilometa 204.13 inaendelea kwa sehemu ya Busisi – Nyang'wale kilometa 55. Kwa sehemu iliyobaki ya Nyang'wale – Nyambula (Kahama) yenye urefu wa kilometa 149.13, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. Mara baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusahihisha, Barabara ni kutoka Busisi – Nyang'wale - Nyangh'olongo – Kahama, siyo Nyambula. Baada ya masahihisho hayo, Mheshimiwa Waziri, majibu haya takribani sasa ni miaka 14 na ahadi hizi za Viongozi Wakuu wa Nchi kuanzia Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, mpaka leo hii ahadi hii haiajatekelezwa na kila ninaposimama tunapouliza swali hili, unasema fedha zitakapopatikana. Swali la kwanza; je, ni lini sasa upembuzi huu utakamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa kuna ujenzi wa kilometa moja kwa kiwango cha lami kwenye Mji Mkuu wa Karumwa takribani zaidi ya miezi 24 na uliahidi kwenda kutembelea maeneo hayo. Je, uko tayari kwa *weekend* hii tuongozane mimi na wewe ukaone kile ambacho kinaendelea pale? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ni ahadi ya viongozi. Ni kweli kwamba tulikuwa tunategemea tungekuwa tuko kwenye usanifu lakini kutokana na mabadiliko ya mfumo wa manunuzi ulivyobadilika, ndiyo ulipelekea tuchelewe kidogo. Hata hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunategemea kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha, tutakuwa tumeshapata mhandisi mshauri kwa ajili ya usanifu wa Barabara ya kutoka Nyankumbu – Kharumwa – *Wing3,* kwa sababu *Wing3* – Busisi tayari na kutoka Kharumwa – Nyangh'olongo – Kahama ambaye atafanya kazi kwa kusimamiwa na Makao Makuu. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalitambua na tutatekeleza kama tunavyosema hapa na tuko kwenye hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa barabara wa kilometa moja katika Mji wake wa Kharumwa. kwanza nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ambaye amefuatilia sana, tulimwahidi kwamba baada ya mvua kukatika barabara hii itakamilishwa. Nataka nimhakikishie kwamba atakuwa shahidi kwamba Mkandarasi yuko *site* na tunategemea kabla ya mwisho wa mwezi Juni na kwa makubaliano awe amekamilisha barabara tarehe 10 Juni. Anaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu kwenda, kwa wiki hii nasema itategemea na ratiba yangu, lakini kama ratiba itaruhusu, kama hata siyo Jumamosi ya wiki hii basi hata utakayoona inawezekana, niko tayari kwenda naye ili kwenda kuona nini kinaendelea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kumba Ndulane, Mheshimiwa Zacharia Issaay, nimewaona.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wananchi wa Wilaya ya Kilwa na Liwale wanashukuru Serikali jana imeweza kurejesha mawasiliano katika Barabara ya Nangurukuru – Liwale. Je, ni lini sasa Daraja la Miguruwe litaanza kujengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea pongezi hizo kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye alitoa maelekezo kwamba kote ambapo palikuwa pameathirika, tuhakikishe tunarejesha mawasiliano. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya madaraja ambayo sasa hivi yameshaletewa tathmini katika Wizara pamoja na madaraja mengi na hasa ya Kusini, Mheshimiwa Rais tulishampelekea taarifa zote za mahitaji. Tutahakikisha kwamba Daraja hilo la Miguruwe ambalo limeathirika sana, linakwenda kujengwa ili kurejesha mawasiliano yaliyokuwepo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Minza…

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti tulisaini mkataba karibu mwaka sasa na kwa kuwa barabara hii inasubiriwa kwa hamu kubwa na wananchi. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii ishasainiwa na kulikuwa na mapitio ya usanifu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi mkandarasi yuko tayari kuanza kurudi *site* na kuanza kuijenga hiyo barabara. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza Mjika, nilikuona.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuuliza, Barabara ya Kolandoto – Kishapu mpaka Meatu ni ya muda mrefu sana na kila siku tunaahidiwa kwamba itaanza hivi karibuni. Je, ni lini sasa itaanza ili wananchi wa Mkoa wa Simiyu na sisi tunufaike na barabara hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo aliyoitaja ni moja ya barabara kuu. Katika mwaka huu wa fedha tumeiweka kwenye mpango ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi.

Na. 414

**Ujenzi wa Barabara ya Mwembe - Mbaga - Mamba – Same**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Mwembe – Mbaga hadi Mamba itafanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuanza taratibu za manunuzi ya kumpata mhandisi mshauri kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Mwembe – Mbaga – Mamba yenye urefu wa kilometa 90.19 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kukubali kufanya upebuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga Barabara hii ya Mwembe – Mbaga mpaka Mamba kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ningependa kujua kwamba Serikali ina mpango gani kurekebisha barabara hii kwa sababu baada ya mvua nyingi hizi, maeneo mengi yameharibika na hayapitiki vizuri. Sasa, ni lini ukarabati utafanyika kusudi barabara hii iweze kupitika kama kawaida wakati tunasubiri upembuzi yakinifu wa barabara hii ili ijengwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ningependa kujua ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja Jimbo la Same Magharibi hususan katika vijiji vinavyopitiwa na barabara hii ili aweze ku-*create awareness* kwa wananchi kwamba barabara yao inafanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mathayo, Mbunge, kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia kuanza usanifu wa barabara hii. Nikianza kujibu, nitaanza na swali lake la pili. Ni wajibu wetu pale ambapo kuna umuhimu wa kwenda kutembelea barabara, tunakwenda na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakubaliana naye lini twende tukatembelee hii barabara, ikiwa tu ni kuwajulisha wananchi nini Serikali yao ya Awamu ya Sita inategemea kufanya katika Barabara hii ya Mwembe – Mamba na tunakwenda mpaka Ndungu kwa maana ya barabara yote. Kwa hiyo niko tayari muda wowote Mheshimiwa Mbunge tutakavyokubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kurekebisha, barabara hii ni kati ya barabara ambazo ziko kwenye miinuko mikali sana. Katika kipindi hiki cha mvua, tunajua sehemu kubwa sana zimeathirika japo tulirejesha mawasiliano kwa muda. Kitu ambacho tunafanya sasa hivi, Meneja wa Mkoa ameshaleta taarifa ya kurekebisha na kurudisha sasa kwenye hali iliyokuwa ili irudi kwenye hali yake ya kawaida hii barabara. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimwa Mbunge, hilo linafanyiwa kazi na tunawahakikishia wananchi wa

Jimbo la Mheshimiwa Dkt. Mathayo kwamba tutarejesha hiyo barabara katika hali yake ya kawaida. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Licha ya athari ya Kimbunga Hidaya kwa Barabara ya Kibiti – Lindi, barabara hii ilikuwa na uharibifu mkubwa ambao ulihitaji matengenezo makubwa hata kabla ya athari ya Kimbunga Hidaya. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kufanyia tathmini Barabara hii ya Kibiti – Lindi na hivyo kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kuanza tena ujenzi au ukarabati mkubwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ilikuwa imechoka sana na kutokana na kuchoka kwake pia ndiyo maana ilipelekea kupata uharibifu kwa urahisi sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalifahamu na Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo, apate tathmini ya kina ya uharibifu, kwanza kwa yale maeneo yaliyoharibika, lakini pia na uchakavu wa hiyo barabara ili aone namna atakavyofanya ili kuhakikisha ya kwamba hii barabara muhimu na ya kiuchumi na barabara pekee inayounganisha Mikoa ya Kusini, inajengwa kwa kiwango ambacho itakuwa inaweza ikapitika muda wowote na ikiwa imara. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, aulize swali lake.

Na. 415

**Kukarabati Skimu ya Umwagiliaji Kalya na Mgambazi – Uvinza**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kukarabati Skimu ya Umwagiliaji ya Kalya na Mgambazi – Uvinza?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Skimu ya Umwagiliaji ya Kalya yenye ukubwa wa hekta 525 ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na inanufaisha wakulima zaidi ya 200. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Skimu za Mgambazi, Kashagulu, Nkonkwa na Ilagala zilizopo Uvinza ili kujua gharama halisi zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya umwagiliaji inaendelea kubaini maeneo ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji katika maeneo mbalimbali ikiwemo Skimu ya Kalya ili kuingizwa kwenye Mpango wa Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwenye skimu hizi nilizozitaja, nyingi katika hizi, kwa mfano Kashagulu pamoja na Mgambazi, wananchi wachache wanaomiliki hayo mashamba ambako ndiko hizo skimu zilienda kujengwa, ndiyo wanaofaidi hizi skimu. Hata zile

kamati ambazo ziliwekwa kwa ajili ya kutunza hiyo skimu, hazifanyi kazi zilifukuwa na wale wenye maeneo katika hayo mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali imepanga skimu ngapi kwenye mwaka huu wa fedha ambazo zitajengwa katika Wilaya ya Uvinza? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tunapokuja kujenga *schemes*, moja ya mambo ambayo tumekuwa tukiyafanya na kuyatekeleza ni kuhakikisha ule mradi tunaupeleka kwa wananchi wa eneo husika ikiwemo, tukijumuisha na Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo kifupi ni kwamba, zitakapokuwa zimekamilika, maana yake skimu hizi tutawapanga upya ili kuhakikisha wananchi katika maeneo hayo, wote wanafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu skimu ngapi zinajengwa katika maeneo hayo, niko tayari na Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge lako, tutaenda kukaa na watu wa watu wa Tume ya Taifa, ili kumuainishia maeneo gani ambayo katika jimbo lake yanajengwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Je, Serikali lini itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji Endasiwold, Getasam, Balangdalalu na Laghanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo tayari kutoa fedha. Jukumu ambalo tunalo sasa hivi, ni maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameeleza, yapo katika mpango wetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala, nilikuona. Nenda kwa Mheshimiwa Hhayuma.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Skimu ya Umwagiliaji ya Kidoka Wilaya ya Chemba imekuwa ni chakavu na Serikali haioneshi dalili yoyote ya kuhudumia skimu ile. Sasa, ni lini Serikali itakwenda kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa skimu ile ili wananchi waweze kuendelea na kilimo chao cha umwagiliaji na kupata tija pia katika skimu hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ambayo sisi Wizara ya Kilimo tunayo ambayo tumepatiwa na Mheshimiwa Rais ni kwamba, moja ya jukumu letu ni kujenga skimu mpya, kurekebisha skimu za awali zikiwemo zile ambazo wananchi walizianzisha wao wenyewe. Kwa hiyo ikiwemo Skimu ya Kidoka ambayo ni chakavu, ni kweli tunakiri, tunafahamu hilo na ipo katika mipango yetu. Maana yake tukishamaliza suala la usanifu wa kina na upembuzi yakinifu, tutaweka fedha na tutajenga na itawanufaisha wananchi wote katika maeneo hayo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Jimbo la Kalenga lina skimu takribani 19 ambazo ni chakavu na wananchi wamekuwa wakipata adha. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha skimu hizi zinarekebishwa na wanapata huduma nzuri ya umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa kwamba skimu zote za Kalenga zipo katika mpango wetu wa marekebisho. Ndiyo maana wakati najibu hapa nilieleza kwamba ukiacha ujenzi, tunafanya marekebisho katika skimu zote

ambazo zilianzishwa na wananchi na zile ambazo zilikuwepo tangu awali. Kwa hiyo nikuondoe shaka, wananchi watafaidika na mpango tulionao sisi Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha na sasa hivi nina matangazo.

Nitaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika, kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara, tuna Bwana Elibariki Shammy – *Country Director, Trade Mark Africa* na tuna Profesa Ulingeta Mbamba, Mwenyekiti *TANTRADE*, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Zainab Katimba kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Demokrasia *(National Democratic Institute)* Ndugu Sauda Mapunda, Ndugu Lucy Mwinuka na Ndugu Ocheck Msuva, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa wetu Naibu Waziri Zainab Katimba. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni 19 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo ambaye pia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Maafisa na Walimu Wakuu kutoka Kisarawe, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Jafo. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara, ni Mpiga kura wake kutoka Tarime Vijini Mkoa wa Mara, karibu sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Kunti Majala ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chemba, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, ndugu zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge Mstaafu wa Mbozi na mtoto wa mdogo wake, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi*

Tuna wageni tisa wa Mheshimiwa Halima Mdee, wanachama wa Yanga kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wanachama wenzetu wa Yanga kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 94 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, Watendaji Kata, Vijiji na Waratibu Elimu kutoka Same Magharibi Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana wageni wetu kutoka Kilimanjaro. *(Makofi)*

Tuna pia wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tunao wageni 12 wa kitanzania wanaosoma nchini India wakiongozwa na Ndugu Fabian John pamoja na Wajumbe wa UVCCM Taifa, karibuni sana wanafunzi mnaosoma India kutoka hapa Tanzania. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 75 na walimu saba kutoka Shule ya Awali na Msingi Lusansaro ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Dar es Salaam, karibuni sana mmependeza vizuri sana na walimu wenu karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapa kuna tangazo linatoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa, leo tarehe 22 Mei, 2024 kutakuwa na semina kuhusu Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Toleo la mwaka 2023 itakayotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, semina hii itafanyika mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu na tunaanza na Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, baadaye Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo wajiandae.

Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kutoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini, Wabunge tukitembea huko mitaani na Mikoa mbalimbali wafanyabiashara wengi wamefurahia sana mazingira mazuri ya uwekezaji ambao upo nchini kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu wake pia nitoe pongezi kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu yangu Wakili msomi Abdallah, wanafanya kazi nzuri sana kwenye hii Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hotuba ni nzuri na ipo mipango mbalimbali ambayo Wizara imepanga kusaidia Sekta ya Biashara na Viwanda. Katika ukurasa ya sita kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza pale kwamba sekta ya viwanda na biashara kwa kiasi kikubwa inategemea sekta binafsi, anasema

Mheshimiwa Waziri kwamba kazi ya Serikali kwa asilimia kubwa ni kusimamia uratibu, ushauri na kutoa mwelekeo wa tasnia ya viwanda na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nianze kutoa ushauri wangu kwa Wizara asubuhi hii. Mimi kwa maoni yangu nadhani Wizara iende mbali zaidi, badala tu ya kusimamia uratibu na kutoa mwelekeo wa sekta ya viwanda na biashara, ninashauri na wako baadhi ya Wabunge pia jana wamesema hapa ndani sekta hii au Wizara hii ya Viwanda na Biashara wasiishie tu kuratibu na kutoa mwelekeo, nimeona pia kwenye ukurasa wa 28 wa hotuba, Waziri anasema Wizara imesaidia kuwaunganisha wajasiriamali na mabenki kupata mikopo ya kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa badala ya kuwa wanawaunganisha tu wajasiriamali, ushauri wangu ni kwamba imefika wakati Wizara ya Viwanda na Biashara waanzishe *BBT* ya viwanda, kwa sababu watu wa kilimo wameanzisha *BBT* kwenye kilimo, tumeona mwelekeo mzuri sekta ya kilimo. Watu wa uvuvi wameanzisha *BBT* kwenye uvuvi na mifugo tumeona mwelekeo mzuri, ni wakati mzuri kwa Wizara ya Viwanda na Biashara anzisheni mfuko, Bunge liko hapa tupitishe bajeti kuwa na Mfuko Maalum kusaidia wajasiriamali wadogo wadogo kuanzisha viwanda vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Watanzania wengi wana mitaji kidogo, wana malengo mazuri ya kuanzisha viwanda kwenye maeneo yao. Viko viwanda vya kuzalisha mazao ya nafaka, viko viwanda vya vifaa mbalimbali lakini mitaji yao ni midogo, Wizara hii isiishie tu kuwa mlezi na mwelekezi, wawe na mpango maalum wa kuwanyanyua wajasiriamali hawa kwenda kwenye hatua kubwa zaidi ya viwanda na biashara. Tukifanya hivyo uhalisia au *relevance* ya Wizara hii utaanza kuonekana kwa ukubwa zaidi kwa hiyo tusiwaachie Wizara zingine kuinua watu wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwa kuwa hii Wizara ya Viwanda na Biashara tafsiri yake ni kwamba hawa pia ni watetezi wa wafanyabiashara, mimi ndivyo ninavyoelewa, lakini

Wabunge wote mnajua hapa wafanyabiashara wetu nchini wanazo changamoto nyingi sana hasa inapofika mahali wakifungua viwanda au kufungua biashara na yako maeneo mengine wafanyabiashara wanasema kufungua biashara baadhi ya maeneo ni kama kukaribisha matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishafungua biashara leo siku inayofuata *TRA* tayari wamekuja kwako, *OSHA* wamekuja kwako, *NEMC* wamekuja kwako, Halmashauri imekuja kwako mtetezi wa hawa wafanyabiashara ni Wizara ya Viwanda na Biashara. Ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, mwaka jana nilichangia kwenye Wizara ya Fedha ndani ya Bunge lako, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Wizara hii na Katibu Mkuu ndugu yangu yuko pale namwamini sana, waanzishe Dawati Maalum la Kupokea Kero za Wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hapa kwenye mitandao ya simu wana kitengo cha huduma kwa wateja masaa 24 kama kuna kero wananchi wanapiga simu wanasikilizwa. Wizara ya Viwanda na Biashara nawaomba waanzishe dawati maalum wakiwa kama watetezi na walezi wa wafanyabiashara wapokee kero za wafanyabiashara wawasaidie. Wafanyabiashara hawana mtu mwingine isipokuwa ninyi, wakipata shida huko *TRA* wao wanafuata kodi, *OSHA* wanafuata mambo yao ya *OSHA* lakini wanaopaswa kusimamia ustawi wa biashara ni ninyi Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, wanafanya kazi nzuri, mwaka juzi alikuja Mkoani Njombe tulizungumza naye, akauona Mkoa wa Njombe, mwaka jana tena amekuja Njombe mpaka Ludewa, namwomba sisi Mkoa wa Njombe ni Mkoa wa kimkakati kwa viwanda, tunayo ardhi ya kutosha, tunayo mazao mengi ya kilimo, pia kama ambavyo Rais wetu wa Awamu ya Sita amefanya kulipa fidia kule Ludewa, maana yake sasa Ludewa na Mkoa wa Njombe unakwenda kufunguka. Namwomba upange programu maalum kwa kuwa nyinyi wanaratibu na kutoa mwelekeo, sisi Jimbo la Lupembe tunayo maeneo kwa ajili ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lupembe sasa hivi wakulima wengi wanalima zao ya parachichi, lakini Lupembe nzima ambako watu wake wanalima matunda zaidi katika Mkoa mzima wa Njombe, hawana kiwanda hata kimoja. Nimwombe Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu nawakaribisha Njombe Jimbo la Lupembe waje waone maeneo muhimu, wayaratibu na kutoa maelekezo tupate Kiwanda cha Parachichi Jimbo la Lupembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Njombe *DC* na mimi kama Mbunge na Madiwani wangu tutakuwa tayari kuwapatia ushirikiano. Zipo Kata nyingi Kata ya Ninga, Kata ya Mtwango, Kichiwa, Ukalawa, Mfiriga, Idamba wanalima matunda mengi sana, lakini mengi yanapotea shambani kwa sababu hakuna viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kusema asubuhi hii ni kwamba, nimeona pia kwenye hotuba ya Waziri amezungumza habari ya viwanda mbalimbali viwanda vingi tu. Viwanda vya Chuma, viwanda vya marumaru, viwanda vya mabati na kadhalika, lakini sijaona viwanda vya mazao ya wakulima, sijui ameruka kwa bahati mbaya au hili jambo siyo muhimu? Kwa hiyo, nimeshindwa hata kujua sasa kuna viwanda vingapi vya chai nchini? Kuna viwanda vingapi vya sembe nchini? Nimeshindwa kujua kwenye hotuba ya Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimwombe kwamba, Njombe hasa Lupembe tuna viwanda vya chai na amesikia kilio cha Wabunge wa Mkoa wa Tanga hapa, kilio cha Wabunge wa Mkoa wa Mbeya, kwamba pia viko viwanda vya chai vimefungwa, tungetamani kujua kwenye hotuba yako hii angetuambia kuna viwanda vingapi vya chai, viwanda vingapi vimekufa na vingapi vinafanyakazi tungesaidia kushauri Serikali. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutuambia hapa basi na sisi watu wa Jimbo la Lupembe tujue viwanda vyetu vya chai nchini viko vingapi?

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Wakili Msomi Mheshimiwa Edwin Swalle, Mbunge wa Lupembe kwamba kati ya viwanda vingi hivyo vinaonekana kwamba vilichukuliwa na wawekezaji kutoka nchi jirani, kwa hiyo isije ikawa ni *sabotage* kwamba wamechukua halafu hawazalishi ili wenyewe nchi jirani waendelee kuzalisha chai. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Swalle, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa heshima kabisa na ndiyo maana nimesema hapa, kwamba kama ingeandikwa kwenye hii taarifa ya Mheshimiwa Waziri tungejua viwanda viko vingapi, vingapi vimekufa na mpango ukoje? Nimwombe Mheshimiwa Waziri, najua pengine *either* kama hajapitiwa basi pengine ameandika sehemu nyingine, atakapokuja atuambie viwanda vyetu vya chai vina hali gani nchini kwa sasa kwa sababu sisi watu wa Lupembe tuna maslahi na viwanda vya chai na tunatamani pia ukija Lupembe kufanya ziara tufungulie kiwanda Lupembe siyo tu cha kusaga majani ya chai na kupeleka Dar es Salaam kwa ajili ya *package*, majani ya chai yako Mkoa wa Njombe, Wilaya ya Njombe, Njombe *DC*. Kwa nini Kiwanda cha *Packaging* kisijengwe Lupembe kwa ajili ya wananchi wetu ili tuongeze ajira na mapato ya Halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, napongeza sana, ahsante na naunga mkono hotuba hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Swalle ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mheshimiwa Dkt. Florent Kyombo na Mheshimiwa Sebastian Kapufi ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi leo ya kuchangia katika Wizara ya Viwanda nikiwa kama Mjumbe wa Kamati na naunga hoja hotuba yote ya bajeti na maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikimpongeza Mheshimiwa Rais nataka dunia ijue, nchi ijue na wale wenzetu wajue sababu za kumpongeza. Mheshimiwa Rais amefufua kiwanda cha Kilimanjaro *Tools* kwa muda wa miaka 34, kiwanda hiki kilibinafsishwa kikakosa wawekezaji, lakini Mheshimiwa Rais amepeleka bilioni 1.6 ili kiwanda hicho kiende kifufuliwe na tulikitembelea sasa hivi kinafanya kazi, lakini akapeleka *TEMDO* bilioni moja na pointi kufufua Kiwanda cha *TEMDO*, akapeleka fedha *CAMARTEC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la ajabu sana alilofanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimeanza kazi madini mwaka 1988 nimelikuta Liganga na Mchuchuma ni kila siku tunajadili Liganda na Mchuchuma, baada ya miaka 36 nikiwa Mbunge kwenye Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania najadili Lichuchuma, Rais akiwa ametoa bilioni 15.4 kulipa fidia ili kazi isonge mbele, huyo ndiyo Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hizo fidia walizofanya na faida, jana Mbunge wa Ludewa amesema kwamba sasa mpaka wananchi wa kijiji kile wamenunuliwa Bima za Afya kupitia hiyo fidia, kwa sababu waliamua kuwekeza kwenye bondi za Serikali, bila fidia hizo wasingeweza kuwekeza, hizo ni kazi za Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Waziri Ashatu, wifi yangu, nakuamini sana, umekuwa bosi wangu Wizara ya Fedha, naamini utendaji wako, pia umepewa Naibu Waziri ambaye ni jasiri na mnyenyevu ambaye anakusikiliza. Juzi hapa Naibu Waziri wa Mifugo alisema ukiwa na Waziri ambaye ananuna nuna unashindwa hata kufanya kazi, lakini tumekuwa tukiwaona kwenye Kamati mnavyochekeana, mnavyosikilizana. Pia wakawapa Katibu Mkuu Dkt. Hashil ambaye hakika amekuwa ni mchezeshaji kiungo kati yenu wawili, kazi zake tunaziona zinavyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa namwambia Waziri kiutani kwamba naona ameiba Wizara ya Fedha yote, kuanzia Wakuu

wa Taasisi, Wakurugenzi wako pale, wote umechota wale kule na naamini kazi zinaenda sawasawa, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nina ushauri, nitaanza na Liganga. Siku moja hapa nilimwambia Mheshimiwa Aweso nikiwa Kamati ya Maji, nikamwambia Mheshimiwa Rais alivyoingia humu kuhutubia Bunge mara ya kwanza alimsimamisha na akamwambia Aweso ukinizingua nitakuzingua maji yasipofanikiwa, lakini tarehe 9 tukiwa Kigamboni kufungua kiwanda cha kuunganisha magari, Mheshimiwa Rais alimwambia Waziri wa Viwanda na Waziri wa Uwekezaji Kaka yangu Mkumbo, kwamba nataka Liganga na Mchuchuma ikaanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wakiweza ndiyo watakuwa salama lakini wakiichezea hiyo nafasi wanaweza wasiwe salama, kwa sababu neno la Rais ni maelekezo. Niwaombe sasa pale ambapo pamebaki kidogo pakukaa na mwekezaji waende wakakae tuone Liganga inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunataka Liganga ifanye kazi? Leo Kilimanjaro *Tools* inataka madini ya chuma, leo *TEMDO* wanataka madini ya chuma, kila kiwanda kinachoanza hapa kinataka madini ya chuma na tutayapata wapi? Ni Liganga na Mchuchuma, tunaomba waende wakafanye kazi. kama huyo Mwekezaji hawezi toa aanze majadiliano na mwekezaji mwingine, tunataka kuona wameacha alama, tunataka kura za kuanzia Iringa, Njombe na Ludewa, tusisumbuke ziletwe na Liganga, nawaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kwenye viwanda vyetu vya Kilimanjaro *Tools, TEMDO* na *CAMARTEC*. Viwanda hivi vinategemea sana vyuma chakavu, sasa niwaombe na kila siku wanasema hizi Wizara zishirikiane, mshirikiane na Wizara ya Uchukuzi, tusingependa kuona eti kule uchukuzi, bandarini, reli kuna watu wana tenda ndiyo za kununua vyuma badala ya kukipeleka Kilimanjaro *Tools*, *CAMARTEC* na *TEMDO* vikaendeleza hivi viwanda ambavyo Mama Samia amepeleka fedha kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *TEMDO*, *CAMARTEC* na *TIRDO* ndiyo wakanunue hivyo vyuma chakavu ambayo ndiyo rasilimali yao ya kutengenezea vifaa vinavyotengenezwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Bashe alithubutu hivyo viwanda vilivyokuwa vinasemwa jana vinavyojengwa na *TEMDO* kupitia Bodi ya Sukari, aliwawezesha milioni 200 ili watengeneze hivyo viwanda vya sukari huo ndiyo ushirikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ulinzi wamenunua majokofu kutoka *TEMDO*, majokofu ya kutumika kwenye *mortuary* zetu huo ndiyo ushirikishwaji kwa sababu tuna-*save* dola ambazo zingeenda kununua vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba tuangalie Sheria za Manunuzi. *MSD* wameenda *TEMDO* wamekagua vile vitu wanavyotengeneza, vitanda vya akinamama vya kujifungulia, viti vya kung’olea meno mahospitalini, lakini wanapoomba tenda *MSD* wanaambiwa hamuwezi kupata kwa sababu hamtengenezi *cylinder,* hamtengenezi *drip,* hamtengenezi vitu vingine, sasa tunajikwamisha wenyewe ni shida gani inayofanya tukwamishane hapa? kuna nini nyuma ya pazia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini msiwape tenda ya vitu wanavyotengeneza, hivyo vingine wakanunua sehemu nyingine tuka-*save* hela za kigeni ambazo tunaenda kuagiza vitu nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali twende tukaangalie hizo Sheria za Manunuzi ili kuweza kuokoa viwanda vyetu hivi ambavyo wanajitahidi na vitaweza kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya kuwapa vijana wetu ajira, viwanda hivi ndiyo vitakavyoleta ajira. Mfano, Kiwanda cha Kigamboni cha Kuunganisha Magari kina watumishi wa kudumu 250, kati ya hao wote watatu, ndiyo watumishi wa kigeni waliobaki ni Watanzania, watoto wetu waliosoma kwenye vyuo vyetu vikuu vya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaalam aliyepo *TEMDO* anayetengeneza majokofu hajawahi kusoma nje ya nchi. Ni mwanafunzi aliyesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mtanzania wetu hapa hapa. Kijana wetu hajawahi hata kutoka nje ya nchi, lakini anafanya maajabu sana pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuviwezeshe hivi viwanda kwa uwezo wa fedha. Niwaombe na Wizara ya fedha hii hela iliyobaki ya *Kilimanjaro Tools* iende, kwa sababu walipewa shilingi bilioni 1.7 sasa hivi zimeenda milioni 700 na *point*. Hizo zilizobaki ziende wale wakatengeneze hicho kiwanda. Pia, vifaa chakavu vikanunuliwe na viwanda hivi. Hatutapenda kuona eti kuna watu wana *tender* za kununua vyuma chakavu wakati ni malighafi inahitajika kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuma chakavu vitoke reli na bandari viende *Kilimanjaro Tools, TEMDO* na *CAMARTEC*. Pia, Wizara ya Mifugo kaangalieni hawa wanatengeneza pale mashine za kuchakata majani ya mifugo kwa bei rahisi ya shilingi milioni mbili. Kuliko waagize nje kwa nini wasiwape wale ile *tender* ndio wakatengeneza. Leo wamefungua mashamba ya *BBT* ya mifugo, wakanunua hizo mashine za kuchakata kwa hela ya Kitanzania ambayo haitatumia hela za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Serikali wachukue ushauri huo waende wakaufanyie kazi. Nia ya Mama Samia ni kufufua viwanda Tanzania. Kuna Mbunge jana amechangia akasema tufufue viwanda Tanzania, hatutavifufua kwa maneno ni kwa vitendo na ni kwa Wizara zetu hizi kushirikiana. Niwaombe waende washirikiane tufufue hivi viwanda vya Kitanzania ili watoto wa Kitanzania wapate kazi. Hili Mheshimiwa Dkt. Ashatu namwamini analiweza, *Professor* Mkumbo analiweza. Tunataka huo u-*Professor* wake tuuone kwenye vitendo na alipewa maelekezo na Mheshimiwa Rais. Tunataka tuone Liganga ikifanya kazi kaka yangu. Sisi tupo kumlindia kura zake Ubungo yeye achape kazi akafanye Liganga ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly James Ntate. Mheshimiwa Dkt. Florent Kyombo, Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Maryam Omar Said, wajiandae.

**MHE. DKT. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi ya kuwa miongoni mwa wachangiaji katika Wizara yetu ya Viwanda na Biashara. Kwa nafasi ya pekee nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ya kizalendo lakini na maendeleo ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, kwa kuweza kusimamia Wizara hii kwa weledi, pia tunaona kazi nzuri inayoendelea kufanyika ndani ya Wizara hii. Pia, anasaidiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Exaud Kigahe, Katibu Mkuu ndugu yetu Hashil Abdallah pamoja na watumishi wote ndani ya Wizara hii pamoja na Taasisi zote ambazo zipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea maeneo mawili. Suala la kwanza nitagusia mazingira ya biashara katika mikoa inayopakana na nchi za jirani. Pili, nitaongelea suala la bidhaa za chakula na vipodozi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba tu Taifa langu kwa upendo na mazingira mazuri ya biashara, tuweze kuangalia mazingira mazuri ya biashara hasa katika mikoa ambayo inapakana na nchi jirani. Nikichukulia mfano wa Mkoa ninaotoka Mkoa wa Kagera na mahususi Wilaya yangu ya Missenyi ndani ya Jimbo la Nkenge, nikijikita sana katika mpaka wangu wa Mtukula pamoja na mipaka inayofanana na mazingira ya namna hiyo, mazingira ya biashara katika maeneo hayo siyo mazuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha na wenzetu wa nchi za jirani maana yake hapo naamini mnaelewa Missenyi ipo karibu na nchi gani. Mazingira ya biashara kwa kweli kule yameboreshwa na mfanyabiashara yeyote anayeenda kufungua biashara, kwa kweli analelewa kama mtoto mdogo, ili biashara yake iweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza wana utaratibu ambao ukienda kufungua biashara unapewa kipindi cha maangalizi *(grace period)* ya zaidi ya miezi sita mpaka mwaka mzima. Wakati huo wataalam wa kibiashara wakiwa wanakutembelea kujua ni nini kinakusibu ili biashara yako iweze kukua huku wakikushauri biashara ya aina gani ambayo inaweza ikawekezwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Mtukula utashangaa. Ndani ya kilometa 10 za upande wa nchi jirani, zaidi ya 70% ya biashara iliyoko kule ni ya Watanzania. Wamekimbia huu upande wa Tanzania ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu mazingira yamekuwa ni magumu. Sasa, ushauri wangu kwa Serikali yangu pendwa niiombe, tunajua tuna sheria, kanuni na miongozo inayoendesha biashara zetu na mazingira ya biashara lakini ni vizuri tukatenga *segments* za kibiashara. Sisi tunacholenga ni kuhakikisha kwamba, tumepata mapato makubwa na nchi yetu imekusanya fedha za kutosha. Huo ndio msingi wa kwanza ambao tunahitaji. Kwa hiyo, tunaweza tukatenga *segment* kwamba ndani ya Mkoa wa Kagera, kwa sababu wapo karibu na nchi ambazo ni tatu zimezunguka pale Burundi Rwanda, Uganda tunaweza kuweka mazingira ya kibiashara ambayo siyo sawa na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine zinatumia utaratibu huo ili kuweza ku-*win* mazingira ya biashara ukilinganisha na nchi za jirani. Tukiendelea kukomaa kwamba sheria ni moja maeneo yote wakati mazingira ya biashara yanatofautiana, itaendelea kuturudisha nyuma na basi Tanzania itaendelea kubaki kama kichaka na mdororo wa biashara hasa katika mikoa ambayo inapakana na nchi za jiarani. Ukiangalia Mkoa wa Kagera kwa Wilaya za Missenyi, Kyerwa, Karagwe na Ngara basi watakuwa ni wahanga wakubwa pamoja na maeneo mengine. Kwa hiyo nishauri Idara yetu ya Biashara na sasa hivi imeboreshwa imepewa *full* idara. Wawe wenyewe ni watu wa kutoa elimu na kuelimisha wananchi wetu biashara gani watafanya. Mazingira haya yakiboreshwa, naamini biashara inaweza ikakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mji wangu wa Mtukula pale ni Mji ambao kikodi unakusanya kodi nyingi. Ukilinganisha na *border* nyingine unaweza kuwa wa kwanza, pili au wa tatu lakini mazingira ya biashara ya watu wetu pale Mtukula imebaki kama ni mahame watu wamehama. Wizara ya Ardhi imeenda pale imejenga jengo zuri la Kimataifa la *National Housing,* lakini leo ukienda pale wamebaki mle ndani wafanyabiashara wawili, wengine wote wamehamia upande wa Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lipo wazi twende pale waone mambo yanavyokwenda ili muweze kusaidia nchi yetu. Kwa hiyo, bado nasisitiza niwaombe sana mazingira ya biashara yakiwa mazuri wananchi wetu watafanya biashara upande wa Tanzania ambapo kuna amani na utulivu na biashara itakuwa huku nchi yetu itaendelea kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine la jirani na nchi zingine, kuna viwanda vyetu ambavyo vipo kwa sasa. Tuna *by product* ambazo zinazalishwa kutoka katika viwanda. *For instance,* mimi niongelee katika viwanda vya sukari. Bahati nzuri nilihudumu kama Mkurugenzi hapo Mvomero nikihudumia Kiwanda cha *Mtibwa Sugar* na sasa hivi ni Mbunge wa Missenyi ambako tuna *Kagera Sugar*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivyo vinazalisha *molasses*. Ile *molasses* ukiiangalia pale ni kama *by product* ambayo katika nchi yetu inakuwa kama haina maana, lakini nenda kwenye viwanda hivyo uone maelfu ya magari yanayosomba *molasses* kwenda nchi za jirani. Yakienda nchi za jirani wanatengeneza *spirit* ambayo inarudi Tanzania tunainunua kwa bei ghali. Sasa, unajiuliza *by product* unayo ndani ya nchi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa *molasses* ndiyo gharama na siyo kuuza. Ile *product* yenyewe inauzwa kwa bei ndogo sana kwa lita. Ukiangalia hata viwanda vinaona kama ni suala la kutupa. Kwa hiyo, niombe katika kazi nzuri ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Viwanda na Biashara na Wizara yetu ya Mipango na Uwekezaji, naamini haya mambo tuyaangalie kwa

kina ili chochote kinachopatikana Tanzania siyo tunamwachia jirani anafaidi halafu sisi tunaenda kununua kwa bei kubwa na wakati tungeweza kushawishi au kuleta uwekezaji wa viwanda ndani wakaweza kuweka viwanda vya kutengeneza *spirit*. Hizo *by product* zote najua hata huko Kilombero zinatoka zikatumika ndani ya nchi yetu na sisi tukapata faida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuomba Wizara ya Viwanda na Biashara iweze kujitenga na miundombinu ya barabara ambayo hasa inaboresha biashara. Kuna barabara ambazo ni muhimu sana kutuunganisha sisi na nchi za jirani. Ukiangalia baadhi ya nchi zinapokuwa hazina maelewano mazuri, sisi kwetu ni faida. Kwa hiyo, kuna barabara ambayo inatoka Nyakahanga kwenda Benako inaunganisha kuja mpaka Karagwe na Mtukula. Ni barabara nzuri ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati tunataka kufungua njia za kibiashara niombe sana, tujikite kuhakikisha miundombinu kama hiyo Serikali inawekea kipaumbele. Tufungue hizo njia ili sasa tuweze kupata njia nzuri ambayo wafanyabiashara wetu wanapita kwenda nchi za jirani ili biashara zao ziweze kwenda vizuri, lakini na sisi tozo tunazotoza ziweze kuwa ni faida kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, niseme nimeapa kusema ukweli na ukweli nitashauri pale inapobidi. Pia, mimi ni mtumishi wa afya, niliapa viapo vyangu vya maadili ya kiutumishi. Pale ambapo naona jambo haliendi sawa, nitaendelea kushauri mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia *TBS* kwa suala la viwango wanafanya kazi vizuri iliyotukuka. Ni kazi nzuri mno ambayo kwa kweli na wenyewe wanashauri pia na *ZBS* ya Zanzibar; kazi ni nzuri. Mimi hapa nipo kusimama kwa ajili ya *public safety* nikiangalia *quality* na *safety* ya bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa tunajibu hizi hoja tunachanganya mambo. Katika kuchanganya hapo tunaangalia

maslahi ya ukusanyaji wa maduhuli *against public safety.* Afya ya mwananchi siyo ya kuchezea hata kidogo. Nikishaathirika leo na chakula au vipodozi, hakuna sehemu yoyote unaweza ukanirudishia afya yangu. Sasa niombe, Serikali ni moja, maduhuli yanayokusanywa yanaenda Serikali Kuu, ambayo ni moja, yakusanywe na nani? Siyo suala la kuulizana. Tunachoulizia ni afya ya mwananchi inalindwaje kuhakikisha mwananchi anaendelea kuwa na afya njema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeendelea kuchangia nikasema wenzangu tuangalie *best practice* ya kidunia, kikanda na kimataifa inasemaje. Tukianza kujikita kwenye mambo kwamba, sisi tumeamua kufanya hivi siyo jambo la ukweli. Nikawaambia twende hapo Zanzibar kama basi ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Leo *ZFDA* inasimamia vyakula na vipodozi lakini Bara ni tofauti ambaye Bara ndio amemzaa Zanzibar, *ZBS* kule inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waende wasome *blue print* zipo *paragraph* kibao za kusoma, nikizitaja; *paragraph* 32, 33 na kuendelea. Wasome *Performance Audit Reports* za *CAG*. Nchi yetu tunataka iende katika mustakabli wa kulinda afya za wananchi. Mheshimiwa Rais anasaidia wananchi kwa kuleta Bima ya Afya kwa Wote, siyo kutibu magonjwa yanayosababishwa na bidhaa ambazo hazijadhibitiwa zipo sokoni. Leo unaona Jack Daniels feki zipo mtaani zinasambaa na vipodozi watu wanajipaka wanaathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali iendelee kujikita…

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wake umekwisha Mheshimiwa, mwache amalizie.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wake umekwisha Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. DKT. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kujikita katika kuhakikisha kwamba, inasimamia utaratibu huu unakuwa mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nishukuru sana Serikali yangu, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent Kyombo, ila Zanzibar haikuzaliwa na Bara. Zanzibar na Bara zote zimezaliwa. *(Kicheko)*

Nilimtaja Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Maryam Omar Said wakati huo Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nitajikita katika maeneo machache. Kama ilivyo ada na nianze kwa kumpongeza Rais wangu Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatamani kwenda kwenye mapitio ya jumla ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambapo lipo eneo la *BRELA*. Katika eneo hili niwapongeze na niseme jambo moja. Mheshimiwa Waziri kama ambavyo umekuwa ukitoa elimu kwa watu wengine ikiwa ni pamoja na Wabunge, naomba uende mbali zaidi elimu kwa watu wetu kuhusiana na kazi za *BRELA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu nimeona wanasema usajili kwa kutumia mfumo wa kielektroniki. Zamani zoezi lilichukua wiki tatu za usajili wa kampuni na jina la biashara wiki mbili, lakini kwa kupitia mfumo zoezi hilo limekuwa ni siku moja hadi tatu. Haya ni maendeleo kwa maana ya kazi inayofanywa na *BRELA*. Elimu hii iendelee kupelekwa kwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa tunalolihitaji kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, sisi kama nchi kile kitu wanaita *ease of doing business,* niliombe sana hilo. Nchi yetu hapo eneo hilo tunapata tabu kidogo. Hayo ya jumla pia nafurahi kwenye lile lililokuwa

kwamba Sekta ya Viwanda na Biashara wameenda kuigusa hiyo sekta ya watu binafsi wakiamini uwekezaji wa mitaji ya watu wetu hawa wa binafsi. Hili limenigusa likanifanya nitoke hapo nirudi jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimboni kwa ujumla wake Mheshimiwa Waziri wewe na Wizara yako ni walezi wa wafanyabiashara. Tarehe 6 Mei, Jimboni Katavi, Mpanda kulitokea taharuki kubwa Mheshimiwa Waziri. Asubuhi wafanyabiashara wa maduka ya jumla waligoma wakaamua kufunga maduka. Nipo Bungeni nikifanya kazi ya kibunge, Mwenyekiti wao akanipigia simu akaniambia tumegoma kutoa huduma Mji wa Mpanda. Nikauliza kulikoni? Akaniambia yaliyopelekea tugome ni pamoja na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamejikuta mfanyabiashara anaweza akatoka Mpanda anakwenda Dar es Salaam, ili akafunge mzigo anakwenda anakuta akaunti imefungwa. Mfanyabiashara anajikuta analetewa madeni asiyoyafahamu. Hiyo kama haitoshi kwa maana ya watu wa *TRA* sambamba na malimbikizo ya kodi za zamani nyingi. Yote haya lakini suala la kwamba akaunti yake imefungwa wanasema tutafanyaje kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara hawa ni wadau muhimu kwenye Sekta nzima ya Biashara. Nililiangalia hilo nikasema kama hawa watu siyo muhimu, ile siku moja tu wamefunga biashara kukawa na sintofahamu katika Mji wetu wa Mpanda. Mimi mwakilishi nipo Bungeni, sintofahamu imetokea mpanda, wengine wanafika sehemu Mbunge wetu mbona hatukuoni katika hili? Kwa hiyo, unachonganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *TRA* niwaombe, hakuna ugomvi kati ya wao na wafanyabiashara, sisi wote tunahitajiana. Kwa hiyo, niwaombe sana katika hili. Huko nyuma tuliwahi kuambiwa hakuna siku utakuta watu wa *TRA* wameenda kufunga makufuli kwenye maduka ya wafanyabishara zaidi ya kukaa na kusikilizana. Niombe turudi kwenye meza ya mazungumzo ili tuendelee kutoa huduma kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, natamani sana niendelee kusema katika *angle* moja ya mapinduzi ya viwanda. Nilikuwa nikipitia pitia hapa nikakumbushwa tunaambiwa kwa maana ya mapinduzi ya viwanda. Awali kabisa mwaka 1760 mpaka 1830 tulikuwa tunazungumzia habari ya mashine za mvuke *(steam engines)* na kazi kubwa ilikuwa ni utengenezaji wa nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuja karne ya 19 mpaka ya 20 mapinduzi ya pili; hayo ya kwanza ndio niliyoyasema. Yale ya pili ilikuwa ni kwa maana ya maendeleo ya umeme. Tukatoka hapo kwa maana ya maendeleo ya umeme, uzalishaji ulikuwa ni mwingi na mashirika ya kisasa. Tukaja mapinduzi ya tatu katikati ya karne ya 20 ilikuwa ni maendeleo ya kompyuta, elektroniki, uzalishaji wa *automatic* na uchumi wa kidijiti. Leo Mheshimiwa Waziri tupo mapinduzi ya nne. Mheshimiwa Waziri tunaambiwa ni pamoja na akili bandia, roboti, mtandao wa vitu na *data* kubwa ambayo kwa ujumla wake imebadilisha maisha ya watu na jinsi tunavyoishi, jinsi ya kufanya kazi na kuingiliana na ulimwengu unaotuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo bila kuyaangalia haya mapinduzi kuanzia ya kwanza, pili, tatu na leo tupo ya nne ya viwanda, yote tunayoyazungumza itakuwa ni kazi bure. Ni kwa nini nalisema hili? Ukija kwa maana ya haya mapinduzi ya nne tuliyoyasema, leo kwa mapinduzi haya ya nne ambayo yanagusa suala la akili bandia na masuala ya roboti, mtandao wa vitu na *data* kubwa, biashara nyingine *automatically;* nitakupa mfano mmoja kwa maana ya biashara mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kampuni ambazo kwa wakati fulani zilikuwa zinazalisha nakala ngumu, leo zimejikuta zinafanya biashara nzuri kwa kuzalisha nakala tepe na watu wengi ambao walizoea kwamba, lazima tukutane na nakala ngumu wamekwenda kwenye nakala tepe. Hilo huwezi ukalikwepa. Ni lazima watu wetu tutakapokuwa tukiongelea biashara tukumbuke kwamba, tupo kwenye mapinduzi ya nne. Muda wote tuliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzalishaji wa bidhaa mitandaoni. Leo unaweza ukakaa umetandaza nguo zote hapa lakini mwenzako amekaa tu ndani kwa kupitia mapinduzi ya nne, kupitia mitandao akajikuta anafanya biashara. Nataka kusema nini? Tuwaelekeze watu wetu huko na leo nimefurahi kusikia watu wakiongelea Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa tunapitishwa kwenye semina ya haki rasilimali, wakatwambia pamoja na kuangalia, kwa mfano *LNG,* gesi yetu huko Lindi, lakini bado taasisi za kimataifa wanakwambia uzalishaji huo unakwenda pamoja na masuala haya ya tabianchi. Sasa, nataka kusema hivi, tukichelewa matumizi ya rasilimali tulizonazo tunakutana na vikwazo vingine hivi vya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watakwambia labda hatuhitaji matumizi ya makaa ya mawe. Leo teknolojia inabadilika, nilikuwa nawaambia hata watu wangu katika eneo la machimbo ya madini kama dhahabu; leo mtu anaweza akaenda kwenye shughuli akamaliza shughuli yake, ukimwona amevaa amependeza ana pete, ana mkufu, lakini ni *artificial gold,* si *gold* hii ambayo tunachimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusipokuwa makini tutaendelea kujisifu kwamba tuna rasilimali ya kutosha, lakini ambayo wakati mwingine imepitwa na wakati, kwa maana ya teknolojia. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri tusiache kuliangalia hilo, kwa maana ya dunia inakwenda wapi na masuala mengine kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifarijika Waziri alipozungumzia suala la intelijensia ya masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini kwenye masoko ya kimkakati.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, muda wako umekwisha.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nampisha Mheshimiwa Naibu Spika ili aweze kuendelea na shughuli za Bunge. *(Makofi)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Omar Said. Mheshimiwa Sichalwe. Mheshimiwa Sichalwe, si umo kwenye orodha? Mheshimiwa Kunti. Sasa unachangia au bado unapiga *Albadri*? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Orodha yangu ilikuwa ya mwishoni, kwa hiyo nilikuwa nimejiandaa kwa mwishoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara nailinganisha na Wizara ya Kilimo kwa sababu Watanzania wengi kwenye sekta hii, mtu yeyote anaweza akajiajiri hata pasipokuwa na elimu. Watu wa elimu ya kawaida wanaweza wakafanya biashara, watu ambao hawajasoma kabisa wanaweza wakafanya biashara, wasomi wenye elimu kubwa wanaweza wakafanya biashara. Pia, hata wale watu ambao hawajasoma ambao wamepewa uwezo na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuvumbua mambo kadhaa wanaweza wakaleta mawazo mazuri ambayo yanaweza yakaleta mambo ya ubunifu kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja mbili tu kwa siku ya leo. Hoja ya kwanza ni kuhusiana na masoko kwenye wizara hii. Kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusiana na masoko hususan kwenye Nchi za *SADC* na hapa nikiongelea zaidi Nchi ya *DRC*, kwenye eneo hili siwezi kuwalaumu watu wa Viwanda na Biashara. Hii ni kwa sababu kuna mazingira ambayo wanapaswa kuwekewa na yaweze kutekelezeka ndipo wao waweze kusimamia vizuri eneo la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeboresha bandari zetu nyingi. Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Tanga na vilevile tunaendelea na ujenzi wa reli ya *SGR*. Tumeboresha pia bandari nyingi sana ambazo ziko kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika. Tumejenga Bandari kubwa sana ya Karema kwa zaidi ya shilingi bilioni 49; na bandari zingine zimeboreshwa. Ilipo Bandari ya Karema ambayo ina zaidi ya shilingi bilioni 49 kuelekea upande wa *DRC* kuna mji unaitwa Moba. Kutoka Moba kwenda Katanga, ambao ni Mji wa Lubumbashi na jimbo lingine ambalo linaendelea, Lualaba, ni kilometa 1,100. Ni kama mwendo pungufu kutoka Dar es Salaam kwenda Tunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Waziri wa Viwanda na Biashara; iko haja ya kukaa na Wizara ya Uchukuzi na kutafuta namna ya kushirikiana na Nchi ya *DRC* tuweze kuwajengea barabara kwa mapatano. Tunaweza tukawawekea *gate toll,* tukaendelea kulipisha zile barabara na hivyo tutaweza kurejesha pesa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ambayo tutaitumia kujenga barabara na matokeo ambayo tutayapata ni makubwa kuliko gharama ya barabara. Tusiendelee kusema kwamba *DRC* haipitiki. *As we are speaking now*, *China* wamejenga *railway* yao kutoka Angola mpaka Kolowezi kwenda Lubumbashi. Kwa hiyo, kama sisi *DRC* tunapakana nao kwa karibu, siku za usoni zinazokuja badala sisi tuwapelekee *DRC* bidhaa, wao watatuletea kwa sababu *Chinese* watatumia hiyo njia kutuletea sisi baada ya kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia vizuri kwenye wizara zinazokuja ili nitoe vizuri ufafanuzi. Sasa nahamia kwenye hoja ya pili. Kwenye Wizara hii ya Viwanda na Biashara wakati mwingine nawaona *SIDO* hawajafanya kazi yao kikamilifu. Katika hili namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kuna hoja yangu moja hapa nimekuwa muda wote nikichangia inaonekana kama ni *funny story*. Najua Waziri yeye anafahamu. Aende kwenye taarifa za *TRA* watuambie, vinywaji vikali ambavyo vimeingia nchini vimeingiza pesa kiasi gani kutoka kwenye mataifa mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu liko hapa, kama vinywaji vingine vikali vinaweza vikaruhusiwa kuingia nchini kwetu na watumiaji ni Watanzania hawa hawa ambao wanaendelea kutumia hivyo vinywaji vikali, shida iko wapi pale ambapo Watanzania hawa hawa kwa uwezo ambao wamepewa na Mwenyezi Mungu wanaweza wakabuni mawazo ya kutengeneza vinywaji hivyo hivyo vikali; lakini badala ya *SIDO* na Wizara ya Viwanda na Biashara kuyachukua yale mawazo yao kuwasaidia tu kuwatafutia mtambo wa kuweza kutofautisha *methanol* na *ethanol* ili tuweze kupata vinywaji vikali, yaani Wizara ya Viwanda na Biashara wameshindwa jambo hili, lakini wako tayari kuendelea kuruhusu vinywaji vikali viendelee kuja na viendelee kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji mmoja alisema hapa jana kwamba, ukienda kule *China* ni kweli utakuta hata watoto wadogo, wabibi wanafanya shughuli kuendelea kupaki bidhaa kutuleta nchini kwetu. Kama sisi mawazo ambayo Watanzania wanaweza wakawa nayo wao wenyewe, yakaboreshwa na sisi tukatengeneza vinywaji vikali tukauza nchini, shida iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwaomba watu wa *TBL (Tanzania Breweries)* pamoja na watu wa Konyagi, kama Serikali imeona haiwezi kuwasaidia Watanzania kutenganisha *methanol* na *ethanol* iliyoko kwenye gongo, basi watu wa Konyagi wachukue hiyo fursa waende kule vijijini wakatumike kama wanunua malighafi ili wajipatie bidhaa mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine najiuliza, niliongea na mtu mmoja mtumia pombe, mimi situmii pombe, nilikuwa namuuliza kuhusiana na pombe moja wanaita *Amarula*, wanatengeneza kwa kutumia maziwa. Yaani ng'ombe wote walioko hapa nchini wa Mheshimiwa Ulega ambao tunaweza tukakamua maziwa ya kutosha, kweli tumeshindwa kuchukua gongo ya Watanzania tukachukua na maziwa yetu tukatengeneza na sisi tukapata *Tanzaniarula* yetu ili watu wakaona hii ni *Amarula* ambayo imetoka huko nchi inakozalishwa na hii ni pombe yetu kutoka kwenye maziwa yetu wenyewe,

pamoja pombe zetu wenyewe kama Gongo ambazo zinatengenezwa kwa kutumia mahindi na kwa kutumia mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1987 kuna mwanamuziki mmoja kutoka Nchi ya *South Africa* (Yvonne Chaka Chaka) alitoka na kibao chake kimoja kikali kilikuwa kinaitwa *Umqombothi* akautangazia umma na dunia, akaiimba pombe yao ambayo inatengenezwa kule Nchini *South Africa*. Dunia nzima na Wazungu wakajua kwamba kuna pombe inaitwa *Umqombothi* inawaburudisha watu wa *South Africa* na Waafrika wanafurahia kinywaji chao, lakini sisi tukija hapa tukisema gongo unaonekana wewe ndiyo mshamba, yaani inaonekana kama na shuleni sijaenda. Hapana na shuleni nimeenda, lakini ni mawazo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *jeans* zinaweza zikaingizwa kutoka nchi za mbali, Watanzania wa kawaida wakatengeneza *jeans* hapa, kuna shida gani kuziboresha hizo *jeans*? Huu umekuwa karibu ni mwaka wa nne nimekuwa nampa hoja hiyo hiyo Mheshimiwa Waziri, yaani hawana mtambo wa kwenda kutenganisha *ethanol* na *methanol* kwenye gongo ili kiwe ni kinywaji halali ili kitumike? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshaongea na watu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakasema wana maandiko mengi ambayo wameandika kuhusu gongo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Si waende wakakae nao wawasaidie ili gongo iweze kuhalalishwa ... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa umeingia humu ndani na hivyo vitu? Maana nakwambia ahsante unaendelea tu. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa sijasikia.

**NAIBU SPIKA:** Hujasikia! Utasikiaje na tayari? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Kunti na Mheshimiwa Gwajima wajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa. Suala la kwanza ni mambo ya kiujumla kwamba, Wizara inaomba shilingi bilioni 110.899 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha. Sina tatizo na hilo na naamini kwamba hizo fedha zinawatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, napongeza sana Serikali kuyapata masoko ya Saudi Arabia, *Qatar* pamoja na Falme za Kiarabu kwa ajili ya kuuza nyama nje na mauzo yetu ya nyama kule nje sasa yamefikia tani 4,997.7 ambayo yana thamani ya shilingi bilioni 56.78. Huu ni ushindi mkubwa kwa Serikali kwa sababu tulitaka iwe hivi. Kampuni hiyo ya *Tan Choice* pamoja na *Eliya Food Industry*, tunawapongeza sana kwa hatua hiyo waliyofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu katika mambo ya kiujumla ni muungano wa kampuni, yaani zile kampuni zinapo-*merge*. Taarifa ya Waziri inasema kwamba zaidi ya kampuni 65 zimeungana bila taarifa ya *FCC*. Sasa unajiuliza yaliwezaje kuungana bila taarifa ya *FCC* kwa sababu muungano wowote ule wa kampuni unaruhusiwa na *BRELA*. Sasa, *BRELA* anawezaje kuruhusu muungano wa kampuni bila kibali cha *FCC* katika taarifa ya Waziri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kuliongelea kwenye mambo ya kiujumla, jambo la nne katika mambo ya kiujumla, Waziri wa Viwanda ameeleza kuwa, mauzo ya nje katika masoko ya Ulaya, *EAC, SADC, AGOA* pamoja na Bara la *Asia* yamepungua kwa trilioni 2.851 katika mwaka wa 2023. Waziri wa Kilimo alipoleta taarifa yake hapa alitueleza kwamba katika masoko hayo mauzo ya nje yaliongezeka kwa

trilioni 2.86. Je, ni nini chanzo cha mgongano huo wa takwimu kwa Mawaziri hawa wawili katika kipindi hicho kimoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika kipengele cha tatu ni kuhusu suala la msamaha wa kodi. Tumekuwa tukiletewa hapa misamaha ya kodi, tukiombwa msamaha wa kodi ili kuweza kuchochea uwekezaji, mauzo nje, kuchochea ajira ziweze kupatikana kwa wingi, lakini na kuwasaidia wananchi wetu kupata bei nafuu ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kuongeza mauzo nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, utapitia hotuba ya Waziri yote, mwaka jana tumefanya msamaha na miaka iliyopita tumefanya msamaha. Huwezi kupata tathmini ya msamaha huo, kwamba tulipotoa msamaha hapa kama Bunge tumeleta tija gani? Imeajiri Watanzania wangapi? Tumevutia uwekezaji na kuingiza mtaji wa kiasi gani ndani ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili lisipotumika vizuri na tusipopata *feedback* sisi kama wawakilishi wa wananchi, tulitoa hicho kibali cha kutoa msamaha, leo hatuambiwi huo msamaha una tija gani. Leo hatuambiwi faida ya huo msamaha ni nini. Tumenufaisha nini. Tusipofanya hivyo na Bunge linalokuja hili tutaomba msamaha tena tubariki msamaha mwingine. Tukiendelea na mtindo huo, Wabunge tukaendelea kutoa huu msamaha bila kudai kufanyiwa tathmini, hili eneo la msamaha wa kodi linaweza likatumika kama eneo la biashara kama biashara nyingine ambazo zinafanywa na baadhi ya Watendaji wa Serikali na watu binafsi na baadhi ya Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka nchi yetu kwa sasa hivi iko nyuma sana katika ukusanyaji wa kodi. Tuna 12.5% ya pato la Taifa, ndiyo kodi tunayokusanya, ikilinganishwa na Nchi za wenzetu za Kenya na Rwanda ambao wako kuanzia 15% hadi 16% na kuendelea. Hii changamoto ni kutokana na moja ya msamaha huu wa kiholela na vitu vingine. Kwa mfano, tuliwahi kusamehe hapa kodi ya uunganishaji wa matela, nadhani na haya magari yanayounganishwa. Haya magari yanaletwa yakiwa yamekamilika. Kinachofanyika wakifika hapa, wanashika

spana tu lakini unawaondolea kodi, unawasamehe kodi halafu unaenda kutoza kodi ya muunganishaji wa pikipiki, muunganishaji wa baiskeli, muunganishaji wa bajaji, huyu anatozwa kodi,; huyu mwenye gari kodi hapana, huyu mwenye tela hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi kodi zinakuwa hazina usawa na tunakuwa hatutendi haki kwa wananchi wetu na mwisho wa siku hata ukiangalia, tumevutia uwekezaji gani katika hizo kampuni mbili zinazounganisha gari hapa? Waziri ametueleza hapa ni shilingi bilioni 75, lakini zote ni kampuni za nje, je, kampuni zetu za ndani haziwezi kufanya biashara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaambiwa kusamehe kodi ya wawekezaji mahiri tangu tuwaruhusu wawekezaji mahiri kusamehewa kodi, wameleta tija gani? Wameongeza kiasi gani? Ni kampuni gani hizo mpaka sasa hivi zilizosamehewa kodi? Ukienda pia katika *transfer price* na kwenyewe tuliondoa 100% ya msamaha hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha wa namna hii ambayo sisi kama Wabunge hatuletewi taarifa ya msamaha unaoombwa, inaweza ikatumika vibaya kama nilivyosema na kusababisha nchi yetu kukosa mapato; lakini kuwasaidia watu tu kwa sababu inaweza ikatumika kama biashara tu, kwamba, bwana wewe tutakusamehe kodi. Fanya hivi sisi tukusamehe kodi. Ni mambo ambayo hayakubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ilikuwa ni Serikali kufuta faini ya 15% katika utaratibu wa *PVOC*. Tuliufuta huu utaratibu na mwaka jana Wabunge tulilalamika sana kufutwa kwa utaratibu huu *PVOC*. Leo Waziri ameshindwa kutueleza imepatikana tija gani katika kuufuta utaratibu wa *PVOC*? Tumepata tija gani kama Taifa? Hatimaye ni nini kilichotokea? Tumefuta utaratibu huu *TBS* ikiwa haijajiandaa vya kutosha, haina maabara za kutosha na haina watumishi wa kutosha. Matokeo yake nchi yetu imegeuka kuwa jalala la bidhaa *fake* na bandia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBS* ina hawa ma-*vender* wanaotoa hizo *services* katika hayo maeneo husika na wana mikataba nayo na moja ya kinga ilikuwa ni hiyo 15%. Leo tumeiondoa mikataba hiyo, matokeo yake *TBS* anaweza akashtakiwa wakati wowote na hizo kampuni kama sababu hiyo 15% ndiyo ilikuwa kinga yao ya kuzuia watu kusafirisha bidhaa kutoka nje ya nchi kabla hazijakaguliwa, leo tumeiondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu sasa tunaigeuza kuwa jalala na watu wanaweza kuikimbia, kwa sababu kama huna mifumo mizuri ya udhibiti na unaondoa mifumo ya udhibiti kwa makusudi unategemea nini? Nchi yetu imegeuka kuwa jalala na hakuna tathmini iliyofanywa mpaka sasa hivi tumepata tija gani. Ukweli ni kwamba bidhaa *fake* zimetapakaa kila sehemu. Wananchi wetu wanaumia wananunua vifaa vya umeme *fake*, wananunua matairi *fake*, wanapata ajali za hapa na pale. Mpaka pikipiki *fake* kwenye nchi hii zipo na watu wanapata matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu biashara ya mbolea hapa nchini. Biashara ya mbolea hapa nchini inavyoendelea hivi sasa, tulikubali kama nchi kutoa ruzuku ya mbolea, leo walioenda kunufaika na ruzuku hiyo ni 25% tu ya wakulima wanaotakiwa kupata mbolea; ni 25% ya wananchi wanaotakiwa kunufaika na mbolea hiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa. Mheshimiwa Mpina kuna taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi na kwa mchango kwa Mheshimiwa Mbunge. Nataka tu kutoa taarifa moja ili aendelee vizuri, kuhusu suala la *strategic investors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ni kwamba, utaratibu kwa *strategic investors* ni kwamba, mwombaji anaomba *TIC*. Ipo Kamati ya Kisheria ambayo inaundwa kwa Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2002. Mwenyekiti wake ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha. Inakwenda kwenye *NISC*. *NISC* Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Waziri Mkuu na hatimaye inakwenda kwenye *Cabinet*. Ikishaidhinishwa na *Cabinet* imeisha, hivyo ndivyo utaratibu wa sheria ulivyo, kwa hivyo utaratibu wa kuleta Bungeni haupo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina taarifa hiyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake siipokei na hapa ninachotaka, tunataka uwazi, tunapotoa misamaha kama hii tunataka uwazi, uwazi huo yeye leo hii angetueleza toka tutoe huo msamaha ni watu gani walionufaika katika maeneo gani, ndiyo hicho ninachotaka. Huwezi ukasema Bunge halitakiwi kujua, kama halitakiwi kujua kwa nini alikuja kuomba hapa kibali cha yeye kwenda kutoa misamaha hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee muda nimalizie hicho kipengele changu cha mwisho sasa kwa kusema kwamba, sasa tuiruhusu Serikali kutoa mbolea ya ruzuku, wanaonufaika sasa hivi na mbolea ya ruzuku ni 25% tu ya Watanzania wote waliojiandikisha kupata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, ahsante, muda wako umekwisha. Tukikuongezea utachukua muda wa mtu mwingine, kwa hiyo, Mheshimiwa Mpina, ahsante.

Nilishamwita Mheshimiwa Kunti, wajiandae Mheshimiwa Gwajima na Mheshimiwa Ng'wasi.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia muda niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii. Naomba nianze na suala zima la leseni, Mheshimiwa Waziri mwaka jana nilichangia hapa suala zima la

uwepo wa leseni moja kwa wafanyabiashara wetu, lakini wakati wa Taarifa za Kamati pia nilitoa mchango wangu kwamba Serikali na Wizara waone sasa kuna haja ya mfanyabiashara ambaye ana biashara zaidi ya moja kuwa na leseni moja badala ya kumsumbua mfanyabiashara kuwa na leseni zaidi ya moja kwenye biashara zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala zima la uwepo wa taasisi mbalimbali ambazo zinatoza tozo mbalimbali ili huyu mfanyabiashara aweze kupata huduma. Nalo hili nililisema na nikatoa ushauri hapa ndani kwamba, Serikali ione sasa tuwe na kituo jumuishi ili mwananchi huyu anapokata leseni, anapopata *TIN* ajumuishiwe na hizo taasisi zingine kama *OSHA*, kama *Fire* na watu wengine wote ili iweze kufanyika kwenye eneo moja lakini pia alipe malipo yale kwa mara moja badala ya kuwa tunamsumbua, watu mbalimbali na kwa wakati tofauti tofauti kwenda kumdai hizo tozo na hiyo michango mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo natamani kulisema ni suala zima la wakala wa vipimo, Wizara ya Viwanda wana Taasisi ya Wakala wa Vipimo Tanzania. Tuna changamoto kubwa sana kuhusiana na suala zima la vipimo hususani kwa wakulima wetu waliopo vijijini. Wakulima wetu waliopo vijijini hawatumii vipimo, wafanyabiashara wanakwenda na vipimo vyao wanavyovijua wao, kusababisha wakulima wetu kupata hasara na kulima kilimo kisichokuwa na tija. Sasa taasisi hii ipo kwa Mheshimiwa Waziri, tuombe hii taasisi ishuke chini iende ikatoe elimu kwa wananchi wetu ili waweze kutumia vipimo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, washirikiane na TAMISEMI, tuna watendaji wa kata ambao wanawakaribisha hao wafanyabiashara kule chini, wahakikishe hawa wafanyabiashara wanapoenda kule chini wawambie wananchi wetu waweze kwenda na vipimo kwa maana ya mizani ili wananchi wetu waweze kuuza mazao yao kwa mizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja itatupa faida kwa sababu halmashauri zetu zitapa mapato stahiki, lakini pili na mkulima naye atanufaika. Kwenye suala la vipimo hivyo isiende kwenye mazao

tu, hata mifugo pia bado tuna changamoto sana. Ng'ombe anaenda kuuzwa mnadani anaangaliwa kwa sura badala ya kupimwa, kwa hiyo, hilo nalo pia tuone kwenye suala zima la vipimo, tunaomba watu wa Mheshimiwa Waziri waweze kushuka chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala zima la stakabadhi ghalani. Watu hawa wanafanya kazi kubwa, lakini bado *speed* yao ni ndogo, uwepo wa maghala bado ni changamoto na kibaya maeneo mengine bado wanajenga maghala mjini, wameacha kujenga maghala vijijini ambako ndipo mazao yetu yanapotokea. Kwa hiyo, niombe Wizara ya Viwanda pamoja na Wizara ya Kilimo waone wanashirikianaje kujua zao hili lipo wapi na wananchi wakajengewe maghala kwenye maeneo yao ambapo mazao yao yanatoka badala ya kuendelea kuwajengea wananchi maghala ambayo maeneo ni mbali, lakini pia wanatumia gharama kubwa na upotevu pia wa mazao unakuwa ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitamani kulisema ni suala zima la *TFDA* pamoja na *TBS*, nilikuwa najaribu tu kujitafakarisha mwenyewe, nikawa najaribu chanzo ambacho kilisababisha *TFDA* kwenda *TBS* ni kama huu mchakato niliousema hapa kwamba mwananchi huyu anatakiwa kwenda *TRA* akachukue *TIN*, mwananchi huyu anatakiwa kwenda manispaa akachukue leseni, mwananchi huyu anatakiwa kwenda *OSHA*, mwananchi huyu anatakiwa kwenda *Fire*, mwananchi huyu sijui anatakiwa kwenda wapi, hii milolongo yote, moja inapoteza muda, lakini pia na gharama zinakuwa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tukaishauri kwamba kwa kuwa wafanyabiashara wetu wa mazao wanapata tabu aende *TFDA,* Wizara ya Afya apeleke sampuli, atoke arudi *TBS* apeleke sampuli, huu muda anaoupoteza na hizi tozo hapa kwa kuwa hiki mwisho wa siku *TBS* ndiyo anayetoa ridhaa ya kwamba kitu hiki kipo salama na kimeshathibitishwa na nchi yetu. Ni kwa nini watu hawa wa *TFDA* wasitoke huku wakaenda *TBS* ili watu hawa wakafanya kazi kwa pamoja na mwananchi huyu mmoja

tukamwokolea gharama, lakini pili tukamwokolea muda? Sasa kuna mvutano hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani tujue hivi baada ya *TFDA* kutoka Wizara ya Afya na kwenda *TBS* ni athari kiasi gani iliyotokea kiasi kwamba tunatamani tuirudishe huko ilipotoka, mimi nadhani Serikali mje hapa mtuambie kwamba ni athari gani ambayo imetokea kuitoa *TFDA,* Wizara ya Afya kwenda *TBS* ni lazima kuwe na madhara ili ndiyo tuweze kuona hiyo kitu kuna maana ya kurudi tena Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo natamani kulisema hili ni suala zima la biashara zetu kwa wafanyabiashara wote. Tunafahamu fika kwamba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara wewe ndiyo uliyebeba dhamana na sera ya nchi hii kuhusiana na viwanda na kuhusiana na biashara, lakini ukiangalia watu hawa wote hawapo mikononi mwa Waziri, sasa shida hapa hatuombi muunganiko baina yake pamoja na wizara zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaombe wao ni Serikali moja na hawa wafanyabiashara na hawa watu wa viwanda wao wana wajibu, hakuna mfanyabiashara anayejua leo kwamba yeye hahusiki. Kwa hiyo ni wajibu wake yeye kuona namna gani wanashirikiana na TAMISEMI ili wafanyabiashara wetu wadogo wadogo kwa maana ya Wamachinga wanapata maeneo salama na yenye ubora, yenye hadhi ili vijana wetu na akinamama na watu wengine waweze kufanya biashara kwenye mazingira rafiki, badala yake tuna kazi ya kutupiana mpira ambao mwisho wa siku hautuletei tija sana kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye suala la viwanda halikadhalika, wananchi na Wabunge Mheshimiwa Waziri amewasikia hapa wanavyolalamika, akija hapa tukimwambia Kiwanda cha Sukari atatuambia kipo kwa Bashe, tukimwambia Kiwanda cha Nyama atatuambia kipo kwa Ulega, wakati yeye ndiye amebeba hiyo dhamana ya viwanda. Kuna changamoto kubwa kwenye viwanda vyetu hususani kwenye suala zima la wafanyakazi, bado wafanyakazi wanaofanya kazi viwandani

hawapatiwi vitendea kazi vinavyostahili, lakini hata malipo yao bado ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri ndiye aliyebeba hiyo dhamana, yeye ndiye anayesimamia hiyo sera atusaidie na alisaidie Taifa hili kuhakikisha wafanyabiashara na watoto wetu wanaofanya kazi viwandani wanapatiwa haki zao kwa kushirikiana na Wizara zingine ambazo wanakuwa na huo muunganiko ili tuweze kuleta tija kwa Taifa letu, lakini na maslahi mapana kwa Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, japokuwa siyo kwa umuhimu ni suala zima la uwepo wa viwanda kwenye Mkoa wetu wa Dodoma. Tunalima sana mahindi, tunafuga lakini Dodoma leo tunatazamana tu hapa, tunahitaji kujua Wanadodoma hivi tunapata lini Kiwanda cha Maziwa, tunapata lini Kiwanda cha Nyama, lakini tunapata lini viwanda vikubwa vya kuchakata mazao tunayoyalima ndani ya mkoa wetu likiwemo zao la mahindi. Hilo ni zigo nimempa dada yangu kipenzi, Wanadodoma wamenituma, wanatamani kusikia jambo hili, ni lini na sisi tutakuwa kwenye historia ya kuchakata mazao yetu pamoja na mifugo yetu badala ya watu wanakuja kutoka Kenya, wanakuja kutoka sijui Uganda wananunua ng'ombe wetu, wanabeba na pembe zetu, makongoro, Ngozi na wanabeba na kila kitu. Tunataka viwanda hapa, ng'ombe anunuliwe, achinjwe ngozi yetu tuitumie kutengeneza bidhaa mbalimbali, lakini zile pembe nazo...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tutumie kutengeneza bidhaa mbalimbali ili tuweze kuukuza Mkoa wetu wa Dodoma.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 33 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, wana wastara Mukadam kutoka Taasisi ya Mukadam. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 40 wa Mheshimiwa Ally Makoa, viongozi wa Chama na Serikali kutoka Kondoa Mjini, Mkoa wa Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Abdallah Chikota, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao wanatokea Mkoa wa Mtwara na Lindi. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 76 wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, Maaskofu na Wachungaji kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimwita Mheshimiwa Gwajima, jiandae Mheshimiwa Ng'wasi.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii ya viwanda na biashara. Kama unavyojua kazi ya Mbunge ni kutunga sheria, kupitisha bajeti za Serikali, kuishauri na kuisimamia Serikali. Tunapozungumza kwa habari ya viwanda na biashara ni hoja kubwa sana inayobeba hoja nyingi zinazofanya nchi iendelee au isiendelee, Wabunge wenzangu wote kwa umahiri sana wamezungumza sana kwa habari ya matatizo na hoja za kusababisha hii Wizara ya Viwanda na Biashara i-*improve*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza sana tangu jana, mambo mengi yanayozungumzwa ni matokeo ya tatizo, ukishughulika na matokeo ya tatizo huwezi kuondoa tatizo. Naona tatizo kubwa sana linalo tu-*face* ni maono ya nchi ya muda mrefu, hoja hii nimeisema tena na tena ni kwamba kilimo ni biashara, ufugaji ni biashara, uvuvi ni biashara kwa hiyo, kama kilimo ni biashara, ufugaji ni biashara, uvuvi ni biashara, uchimbaji wa madini ni biashara, hivi vinahusianaje na Wizara ya Viwanda na Biashara? Kwa hiyo, *connectivity* kati ya Wizara moja na

Wizara nyingine Serikalini ndiyo hasa tatizo kubwa tunaloli-*face* sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili hawa wafanyabiashara waende vizuri nikupe mfano mzuri, ni kiwanda kimoja kinaitwa *Kioo Limited*, kiwanda hiki kipo Temeke eneo la Sokota na kiwanda hiki tangu 1963 kipo, kiwanda hiki ni kikubwa kuliko viwanda vyote vya kutengeneza chupa Afrika Mashariki na kati. Kiwanda hiki kina-*export* nje chupa zaidi ya nchi 17. Kiwanda hiki ndiyo kinazalisha chupa zote unazoziona Tanzania, chupa za *Pepsi*, *Coca-Cola*, Konyagi, Serengeti na bia zote unazoziona, lakini *material* zake za kutengeneza hivyo vitu ni *material* kama nne zinazotumika ku-*manufacture* hizo chupa. Ya kwanza inaitwa *feldspar* ambayo inachimbwa Morogoro kwa wingi sana, ya pili ni *silica sand, silica sand* inapatika Mkuranga kwa wingi sana, ya tatu ni *limestone* ambapo kwetu kule Tanga ipo nyingi sana na ya nne ni *soda ash* ambayo tuna-*import* kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaona kwa mfano kiwanda hiki kimojawapo ambacho nataka kukitumia kama *study case* ya kukosa *connectivity* kati ya wizara moja na wizara nyingine au nchi kukosa maono ya kufanana. Kwa hiyo, unakuta kila Wizara inasukuma kivyake, huyu anakwenda kushoto, mwingine anakwenda kulia, mwingine anakwenda magharibi, matokeo yake huyu Waziri wa Viwanda tutamuua bure tukifikiri kwamba shida hii ni ya kwake, lakini kumbe shida ni kukosa maono ya muda mrefu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais baada ya kuwa tumeongea hii hoja akaunda Wizara ya Mipango ambayo Profesa Kitila anaisimamia. Profesa kwenye hoja yako inabidi utuoneshe kweli *you are a university Professor,* itabidi utuoneshe wakati hoja yako inakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni hiki *products* zinazofanya chupa itengenezwe ni nne na *materials* zake zote zinapatikana nchini kwa wingi, lakini kwa mfano *material* moja wapo ni *feldspar* inapatikana Morogoro, lakini matokeo yake hiki kiwanda kina-*import* kutokea nje ya nchi. *Material* nyingine ni *soda ash*, *soda ash* hapa kwetu ni nyingi

kwelikweli lakini kiwanda hiki kina-*import* kutokea nje, kinatoa Uturuki, Pakstani na Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia hiki kiwanda kinaingiza *soda ash* ya thamani ya shilingi dola milioni 150 kwa mwaka, lakini tunatumia *forex* na hapohapo tunalalamika kwamba hatuna *forex* wakati huo huo tuna-*import soda ash* kwa dola milioni 150 kwa *product* ambayo ipo hapa nchini. Kwa nini? Ni kwa sababu *soda ash* hiyo inachimbwa karibu na lile Ziwa Natron. Ziwa Natron hatuwezi kuchimba kwa sababu fulani fulani ambazo lazima kuwe na *connectivity* kati ya wizara husika na Wizara ya Biashara na kisingizio ni kwamba maeneo hayo yana *flamingo*, tukichimba flamingo wanaweza kuhama, lakini ule upande wa pili wa *Lake* Natron Kenya wenyewe wanachimba na wao Kenya wanachimba ndiyo wanatuuzia sisi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaweza kujiuliza sana sisi tunayo *soda ash* kwenye Ziwa Natroni, hatuwezi kuchimba kwa sababu ya *flamingo*, Kenya wanayo *soda ash* wenyewe wanachimba kwenye *flamingo* hao hao wanatuuzia sisi huku kwetu, lakini shida nini kwa sababu Wizara ya Biashara, Wizara ya *Mining* hawawezi kuwapa kibali hawa, lakini hapa kuna *connectivity* na wizara husika ya Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, kama tukifanikiwa kuwa na maono ya pamoja ya nchi, Wizara zote zikasomana kwa pamoja nchi ikawa na *vision* inayofanana, Wizara zote zika-*submit vision* yake kwenye Wizara ya Mipango na tukawa na *vision* ya Pamoja, nchi yetu itaenda vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni Mhubiri wa Injili, naomba ninukuu andiko moja kwenye kitabu cha Wakorintho, kitabu cha Wakorintho 1Wakorintho Mtume Paulo anawaambia watu anasema hivi: *"Kwa kuwa mwili si kiungo kimoja bali vingi." 1Wakorintho12:14 "Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi. Mguu ukisema, kwa kuwa mimi si mkono, basi si mwili; je! itakuwa ni kweli? Na sikio likisema, Kwa kuwa mimi si jicho basi mimi si mwili je litakuwa si mwili kweli? Kama mwili wote ukiwa jicho kuko wapi kusikia? Kama mwili wote ukiwa sikio, kuko wapi kunusa?"* Viungo

vyote vinategemeana ili utendaji kazi wa mwili uwe sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndivyo ilivyo Serikali, kwa mfano ni Kilimo ni biashara lakini huyu wa Kilimo anamsomaje wa Biashara, uvuvi ni biashara lakini wa Uvuvi anamsomaje wa Biashara, matokeo yake kila mtu anakimbia kwa mbio zake yeye mwenyewe na tuna-*miss the target*. Kwa hiyo, tatizo hasa ni moja, tatizo tunahitaji sasa kwa sababu Mheshimiwa Rais amekubali kuanza Tume ya Mipango, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, atuletee mpango wa nchi wa maono ya muda mrefu na tuuone kwamba ni mpango, siyo mtiririko wa matukio yanayotokea kwa kufuatana fuatana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mzimu wa Liganga na Mchuchuma, huu ni mzimu kweli kweli kama alivyosema Profesa Muhongo, Liganga na Mchuchuma iligunduliwa karne ya 18. Liganga maana yake ni mlima wa chuma wa *iron ore* ambao ndani yake una *vanadium* na *titanium*, pembeni mwake kuna mlima wa makaa ya mawe yaani chuma tumepewa pembeni na moto wa kuyeyusha chuma nao upo pembeni, lakini hatuwezi kuyeyusha mpaka leo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema ni kukosa mipango, kwa nini? Kwa mfano *component* kubwa ya reli ni chuma, tuna mradi wa reli ambao Mheshimiwa Rais, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuusimamia vizuri sana, tulianzaje kuanza mradi wa reli, tunaagiza chuma Misri, tunaagiza chuma Uturuki, tunaagiza chuma India, kwa nini hatukuanza mradi wa kuyeyusha chuma yetu kwanza ili tuje tutumie chuma yetu kutengeneza reli? Ni kwa sababu ya mipango ya muda mrefu ambayo mifumo haisomani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kama inawezekana Wizara husika ishughulike na suala la Liganga na Mchuchuma. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa fidia ya shilingi bilioni 15 aliyoitoa kwa wananchi wale, ili kutoa nafasi ya mradi huo uanze. Naomba sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Asukume kwa kadri

Anavyoweza ili mradi huo uanze, watu wa eneo hilo wapate faida na tuache kuagiza chuma kutoka nje ya nchi. Tuokoe *forex* zetu katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ukifanikiwa kubadili namna ya mtu kufikiri hauhitaji gereza. Narudia tena, *if you are able to change someone's perspective you do not need a prison.* Tunatakiwa tubadilishe namna ya kufikiri kwenye Wizara zetu tujue kwamba, nchi ni moja. *Therefore,* Wizara zote ni lazima zisomane ili zifanye kazi moja ya kujenga nchi yetu. Nakushukuru Sana. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ng'wasi, jiandae Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Kwanza naanza kwa kuipongeza sana Wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imefanyika kwa mwaka huu wa fedha uliokwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikiwa ni Mjumbe wa Kamati hii ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ninatoa ushuhuda wa kwamba, Wizara hii imepiga hatua kubwa sana. Kazi inayofanywa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake ni ya kupigiwa mfano. Sisi tunamtia moyo Mheshimiwa Waziri aendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza mchango wangu kwa kunukuu maneno ya Baba wa Taifa. Baba wa Taifa aliwahi kusema kwamba, "*Nchi hii haiwezi kuendelea bila kuwa na viwanda vya uhakika*" na kwa kusimamia sentensi yake hiyo, Baba wa Taifa wakati anaachia au ang'atuka madarakani aliacha viwanda 414 kila sehemu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nanukuu pia, maneno ya Balozi wa Marekani Nchini Tanzania, ambayo ameyasema Siku ya Tarehe 20, juzi tu, Dar es Salaam, amesema na naomba nitumie lugha ya Kiingereza aliyoitumia. Amesema, "*The reason we believe so*

*strongly is this, when you look at Tanzania as a country with about 65 million people on its way to become 130 million people by 2050, there is no way in the world that Tanzania can afford to have that large population without an industrial base, without a manufacturing base.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi huyu wa Marekani amesema kuwa sensa yetu inaonesha tuna watu zaidi ya milioni 60, lakini kwa mipango ya nchi yetu tunatazamia kufikia mwaka 2050 tutakuwa na watu milioni 130. Anatumia maneno, "*there is no way in the world*", hakuna namna duniani hapa Tanzania itaweza kubeba wingi huu wa watu milioni 130 bila kuwa na *base* nzuri na imara ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachelea kusema kwamba, kesho ya Tanzania yetu ipo chini ya Wizara hii. Tumekwenda kutembelea viwanda, kama Kamati na nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, katika mwaka wa fedha uliopita pekee ametenga fedha ya kutosha kufufua viwanda vyetu ambavyo vilikuwa vimekufa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunazungzumzia Kiwanda cha *KMTC* Kilimanjaro. Kiwanda hiki tumekitembelea Wanakamati wenzangu watashuhudia, tulishangazwa na mambo yanayofanyika pale; wanayeyusha chuma, wanatengeneza vipuri vingi vyote vya msingi, lakini utashangaa ni kwa nini bado tuna-*import* vipuri kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetembelea Kiwanda cha *TEMDO,* kiwanda ambacho kinatengeneza vifaa vizuri sana, kwa ajili ya Sekta yetu ya Afya; majokofu ya kuhifadhia maiti, vitanda vya kulalia wagonjwa vya kila namna na makabati ya hospitali. Kilichotushangaza, kama Wajumbe wa Kamati, ni kitendo cha Wizara ya Afya, kushindwa kununua vitu hivi kutoka kwa *TEMDO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajenga nyumba moja, tuongozwe na uzalendo, Tanzania ni nchi yetu sote. Ni kwa vipi leo hii Wizara ya Afya inaamua ku-*import* vitu kama ambavyo

vinavyotengenezwa na kiwanda chetu cha ndani? Vitu ambavyo vimethibitishwa kwa viwango vyetu vya *TBS* kuwa, ni imara na vinaweza kutumika? Badala ya kuchukua vitu vyetu wenyewe tunachukua vitu nchi za nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatumia fedha nyingi za kigeni, lakini si hivyo tu, Serikali ndio *procurer* namba moja, ndio mnunuzi namba moja, katika nchi hii. Kama Serikali, kupitia Wizara zake, ikiamua kuanza kutumia bidhaa zetu za ndani ambazo tunawekeza fedha nyingi katika viwanda vyetu, ninaamini tunakwenda kukuza viwanda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda kutembelea *CAMARTEC,* inatengeneza matrekta mazuri, imara na yamethibitishwa. Ni kwa nini Wizara husika hazichukui matrekta kutoka *CAMARTEC* na badala yake tunaagiza matrekta kutoka nje? Kwa nini hatuweki vigezo au kodi kubwa kwa vile vifaa vinavyozalishwa ndani kuagizwa kwake nje, ili tuweze kuvipa nguvu viwanda vyetu vya ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Wizara hii ni ikae na Wizara zote zinazohusika ili tuhakikishe tunavipa nguvu viwanda vyetu vya ndani. Tupunguze kuingiza vitu ambavyo tuna uwezo wa kuvizalisha wenyewe, ili tukuze viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii, natambua kwamba, *TRA* ipo chini ya Wizara ya Fedha. Naamini Mheshimiwa Rais, alikuwa na malengo yake kumuweka Mheshimiwa Waziri, akijua wazi aliwahi kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa wawekezaji na Wafanyabiashara wetu. Tunatambua kwamba, elimu inaendelea kutolewa, lakini napenda kuiomba Wizara hii ikae na watu wa *TRA* kuzungumza nao. Hapa tunavyozungumza Ripoti ya *CAG* ambayo imekuwa *tabled* Tarehe 28 Machi, 2024, inaonesha kuna kesi 947 za kikodi kwenye Mahakama ya Rufaa zenye thamani ya shilingi trilioni 10.41. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hii bajeti yetu tunaongelea shilingi trilioni 44 na wakati kesi za thamani ya shilingi trilioni 10 zipo Mahakamani za Kikodi, tunaenda wapi kama nchi? *TRA* ni lazima wajue kwamba, sisi ni Watanzania na lengo la wawekezaji, wafanyabiashara na watu wenye viwanda ni kujenga nchi hii. Lazima watambue kwamba, bila hawa wafanyabiashara na wawekezaji wao hawatakuwa kwenye hizo Ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu wakawekeza kwenye elimu kuliko kupelekana Mahakamani na kushikilia hizi fedha. Hizi fedha zingeweza kutumika katika kutuongezea mzunguko, lakini leo hii ziko Mahakamani wanapigania *TRA* na wafanyabiashara. Nadhani kuna jambo la kufanya katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kushauri katika Bunge hili na ninashauri tena. Kuna viwanda vingi sana vinaanzishwa na kufufuliwa kwenye nchi yetu; kwa mfano, tunazungumzia kile kiwanda cha ku-*assemble* magari, Kigamboni. Naipongeza sana Serikali ni hatua kubwa sana na nzuri, lakini pia, naipongeza Serikali kwa Kiwanda chetu cha *White Cement*, kiwanda kikubwa kuliko vyote kwenye *Sub-Saharan Africa*. Hii ni hatua kubwa sana na ni lazima tujivunie kama Watanzania. Pia, naipongeza Serikali kwa Kiwanda cha Vioo ambacho kinatoa vioo tani 700 wakati nchi hii tunahitaji tani 100 tu kwa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tujivunie mafanikio yetu, lakini ipo changamoto moja ambayo nitaendelea kuishauri Serikali hii, viwanda hivi vyote vinaanzishwa katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani. Ni lazima Serikali iangalie namna ya kuvitawanya katika mikoa mingine kama alivyofanya Muasisi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuhakikisha tunakuwa na maendeleo sawa kwa Mikoa yote ya nchi hii, viwanda visianzishwe Dar es Salaam na Pwani peke yake. Katika hili Serikali ni lazima itoe *incentives* kama ni za kikodi au za namna yoyote, ili kuhakikisha wawekezaji wanaokwenda kuwekeza kwenye mikoa mingine wanapata unafuu fulani, ili waweze kuvutiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mkoa katika nchi hii ambao hauna kitu ambacho ni *signature* ya mkoa huo. Kwa mfano Mwanza, tuna pamba, tuanzishiwe viwanda vya kuchakata pamba. Watu wanatakiwa kuwekeza huko wasiende kuwekeza viwanda vyao Dar es Salaam, wasiende kuwekeza viwanda vyao Pwani, hukohuko tulipo tufufuliwe viwanda vyetu. Wawekezaji wapewe *incentives* waanzishe, ili mikoa yote katika nchi hii iweze kuwa na maendeleo sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyozungumza sasa tunazungumzia Eneo Huru la Biashara la Afrika. Hatuwezi kwenda kama nchi katika Eneo Huru la Biashara la Afrika bila kuwa na viwanda vyetu ambavyo vitakuwa na bidhaa za kwenda kututangaza katika soko hilo. Soko hili huru kwa Afrika nzima tunahitaji na sisi Tanzania tujinasibu au tujinadi kwamba, tunapeleka kitu gani kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo ni kwamba, nchi za Afrika zinakuja kuchukua malighafi kwetu, zinakwenda kutengeneza vitu, vinakuja vinakuwa *labeled made in* nchi nyingine, wakati malighafi ni za kwetu Tanzania. Kwa nini, tuwe na jambo hilo wakati tunaweza tukaanzisha viwanda? Tukachakata malighafi zetu sisi wenyewe na tukapeleka katika eneo hili Huru la Afrika la Biashara tukaitangaza nchi yetu si, Afrika pekee yake, bali hata hata duniani pia?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna uwekezaji mkubwa unafanyika katika nchi hii. Kwanza katika nishati tuna Bwawa la Mwalimu Nyerere, shilingi trilioni 6.5 imekwenda pale. Tuna miundombinu ya barabara na madaraja mengi sana yanajengwa. *Value* ya uwekezaji huu haipo katika matumizi ya mtu mmoja mmoja, *value* katika uwekezaji huu itaoneshwa na kinachopatikana kutokana na uwekezaji wa viwanda vitakavyopitisha malighafi zake au bidhaa zake katika vitu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme; viwanda vingi vitakavyotumia umeme huu ndio vitakavyotusaidia ku-*justify* uwekezaji mkubwa tulioufanya. Naiomba Wizara hii, tuna kazi

kubwa sana ya kufanya. Namuomba sana Mheshimiwa Profesa Kitila katika mpango wake ambao yupo katika utaratibu wa kuutengeneza wa mwaka 2050 aangalie Sekta hii ya Viwanda kama sekta namba moja na kuiwekea utaratibu mzuri zaidi wa kuikuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Sekta ya Kilimo tunaongelea bajeti ya shilingi trilioni 1.2 wakati katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara, ambayo tunategemea itusaidie kuchakata hizi bidhaa za Kilimo tunaongelea shilingi bilioni 110, ni vitu ambavyo haviendani kabisa. Ni kwa vipi hii Wizara inatengewa shilingi bilioni 110 kwenda ku-*complement* Wizara inayotengewa shilingi trilioni 1.2? Haiwezekani! Lazima tuiangalie upya Sekta hii ya Viwanda na Biashara kwa sababu, kesho yetu sekta zote zinategemea uimara wa Sekta hii ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, ajiandae Mheshimiwa Mama Salma, hayupo? Mheshimiwa Maryam Omar, hayupo? Ajiandae Mheshimiwa Rahhi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naanza kwa kumpongeza sana Waziri wetu wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu wake Mheshimiwa Exaud Kigahe na Katibu Mkuu, Dkt. Hashil Abdallah, kwa kazi nzuri. Vilevile nawapongeza wale watumishi wengine wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya hii Wizara kwa kazi kubwa na mageuzi ya kuridhisha ambayo tunayaona kwenye Sekta hizi za Biashara na Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema ukweli tunaona kuna maendeleo. Kwa mfano, kwenye sekta ya biashara sasa hivi wanachangia *8.3 percent* ya pato la Taifa ambapo mwaka uliopita ilikuwa ni asilimia 8.2, kwa hiyo, kuna kitu kinafanyika. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, wetu kwa kuridhia

kuongeza bajeti ya Wizara hii kutoka shilingi bilioni 92.3 mpaka shilingi bilioni 110.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo pia, imeongezeka kidogo siyo mbaya ila nina angalizo, kama alivyosema Mheshimiwa Kamani. Bajeti ya Wizara hii bado ni ndogo, nitatoa sababu na nitarudia pale alipomalizia Mheshimiwa Kamani kwamba, kuna uwekezaji mkubwa unafanyika kwenye Sekta zetu za uzalishaji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kule kwenye kilimo Mheshimiwa Bashe anatoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wetu. Wakulima wengi walikuwa hawazalishi sana, sasa hivi mbolea imekwenda kule watu wanazalisha. Mheshimiwa Waziri ulitakiwa uende sambamba na kuongezeka tija kwa Wizara hizi za uzalishaji ili na wao uwasaidie kuwekeza kwenye kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiwezeshe *SIDO,* tuiwezeshe *CAMARTEC*, tuiwezeshe *KMTC* na *TEMDO,* watengeneze viwanda vidogo vya kuchakata, kwa mfano, unga, mahindi ili tusafirishe unga badala ya kupeleka mahindi nje. Mpunga tupate mchele, zile zabibu tupate *wine* na kadhalika. Kwa hiyo, unahitaji hela nyingi kuwekeza kwenye haya mashirika niliyoyataja na kuanzisha kongani za viwanda katika maeneo mbalimbali hapa nchini, kama alivyosema Mheshimiwa Kamani.

Mheshimia Naibu Spika, twende kwenye kanda zote tuwe na kongani za viwanda ambazo zitasaidia kuchakata mazao yetu, tusipofanya hivyo hatutakaa tuchomoke. Kwa hiyo, *point* yangu kubwa ni kwamba, hii Wizara inahitaji pesa nyingi siyo shilingi bilioni 100 na kitu, hapana. Tunatakiwa tuwe hata na shilingi trilioni, ikifika pale, ili awezeshwe kuanzisha viwanda. Tusipofanya hivyo hatutapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa utaratibu wake na wenzake wa kukutana na wafanyabiashara na wenye viwanda ambapo huwa anasikiliza

kero zao. Hongera sana, ni jambo zuri. Namwomba, kama alivyosema Mheshimiwa Edwin Swalle, aendelee kuwa na *forum* na hao watu ili kusikiliza kero zao. *(Makofi)*

Mheshimimiwa Naibu Spika, kuna kero za kikodi na za kibiashara kwenye kuanzisha viwanda na biashara, bado zipo. Kwa mfano, nilikuwa ninaongea na baadhi ya wenye viwanda wakasema kodi ya ushuru wa bidhaa kuna kakero kidogo pale, *Electronic Tax Stamp* kuna kakero kidogo pale na *Skills Development Levy* kuna kakero kidogo pale. Kwa hiyo, akikaa na Wizara ya Fedha na hao watu wakimueleza, najua tutatatua hizi changamoto na tutaenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana wenye viwanda, tusiondoke hapa bila kuwapongeza hawa watu. Viwanda vya *Cement,* bia, sukari, sigara, mabati, vinywaji baridi, mabomba, nondo, chumvi, mabati na vioo, hawa watu wametoa mchango mkubwa sana kwenye kulisaidia Taifa letu kwenda mbele. Naiomba Serikali, hawa watu wanazalisha, lakini kuna baadhi ya Wizara kwenye ile miradi mikubwa mikubwa ya Serikali hatanunui bidhaa zao. Kwa mfano, mabati, kwa nini tusiende kununua mabati yanayozalishwa hapa na kutumika kwenye miradi ya Kitaifa inayotekelezwa hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vioo; badala ya kuagiza vioo kutoka nje, China na kwingine, ni kwa nini tusinunue vya kutoka kwenye haya makampuni yetu ambayo yanafanya hapa? *Cement*, mabomba na vitu vingine vyote, kwa hiyo, tuwaunge mkono kwa kuhakikisha kwamba, tunanunua bidhaa wanazozalisha badala ya kukimbilia nje ambako tunapeleka pesa zetu bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Sitaongea sana kwa sababu, wengi wameshaongea, lakini nasisitiza tu. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa ile fidia kwa watu wetu waliokuwa na maeneo kule, wamefurahi na sisi tumefurahi. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri apambane sasa, yeye anajua mambo mengi ya kimkataba, ameshatekeleza, yule mwekezaji ambaye bado

hajaja, apambane naye piga ua ili sisi tuanze kuchimba chuma chetu, kianze kutusaidia kuwekeza kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni wa Kiwanda cha Kutengeneza Viuadudu cha Kibaha. Tuna Kiwanda kikubwa sana pale Kibaha ambacho kimetengenezwa kwa msaada wa Serikali ya Cuba, kiwanda hiki huwa kinatengeneza viuadudu vya kibaiolojia vya kuua mbu na pia, kinaweza kikatengeneza vya kuua wadudu wa mazao na vinginevyo, pamoja na mbolea za kibaiolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha ni kiwanda hiki ni *investment* kubwa imefanywa na Wacuba pale, lakini Serikali hainunui bidhaa kutoka kwenye hiki kiwanda. Nitakuwa *specific* hapa, Wizara ya Afya na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanatakiwa wanunue dawa za kuangamiza mbu kwenye mazalia yao. Kwa mwaka karibu watu 3,600 hivi wanakufa hivi, kwa ajili ya ugonjwa wa malaria, lakini hatununui dawa kule kwenye kile kiwanda na kipo hapa. Sijui ni nini kinaendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa, anihakikishie amefikia wapi hili suala la dawa za kutoka kwenye Kiwanda chetu cha Kibaha kwa sababu, *it will be a waste of money*. Watu wametusaidia, tumewekeza kwenye hiki kiwanda, lakini hatutumii bidhaa zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuwekeza pale Kilimanjaro, sasa hivi nazungumzia Viwanda vya Mkoa wa Kilimanjaro. *Kilimanjaro Machine Tools* ni kiwanda ambacho kimefufuliwa baada ya miaka 30 iliyopita. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumewekeza pale, mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* wameomba shilingi bilioni 3.46 tu ili waweze kujiendesha moja kwa moja kuzalisha vipuri na *spare* nyingine za

viwandani ikiwa ni pamoja na magari, kama watapewa hizi pesa. Kwa hiyo, naiomba Wizara, chonde chonde, tuwapatie hawa watu wa *Kilimanjaro Machine Tools* hizi pesa, siyo nyingi kusema kweli ukilinganisha na kitu ambacho wameshafanya mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, pale *TPC* mashine za kuzalisha sukari ziliungua, hawa jamaa wakaingia pale wakatengeneza na wakatusaidia tukaokoa pesa za kigeni. Kwa hiyo, nawaomba sana tukisaidie hiki kiwanda ambacho kipo Mkoani Kilimanjaro ili kiweze kuendelea na uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nakipongeza Kiwanda cha *Choice Coffee Kilimanjaro,* ambacho kinalelewa na *SIDO,* hawa jamaa wanafanya kazi nzuri sana, tunaona hapa walianza na shilingi 300,000 lakini sasa hivi wana mradi unaofikia zaidi ya shilingi 300,000,000 na wanazalisha kahawa ambayo inapelekwa mpaka nje. Sasa naomba *SIDO* itapakae nchi nzima ili kuanzisha viwanda kama hivi, wasing'ang'anie tu pale Kilimanjaro, waende kwenye kanda nyingine ambazo zinalima kahawa nako tuanzishe viwanda vya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha mwisho kwenye mchango wangu ni viwanda viwili vilivyopo Mkoani Kilimanjaro. Cha kwanza ni Kiwanda cha Kukoboa Mpunga cha Chekereni, kule Mabogini, ambacho kilibinafsishwa akapewa mwekezaji na hakuweza kufanya kitu. Kingine ni Kiwanda cha *Pesticide Manufacturer's Limited* cha Moshi kinachotengeneza dawa. Naiomba Wizara iendelee na mchakato wa kutafuta wawekezaji kuwekeza kwenye viwanda hivi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Yustina Rahhi, wajiandae Mheshimiwa Profesa Kitila, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya na Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Dkt. Ashatu pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii. Vilevile kwa namna ya pekee nampongeza Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli tumeona mambo mazuri katika Wizara hii lakini mojawapo wenzangu wameongea kwamba katika kipindi hiki tumeweza kufufua kiwanda chetu cha *KMTC* ambayo kilishakufa zaidi ya miaka 25, palishakuwa pori, lakini Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweza kutoa fedha tumekarabati kile ni kizuri. Zaidi wamesimika kinu kikubwa cha kufua chuma *(foundry)* chenye uwezo mkubwa na sasa hivi kinafanya kazi *under capacity* kwa sababu ya kukosa *raw material* katika kiwanda hicho. Kimebaki kinategemea vyuma chakavu vya kuokota mitaani, ndiyo maana wenzangu wanasemea sana habari ya Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawapongeza sana, lakini kiwanda hiki kimeomba mtaji *(working capacity)* ya shilingi bilioni 3.4 na katika mpango kazi wao tukiwapa hizi hela shilingi bilioni 3.4 wana uwezo wa kuzalisha shilingi bilioni 10.2 katika muda wa miaka mitano. Naomba tu Waziri akija aniambie mpango wa Serikali sasa wa kuweza kukipatia *working capacity* Kiwanda hiki cha *KMTC* ambacho kina uwezo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ina uwezo wa kuajiri wafanyakazi 1,400 kwa mwaka, ambapo kati ya hawa wafanyakazi 207 watakuwa wa kudumu na wafanyakazi 1,200 watakuwa ni wafanyakazi wa muda. Pamoja na uwezo wa

kuweza kutoa mashine kama 300 kwa mwaka. Pia kuweza kutoa vifaa ambavyo taasisi nyingine kama afya, wenzangu wameshaongea inatoa vifaa vizuri sana. Kwa hiyo tukikiwezesha kiwanda hiki kitaendelea kufanya mambo mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwekezaji ambao Serikali umekwishakuufanya katika *CAMARTEC*. *CAMARTEC* inatoa teknolojia nzuri sana, ni mdau mzuri sana katika kilimo. Kama tumeweka fedha za kutosha katika kilimo tuna kila sababu ya ku-*support CAMARTEC*. *CAMARTEC* inatoa teknolojia, hatuwezi kuweka uwekezaji mkubwa katika kilimo, lakini bado tukabaki kwenye kilimo chetu cha jembe la mkono. *CAMARTEC* ndiyo itasaidia wakulima wa Tanzania kutoka kwenye jembe la mkono kupanda, kwa sababu hata kama wanalima kwa trekta na majembe ya ng'ombe bado wakulima wa Tanzania wanapanda kwa mikono, watapalilia kwa mikono na watavuna kwa mikono. Kuna teknolojia nyingi nzuri ambazo *CAMARTEC* itasaidia sana kukisogeza kilimo chetu kutoka hapa kwenda kwenye kilimo ambacho tunakitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa *CAMARTEC* wameomba mtaji wa shilingi bilioni 7.4. Lazima tuwekeze kwenye *CAMARTEC*. Naiomba Serikali yangu ijaribu kuwasaidia *CAMARTEC* iwape huo mtaji ili uweze ukasaidia wakulima na wafugaji wa Tanzania ambao ndiyo sehemu kubwa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisemee kuhusu bajeti. Bado nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kusema ukweli kuna ongezeko la bajeti ya karibu 21% kwa sababu bajeti inayoisha ilikuwa ni shilingi bilioni 91.9 na sasa tunaenda kutekeleza bajeti ya shilingi bilioni 110. Japokuwa bajeti ya maendeleo ya mwaka jana ilikuwa ni shilingi bilioni 25 na mwaka huu ni bilioni 29, lakini sasa ndiyo tuseme Watanzania kama azma yetu ilikuwa ni kwenda kwenye uchumi wa kati, kupitia uchumi shindani wa viwanda kiwango hiki tunachokwenda kuwekeza kwenye viwanda ni kweli tutatoka kwa namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yangu sikivu kama kweli tuna nia dhabiti ya kuitoa nchi yetu kuipeleka katika uchumi wa kati na kuwasaidia Watanzania tuendelee kuwekeza bajeti ya kutosha katika Wizara hii ya Viwanda. Tuna fursa nyingi sana katika nchi yetu na ndiyo sababu tunasema viwanda vitafanya vizuri. Tuna fursa, tuna madini ya kila aina, tuna gesi asilia, tuna chuma, tuna makaa ya mawe pia tuna mazao. Tunalima korosho 90% ya korosho zetu tunaziuza roho nje, wenzetu kule wanapata kazi ya kusindika, lakini na ile *by product* pale wanatengeneza mvinyo. Sisi kazi yetu ni kulima na kuwapa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunazalisha mahindi ya kutosha. Tunauza mahindi punje, wenzetu kule wanasindika na *by product* wanatengeneza vyakula vya mifugo na vitu vingine. Sisi tumebaki kama tulivyo. Tunazalisha pamba lakini bado sisi hatujaweza kujitegemea, tunasubiria suti za Uturuki hapa tununue shilingi 400,000 na kuendelea. Kwa hiyo tuna kitu cha ziada cha kufanya ili tuone tu kwamba viwanda vyetu vitatusaidia Watanzania kuondoka kutoka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vina kazi kubwa sana kwa Watanzania. Kuna nguvu kazi kubwa sana ya Watanzania. Vijana wetu asilimia kubwa, kwa mfano watu karibu 800,000 kila mwaka wanaingia kwenye soko la ajira. Sehemu pekee ambayo inaweza ku-*absorb* nguvu kazi hii ni viwanda, hakuna sehemu nyingine ambayo tunaweza tukawapeleka vijana wetu kama hatutakuwa na viwanda. Kwa hiyo uwekezaji ni *serious* tufikirie namna gani tuongeze bajeti ya Wizara hii ili iweze kuwekeza kwenye viwanda vidogo vidogo na viwanda vikubwa viweze kuajiri Watanzania, pia viweze kuongeza thamani ya mazao ya Watanzania na wapate faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu lingine ni kwenye kulinda viwanda vyetu vya ndani. Ni kweli tunahitaji wawekezaji katika viwanda lakini ni wapi tunataka tuwashawishi wawekezaji? Kama kuna viwanda vidogo vidogo vya kusindika, viwanda ambavyo Watanzania *(local content)* wanaweza wakafanya kazi tukawaleta wawekezaji ambavyo wenzangu wamekwishasema,

wawekezaji ambao tunawajengea mazingira kuna *grace period* ambayo hawalipi kodi ya nchi. Kuna *incentives* nyingi tunawapa halafu wanakuwa washindani wa viwanda vyetu vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tunazalisha *cement,* mfano *Tanga Cement, raw material* yote ipo hapa. *Tanga Cement* ipo pale inazalisha *cement* kwa *full capacity* ya kwake na kwa gharama zote, pia kuna kiwanda kingine cha Mchina pale cha *Maweni Limestone* kinatoa *cement* ya *Huaxin* nafikiri ambayo huko mitaani bei yake ipo chini kuliko *Tanga Cement*. Kitu gani kinafanyika? Hawa wenzetu wana hiyo *grace period* na misamaha ya kodi lakini wanaajiri Watanzania. 80% ya Watanzania wanaoajiriwa pale ni wale wanaofanya kazi kwa muda, wachache sana ndiyo wameajiriwa kama wafanyaki wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili hiyo wale wafanyakazi hawapo *pensionable* (hawana *pension)*, hawalipiwi bima ya afya na hawaishii kuwa vibarua. Ina maana wana mkataba wa kufanya kazi miezi sita ikiisha wanae-*renew* tena kuendelea kuwa vibarua. Kama aliajiriwa kama Yustina Rahhi akirudi anaenda kuajiriwa kubadilisha jina anakuwa Amina Hamis lakini badala yake watakuwa wamefanya kazi hata miaka 10 watatoka pale wamezeeka na watakuwa hawapo *pensionable*. Kwa hiyo Serikali naomba mwangalie tuendelee ku-*encorage* viwanda vyetu vya ndani na tuangalie msururu wa kodi katika viwanda vyetu wenyewe vya ndani. Tukiweka ushindani na wenzetu wa nje hawa, sisi *product* ya viwanda vya kwetu bei yake itakuwa juu ukilinganisha na wenzetu hawa ambao wana *incentives*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo tuna vitu kama chumvi tunaagiza kutoka nje wakati sisi tuna chumvi yetu hapa ya kutosha na utaona tu chumvi hiyo itakuja huku ndani itauzwa kwa bei ndogo. Sasa tubadilike tuache kuingiza chumvi kutoka nje pamoja na vitu vyote ambavyo huku ndani vinazalishwa na tuweze kuvilinda ili visizalishwe kwa gharama kubwa. Vitu vinavyotoka nje vipewe masharti visiue viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tuna viwanda vyetu vya mbolea. Viwanda vya mbolea vinatakiwa visaidiwe, tumeona *impact* kubwa ya Serikali kuweka ruzuku katika mbolea. Kabla ya ruzuku Watanzania walikuwa wanatumia mbolea kwenye tani 400,000 – 600,000, lakini toka ruzuku ya Serikali imewekwa matumizi ya mbolea *impact* yake imeongezeka mpaka tani 1,000,000. Hii *impact* yake tutaiona katika uzalishaji wa mazao. Ina maana nchi yetu itazalisha mazao mengi kuliko ambavyo isingekuwa na mbolea. Kwa hiyo naomba tu Serikali iendelee kuwekeza kwenye Kiwanda cha Minjingu na kwenye Kiwanda cha *Itracom*, ruzuku ya Serikali imeonesha faida kubwa sana kwa wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuomba tu kwamba, ruzuku iendelee kuongezwa viwandani na viwanda vile viendelee kupewa mtaji. Wenzangu wamesema sana kuhusu Liganga na Mchuchuma. Siwezi kusema sana lakini niseme tu kwamba, hivi kwa nini tunaendelea kufanya mazungumzo na mwekezaji kwa zaidi ya miaka 30? Ingekuwa ni mawazo yangu imefika muda wa Serikali yetu ya Tanzania sasa kuchukua maamuzi magumu kwa sababu tumekwishakufanya kazi kubwa ikiwepo kufidia. Nchi yetu imeshatoa shilingi bilioni 15 pale na huyu mwekezaji wa China nadhani pengine ameona huu mradi kwake sio *viable*. Kwao wana tani zaidi ya bilioni 20 ambazo zipo pale kama *reserve*, sisi labda kwetu kuna tani 130 pengine ameona kwake siyo *viable*. Kwa hiyo tutaendelea kumbembeleza mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imetekeleza miradi mikubwa sana, mfano mmoja wapo ukiwa Mradi wa….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa maandishi ni mahususi kuhusu viwanda vya chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda sasa kumekuwa na kilio maeneo mengi ambako wawekezaji walichukua viwanda vya chai kuanzia Mufindi, Njombe, Rungwe, Korogwe mpaka Lushoto. Maisha ya wananchi yamekuwa magumu, wakulima wadogo wanalia, *bad enough* kwa mfano kule Mufindi wameanza kukata miti ambayo ni ya miaka na miaka, je, siyo hujuma? Hii ilijitokeza *Tanga Fresh,* nchi jirani walitaka kuchukua kile kiwanda lakini hekima ikatawala hawakupewa. Nashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tufanye jambo kuhusu viwanda vya chai kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA BAKAR YUSSUF:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri sana anayoifanya nchini kwetu kwa kuwaletea maendeleo makubwa Watanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na wasaidizi wao wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kama hivi ifuatavyo, kwanza naomba niishauri Serikali kwamba kuna haja sasa ya kuongeza uwekezaji zaidi katika Sekta ya Viwanda kwa kufufua viwanda vyote vilivyokufa nchini pamoja na kujenga viwanda vipya vingi zaidi ili nchi iweze kuzalisha bidhaa nyingi zaidi kuliko kutegemea bidhaa kutoka nje ya nchi, hii pia itasaidia kutengeneza fursa nyingi za ajira kwa vijana wa elimu tofauti. Pia itapelekea kuongezeka kwa maendeleo nchini na itasaidia kupunguza ongezeko la mfumko wa bei nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maombi haya yazingatiwe na Wizara hii yenye dhamana na biashara ya nchi hii, kwa kuhakikisha inasimamia ukuaji wa biashara nchini, kwa mfano kuhakikisha wafanyabiashara hawa wa Iringa:-

(i) Wasibughudhiwe na *TRA,* kwa kufungiwa akaunti zao;

(ii) Wasisainishwe mikataba na *TRA* ambayo haina msingi sana zaidi ya kutengeneza mazingira ya rushwa;

(iii) Wapewe elimu zaidi badala ya kutumia nguvu na kuwatisha katika ukusanyaji wa kodi;

(iv) Kodi za muda mrefu zisitumike kuwanyanyasa wafanyabiashara wakati mamlaka ya *TRA* kwanza walitoa *tax clearance* kwa wafanyabiashara hawa walikuwepo wakati huo ambao ulikuwa sahihi kudai madai hayo, sasa kama italazimu hilo njia za busara na hekima zitumike badala ya kuwanyanyasa wafanyabiashara; na

Mheshimiwa Naibu Spika, *NHC* Iringa pia waaangalie upandishaji wao wa kodi unaathiri biashara, bila kuzingatia ubora wa nyumba zao na bei halisi ya soko kulingana na ubora wa nyumba zenyewe.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi wanavyoliongoza Taifa letu na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli yapo mambo mengi sana yametekelezwa hususan miradi ya maendeleo iliyoshindikana katika sekta mbalimbali kwa muda mrefu katika jimbo langu la Mbulu Mjini, Mungu Mwenyezi alibariki Taifa letu. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Watendaji Wakuu wote wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii na Wajumbe wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana ya Viwanda na Biashara iliyowasilishwa mbele ya Bunge letu hili. Tunaiomba Serikali yetu iangalie utaratibu wa kila halmashauri zetu kuwa na Maafisa Biashara watakaosimamia sekta ya biashara na viwanda ili wataalam hawa waweze kulea na kukuza viwanda vidogo ambayo viko kwenye maeneo ya halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie utaratibu wa kuweka kalenda ya vikao vya mabaraza ya biashara kuanzia ngazi za wilaya, mikoa na Taifa ili kupata nafasi ya kusikiliza, kujadili changamoto zinazowakabili wafanyabiashara kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iangalie utaratibu wa kuanzisha mpango wa kusikiliza wafanyabiashara kuhusu kodi wanayolipa *TRA* kama wanaridhika na viwango vyake pamoja na taswira yao kuhusu huduma wanayopokea kutoka Serikalini. Hivi sasa uelewa mdogo wa kodi kutoka kwa wafanyabiashara umesababisha chuki na manung'uniko kwa Serikali yao kwani baadhi ya wafanyakazi wa *TRA* hutumia nafasi zao kuwabambikizia kodi kubwa wafanyabiashara wa kati ambao hawawezi kuandaa hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; awali ya yote nianze kwa kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji na wasaidizi

wake kwa hotuba yake ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2024/2025. Ni hotuba nzuri yenye taarifa na takwimu muhimu za kutuwezesha Waheshimiwa Wabunge kujadili na kuishauri Serikali kuhusu sekta hii muhimu ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitoe pongezi za dhati kwa wafanyabiashara wote nchini kwa kazi nzuri ya kupigiwa mfano mnayoifanya kuliwezesha Taifa letu kupata bidhaa na kuchangia katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali, hongera sana. Vilevile niwapongeze wafanyabiashara wa Jimbo la Kisesa kwa juhudi kubwa wanazofanya katika mageuzi ya biashara kwa falsafa yetu ya hakuna kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya kijumla; Wizara inaomba kiasi cha shilingi bilioni 110.899 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ambayo mimi sina tatizo nayo na inawatosha kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kuyapata masoko ya nyama ya Nchi za Saudi Arabia, Qatar na Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE)* ambapo Kampuni za *Tan Choice* na *Eliya Food Industries* zimekidhi vigezo vya kuuza nyama katika masoko hayo jumla ya tani 4, 497.7 zenye thamani ya shilingi bilioni 56.78 huu ni mwanzo mzuri, hongera pia uongozi wa Kampuni za *Tan Choice* na *Eliya Food Industries.*

Mheshimiwa Naibu Spika, miungano ya makampuni *(mergers)* 65 bila kupata kibali cha Tume ya Ushindani *(FCC), BRELA* iliwezaje kuruhusu muunganiko huo bila kibali cha *FCC?* (Ibara ya 116 ya hotuba ya Waziri).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kununua kampuni *(acquisition),* Kampuni ya *Etablissements Maurel et Prom S.A* kuinunua Kampuni ya *Wentworth Resources Plc* yenye kitalu cha uchimbaji gesi wa *Mnazi Bay* ambapo sharti kubwa lilikuwa kuiongezea *TPDC* haki ya umiliki kufikia 40%, je kuongezeka kwa haki ya umiliki wa *TPDC* kumesaidiaje kupungua kwa bei ya gesi inayotoka katika vitalu hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa tiba kwa muda mrefu Serikali imeahidi kujenga kiwanda cha vifaa tiba katika Mkoa wa Simiyu, lakini hadi leo hakuna kinachoendelea na hapa nchini uzalishaji wa vifaa tiba bado ni mdogo sana (Ibara ya 143 ya hotuba ya Waziri) kwa sehemu kubwa tunategemea kutoka nje ya nchi. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara katika hotuba yake anaonesha kuwa mauzo yetu ya nje katika Masoko ya Ulaya, *EAC, SADC, AGOA,* Bara la Asia yalipungua kwa shilingi trilioni 2.851 mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022 wakati katika hotuba ya Waziri wa Kilimo inaonesha kuwa mauzo katika masoko hayo yaliongezeka kwa shilingi trilioni 2.86; nini chanzo cha mgongano wa takwimu hizi kwa Mawaziri hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, haijaelezwa changamoto zilizopo katika uwekaji wa vinasaba katika mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa (Ibara ya 104 ya hotuba ya Waziri)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri haijatoa tathmini ya hatua zilizochukuliwa na Serikali katika mwaka wa fedha uliopita na miaka mingine mfano mwaka jana tulitenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 600 kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Dhamana kwa Wakopaji wanaozalisha bidhaa za kuuza nje ya nchi *(Export Credit Guarantee Scheme -ECGS)* na Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wajasiriamali wadogo na wa kati *(Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme - SMEGS)*. Suala la misamaha ya kodi imeleta tija gani? Hatujaelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri haijibu matatizo sugu tuliyonayo ikiwemo hatua ya utekelezaji wa Mkataba wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma (Ibara ya 132 na 133 ya hotuba ya Waziri).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumuko wa bei za bidhaa na ugumu wa maisha, ukiambiwa mfumuko wa bei umeshuka ni wa kwenye makaratasi, lakini mtaani wananchi wanalia na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya kodi imekuwa ikitumika kama nyezo ya kuvutia wawekezaji nchini, kuvutia mitaji, ajira, urahisi wa upatikanaji wa bidhaa na bei nafuu kwa walaji wa mwisho ambao ni wananchi. Tulisamehe kodi maeneo mengi sana mwaka jana na miaka mingine iliyopita, lakini hakuna tathmini ya mafanikio na changamoto ya misamaha hiyo, tulitegemea Waziri wa Viwanda na Biashara atueleze mafanikio tuliyopata kutokana na misamaha ya kodi tunayotoa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokishuhudia ni mfumuko mkubwa wa bei nchini, kuadimika kwa dola na ugumu wa maisha kwa wananchi wetu. Tusipofanya tathmini za mara kwa mara eneo la utoaji wa misamaha ya kodi litatumika kufanikisha maslahi binafsi na nchi kuikosesha mapato. Hivi sasa nchi yetu ni ya mwisho katika nchi za Afrika Mashariki kwa kukusanya mapato kidogo ikilinganishwa na pato la Taifa. Nchi yetu inakusanya 12.5% ya pato la Taifa iikilinganishwa na nchi zingine kama Kenya na Rwanda ambazo zinakusanya zaidi ya 15% ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu misamaha ya kodi kwa viwanda vya kuunganisha magari na matrela; viwanda vya kuunganisha magari viwili na viwanda vya kuunganisha matrela 11 kusamehewa kodi ya *VAT,* misamaha ya aina hii ni ya upendeleo na haina maslahi kwa umma, haingii akilini kusamehe makampuni yanayoagiza magari nje ya nchi na kusamehewa kodi eti kwa sababu tu yanaunganishia hapa nchini. Tunavyo viwanda vingi vinavyoagiza vyuma na kuvichakata hapa nchini kwa ajili ya kupata bidhaa za vyuma ikiwemo nondo, mabati, misumari na kadhalika, lakini viwanda hivyo vinalipa kodi zote kwa nini eneo hili nyeti halijasamehewa kodi na ifahamike kuwa kila mahali palipoachwa maslahi ya umma maana yake kuna maslahi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji unaozungumza ni mdogo sana kwani upande wa kuunganisha magari ni shilingi bilioni 75 tu, makampuni yote ni ya nje huku ajira 550 ambazo nazo hazina uhalisia. Kama suala ni viwanda vya kuunganisha na sio kutengeneza kwa nini bajaj, pikipiki na baiskeli ambazo nazo

huingizwa nchini zikiwa hazijaunganishwa mbona hajizahusika kwenye msamaha huo wa kodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kusamehe kodi wawekezaji mahiri, Waziri atuambie toka tuliposamehe kodi kwa wawekezaji mahiri hadi sasa ni makampuni mangapi yananufaika na msamaha huo? Tumevutia mitaji kiasi gani na imesaidiaje kupunguza bei za bidhaa zinazozalishwa na makampuni hayo ikilinganishwa na makampuni ambayo hayana msamaha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuondoa faini kwenye miamala ya *transfer pricing,* kwa mujibu wa Kanuni za Miamala ya Mauziano ya Bidhaa kwa Makampuni ya Kimataifa *(Tax Administration (Transfer Pricing) Regulation*) na miongozo yake inataka kampuni itakayogundulika kutumia *TP* kukwepa kodi litapigwa faini ya 100% ya kodi iliyokwepwa. Tangu mwaka 2021/2022 faini hii iliondolewa ili kubariki makampuni hayo kukwepa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya *CAG* ya mwaka 2019/2020 ilionesha kuwa *TRA* haina uwezo wa kutosha wa kukagua miamala ya *transfer pricing* kutokana na ukosefu wa wataalam na teknolojia pamoja na bajeti ndogo. Hii ina maana kuwa katika hili eneo tunapigwa sana na makampuni ya Kimataifa *(MNCs)* na tunapoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea leo Waziri atueleze tija tuliyoipata kutokana na misamaha hiyo, lakini haya yote yanafanywa wakati huo huo tunaenda kuanzisha kodi kwa wachimbaji wadogo *(Artisanal and Small-Scale Miners)* ya 2% katika mapato yao na kodi zingine nyingi, wakati huo huo tunaenda kutoza kodi kubwa kwenye mishahara ya watumishi wa umma na sekta binafsi. Hii sio haki kabisa na hakuna usawa wa ulipaji kodi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri ameshindwa kuleta taarifa ya mafanikio ya makampuni yaliyonufaika na misamaha ya kodi maana yake hakuna tija iliyopatikana bali misamaha hiyo iliyoombwa ilikuwa ni kufanikisha maslahi binafsi na kulikosesha

Taifa letu mapato. Bunge limefichwa na halijui kinachoendelea kwenye eneo hili la misamaha ya kodi na hivi punde litaletewa tena kupitisha misamaha mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kufuta faini ya 15% *(PVoC)* kwa bidhaa zinazoingizwa nchini bila Cheti cha Ukaguzi wa Ubora *(CoC);* mwaka 2023 Serikali ilifuta adhabu ya 15% ya thamani ya bidhaa inayotozwa na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* kwa bidhaa zinazoingia nchini bila kuwa Cheti cha Uthibitisho wa Ukaguzi wa Ubora *(Certificate of Conformity-CoC)*. Aidha, bidhaa hizo zisizo na Cheti cha Utambulisho wa Ubora zitafanyiwa ukaguzi wa ubora zinapofika nchini na kulipiwa gharama za ukaguzi pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Waziri atuambie huu msamaha ulilenga kutibu nini na kama Taifa tumepata mafanikio gani kutokana na uamuzi huo. Taarifa zilizopo za changamoto kufuatia maamuzi hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) *TBS* haina maabara yenye uwezo wa kupima bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na ndiyo maana iliingia Mikataba na Makampuni ya *TUV, SGS, BV, INTERTECH* na *CCIC* ambazo zina maabara zilizopewa ithibati ya kidunia na maabara hizo zipo duniani kote. Uchache na uwezo mdogo wa maabara ya *TBS* unasababisha msongamano mkubwa na hivyo kusababisha kuchelewa bidhaa bandarini.

(ii) Kuongezeka kwa bidhaa zisizo na ubora kuingia nchini ambapo imekuwa ikiripotiwa kila sehemu ikiwemo vifaa vya vya ujenzi, umeme, pikipiki na magari. Huko duniani kumeazishwa viwanda vidogo vidogo vingi vinavyotengeza bidhaa duni kwa ajili ya kuziuzia nchi masikini na hivyo kukosekana kwa udhibiti kumeifanya nchi yetu kuwa jalala la bidhaa *fake*.

(iii) *PVoC* inahitajika nyaraka nyingi na vipimo vya maabara kuthibitisha uhalali wa bidhaa hivyo kuondoa cheti cha ubora *(Certificate of Conformity -CoC)*

kunasababisha ongezeko kubwa la bidhaa zinazoingia nchini zisizokuwa na ubora kwa kuwa *TBS* haikuwa na maandalizi ya kukagua mizigo yote iliyokuwa inafanyiwa ukaguzi nje ya nchi na hivyo kuigeuza Tanzania kuwa jalala la bidhaa duni.

(iv) Kukosekana kwa taarifa za awali kwa wafanyabiashara kuhusu viwango vya ubora wa bidhaa walizonunua na kupata hasara kubwa zinapobainika kuwa ni *fake* wakiwa wameshafikisha tayari nchini ambapo huishia kuteketezwa na hivyo kupoteza mtaji pamoja na uchafuzi wa mazingira.

(v) Faini ya 15% ya thamani ya bidhaa imeondolewa huku ikiwa ni sehemu ya mkataba wa kukinga watoa huduma katika kutekeleza Mradi wa *PVoC* jambo ambalo linaweza kuiingiza nchi yetu kwenye mgogoro wa diplomasia na makampuni hayo ya kimataifa.

(vi) Kuondoa utaratibu wa *(Pre-shipment Verification of Conformity-PVoC)* kulihitaji maandalizi ya *TBS* kuwa na maabara zenye uwezo wa kutoa huduma kwa bidhaa zinaoongezeka ambazo awali zilikuwa zikikaguliwa nje. Pia palihitajika kuwa na watumishi wa kutosha hivyo kufanya maamuzi ya ghafla ni kuliingiza Taifa kwenye matatizo makubwa na pengine ilikuwa ni uamuzi wa maslahi binafsi na sio maslahi ya umma.

(vii) Kuifanya nchi yetu kupoteza sifa kimataifa kwa kuonekana ni jalala za bidhaa *fake* zinazohatarisha usalama wa watu na mitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi haya hayalindi usalama na afya za walaji pamoja na mazingira, kuongezeka kwa ushindani usio sawa unaosababishwa na ongezeko la bidhaa duni kutoka nje ya nchi dhidi ya bidhaa zinazozalishwa nchini na hivyo kushindwa kulinda viwanda vya ndani pamoja na kuifanya Tanzania kuwa jalala la bidhaa duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara ya mbolea nchini na nianze na wanufaika wa mbolea ya ruzuku; katika mwaka 2022/2023 wananchi 3,389,951 walijiandikisha kupata mbolea ambapo kati yao wananchi 2,551,239 hawakupata mbolea sawa na 75% pamoja na kwamba walikuwa na sifa zote za kupata mbolea ya ruzuku. Licha ya kuripotiwa kuwa na bakaa ya mbolea ya tani 326,344.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 wakulima waliosajiliwa katika mpango wa mbolea ya ruzuku walifikia 3,910,556. Hotuba ya Waziri haijaeleza idadi ya wanufaika wa mpango wa mbolea ya ruzuku katika mwaka huu wa fedha. Waziri atuambie sababu za kuwafikia wakulima 25% tu huku idadi kubwa ya wakulima wakikosa mbolea ya ruzuku. Ruzuku ya mbolea inayotolewa na Serikali ni haki ya wananchi wote wenye mahitaji. Jambo hili tumelilalamikia hapa Bungeni mwaka jana, lakini huoni hatua za Wizara za kuhakikisha wakulima wote wanapata mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wananchi waliokosa mbolea wanaendeshaje shughuli zao za kilimo? Ruzuku ya mbolea ni kwa ajili ya kundi fulani la wakulima? Hii ni kinyume na kifungu cha 4(1)(h) cha Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009 ambayo inaitaka *TFRA* kuhakikisha kuna usimamizi makini wa uagizaji na usambazaji wa mbolea na kuhakikisha mbolea inapatikana na inawafikia watu wote wenye uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usambazaji wa mbolea, imethibitika kuwa 61% ya wafanyabishara waliosajiliwa katika mpango wa mbolea hawakuuza wala kufanya muamala wowote juu ya mpango wa mbolea ya ruzuku hali ambayo inaathiri usambazaji wa mbolea hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa fedha kugharamia mpango wa mbolea ya ruzuku; katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 *TFRA* na Wizara ya Kilimo walinunua mbolea ya ruzuku yenye thamani ya shilingi bilioni 480 wakati bajeti iliyoruhusiwa na Bunge ilikuwa ni shilingi bilioni 150 hili ni sawa na ongezeko la 220%. Wizara ilipata wapi kibali cha kununua mbolea ya ruzuku

zaidi ya shilingi bilioni 330 ya kiwango kilichoruhusiwa na Bunge, shilingi bilioni 480 zimetumika fedha za walipakodi wanyonge, lakini mbolea ya ruzuku imewafikia wakulima 25% tu nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri kupitia hotuba yake ameshindwa kueleza ni kiasi gani cha fedha kimetumika kugharamia mpango wa mbolea ya ruzuku tangu ulipoanza mwaka 2022/2023, aidha tumekuwa tukimtaka hapa Bungeni kuweka wazi matumizi hayo bila mafanikio. Taarifa za ukaguzi zinaonesha kuwa malimbikizo ya madeni yamefikia shilingi bilioni 262. Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kutosha kuhusu suala hili kwani hana mamlaka kisheria kubadilisha matumizi ya vifungu na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa bei ya mbolea ya ruzuku, ili kupata tija katika utoaji wa mbolea ya ruzuku ni lazima bei zinazotangazwa ziwe halali, wakulima wamudu bei hizo na fedha za umma zitumike kihalali. Pasipo usimamizi imara na kuwepo bei elekezi *(indicative price)* ruzuku inayotolewa haiwezi kuwanufaisha wakulima kwani bei zitaendelea kuwa juu na kuwepo madai hewa ya waagizaji na wasambazaji wa mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana msingi wa mjengeko wa bei na hivyo kwa sehemu kubwa bei inatokana na matamko ya wafanyabiashara, *TFRA* na Wizara kuacha kutumia mfumo wa *BPS* katika kuagiza na kusambaza mbolea nchini na hivyo kuondoa ushindani na manufaa ya ununuzi wa pamoja *(Economies of Scale),* katika mwaka 2022/2023 manunuzi ya kutumia mfumo wa *BPS* ulikuwa 6.3% tu. Hii ni kinyume na Kanuni ya Ununuzi wa Pamoja *(Bulk Procurement Regulation 2017)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *BPS* inataka kufanya uhakiki wa bei katika masoko mbalimbali *(due diligence)* ili kushindanisha wazabuni kwenye soko lenye bei nafuu na kuagiza kwa pamoja ili kupata bei nzuri. Kitendo cha Wizara kuacha mfumo wa *BPS* katika kuagiza mbolea ni kuacha maslahi ya umma na kwa vyovyote bei ya mbolea itabaki juu hata kama kutakuwepo ruzuku na bei elekezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi dhaifu wa bei elekezi; pamoja na kuwepo bei elekezi lakini baadhi ya wauzaji na wasambazaji wa mbolea hawazingatii bei elekezi iliyotangazwa na *TFRA,* imethibitika kuwa wauzaji wengi wa mbolea *(Agro Dealers)* katika *LGA* zaidi ya 80% wanauza kwa bei kubwa tofauti na bei elekezi iliyowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji dhaifu wa bei katika soko la dunia, karibu kila mwezi bei ya mbolea ilikuwa ikishuka, lakini bei ya mbolea hapa nchini ilibaki vilevile hadi Machi, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitendo visivyo vya uadilifu katika mpango wa mbolea ya ruzuku; Wizara na *TFRA* kwa kiwango kikubwa wameshindwa kudhibiti vitendo visivyo vya kiuadilifu katika mpango wa utoaji wa mbolea ya ruzuku hali iliyopelekea kuwepo kwa mbolea *fake*, kuuzwa mbolea isiyosajiliwa, mbolea bandia, kuuzwa kwenye mifuko ya wazi na isiyo na uzito sahihi, wakulima kuuziwa mchanga badala ya mbolea, kuuziwa mbolea iliyokwisha muda wa matumizi, utoroshaji nje ya nchi na kuliingiza Taifa kwenye hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, imebainika kuwa, pia baadhi ya wauzaji wa mbolea, wanajisajili kama wakulima kwa majina hewa na mashamba hewa ili kupata kiwango kikubwa cha mbolea ya ruzuku ili wauze kwa bei ya soko na nje ya nchi. Fedha za umma za wanyonge zinatumika kunufaisha watu binafsi. Haya yote yanafanyika Waziri wa Kilimo na *TFRA* wapo na hatujaona masahihisho yoyote kukabili changamoto hizo. Leo tunaingia bajeti ya mwaka wa tatu tangu mpango huu uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa utoaji wa mbolea ya ruzuku; mwaka jana nililalamikia Wizara ya Kilimo kutumia mfumo wa mbolea ya ruzuku unaoruhusu kufanya udanganyifu kwa kuwa hauna usalama *(security)* kiasi kwamba unaruhusu ku-*scan* kiasi cha *QR Codes* zaidi ya mara moja *(multiple scanning)* inaweza kufanywa na waagizaji, muundaji wa mfumo au haramia mwingine yeyote wa mifumo ya mtandao ili kufanya udanganyifu na kuleta madai hewa ya fedha kwa Serikali, na hapa madhara yake tunayaona Serikali kudaiwa

mabilioni ya fedha huku wakulima waliopata mbolea ni 25% tu. Hii kashfa ni kubwa sana kwa Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imethibitika kuwa Wizara ya Kilimo ilijenga mfumo wa utoaji wa mbolea kupitia kampuni binafsi *(vendor)* na bila ushindani na kuanza kuutumia mfumo huo bila kupata kibali *(clearance)* cha Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)* ambapo ni kinyume na Kifungu cha 24 cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019 *(e-Government Act No. 10 of 2019)* na Kanuni ya 27 ya Kanuni za Serikali Mtandao ya mwaka 2020 pamoja na miongozo yake. Mbaya zaidi hadi sasa *sever* ya mfumo huo inamilikiwa na *vendor* na hivyo anaweza kufanya chochote kama kucheza na takwimu zilizoko kwenye mfumo na kusababisha madai na malipo hewa ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji wa mbolea ya ndani ya nchi; pamoja na nchi yetu kuwa na uzalishaji mkubwa wa mbolea ya samadi na mboji, lakini hakuna mkazo wowote wa Wizara katika kuweka mipango na mikakati ya kuhakikisha kuwa mbolea za samadi na mboji zinasambazwa katika mashamba badala yake Wizara iko *busy* kuweka mpango wa uagizaji mbolea kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mkazo wa kuongeza uzalishaji wa viwanda vya ndani ni wa kinadharia tu kwani Wizara kwa sehemu kubwa inategemea mbolea za kutoka nje ya nchi, mfano mbolea iliyopangwa kutumika katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kutoka viwanda vya ndani vya Mbolea vya *INTRACOM* (Fomi) ni 21% na Minjingu ni 20% ya mbolea inayozalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kuwa kutokana na maelezo niliyoyatoa katika vipengele saba hapo juu inathibitisha kuwa utoaji wa mbolea ya ruzuku unatija ndogo sana kwani unawafikia wakulima 25% tu, mpango huu una mianya mikubwa ya ubadhirifu na hivyo kunufaisha genge la watu wachache huku Serikali ikitumia mabilioni ya fedha za Watanzania kugharamia mpango huo. Bado naamini kuwa kama kungekuwa na usimamizi makini wakulima wengi wangepata mbolea tena kwa bei nafuu na mzigo kwa Serikali ungekuwa

mdogo. Nashauri yafuatayo ambayo pia nitayasimamia katika upitishaji wa Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza utaratibu wa utoaji wa mbolea ya ruzuku usitishwe kwa kuwa umeshindwa kuleta tija kwa wakulima ambapo wanaopata mbolea ni 25% tu huku mabilioni ya fedha za umma yakiendelea kutumika. Serikali ianze kusimamia kikamilifu mfumo wa *BPS* ambao unahakikisha kushuka kwa bei ya mbolea na ndiyo maana tulipoanza kutumia mfumo huu mwaka 2017 bei ya mbolea ilishuka kwa zaidi ya 50% ikilinganishwa na bei iliyokuwepo katika mfumo wa ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, watu wote waliohusika kuliingiza Taifa kwenye hasara kubwa ikiwemo wakulima 75% kukosa mbolea, malipo hewa ya mbolea na matumizi ya fedha za umma nje ya bajeti, wachukuliwe hatua ikiwemo kushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi. Ulinzi wa viwanda vya ndani; katika hotuba ya Waziri wa Mifugo, viwanda vya *TANCHOICE* (hotuba ya Mambo ya Nje), *Hester Bioscience, Farm Base.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa bei za bidhaa na chakula; mabando na vifurushi vya mitandao ya simu, vifaa vya ujenzi na bei za vyakula, sukari, ngano na mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa orodha ya Serikali imebadilika, tutaanza na Mheshimiwa Kihenzile dakika tano, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kupongeza sana Wizara kwa hotuba nzuri. Pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye upande wa uwekezaji na biashara kwa ujumla nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujikita kwenye eneo moja tu. Kwanza kuweza kuliambia Bunge lako Tukufu na

Wabunge kwa ujumla kazi kubwa ambayo imefanyika katika eneo hili ili kuboresha biashara kama roho na *engine* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika miaka hii mitatu au minne ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu amechukua nchi tumejifunza mambo mengi na makubwa. Mfano, miradi iliyokuwepo mwaka 2020 ilikuwa 207 leo tuna miradi ya kibiashara karibu 449. Ajira zilikuwa 17,000 leo zipo 234,000 lakini uwekezaji ulikuwa shilingi trilioni mbili ndani ya miaka mitatu imefika shilingi trilioni 14. Hii ni kazi kubwa sana ambayo imefanyika ambayo inastahili pongezi. Kwenye upande wa sekta yetu ya uchukuzi nasimama kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wetu kazi kubwa ambayo Rais wetu anafanya ni kui-*transform* nchi kuipeleka mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye upande wa bandari mpango wa miaka 10 iliyopita ilikuwa ni kwamba itakapofika mwaka 2025 angalau 2030 tufike angalau mzigo *metric tons* milioni 25 lakini hivi ninavyozungumza tumeshafika milioni 24 na alipokea nchi ikiwa na mzigo tani milioni 18. Kwa hiyo unaweza kuona hata lile lengo sasa tunaanza kuliangalia upya kwa sababu anakimbia kuliko uhalisia na yapo mengi ambayo ameyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira yake ni nini? Ni kuhakikisha kwamba Tanzania inafikia na inanufaika na uchumi wa kijiografia lakini pia inaongoza kwa *rate port* kama wenzetu wa Dubai, hawatengenezi magari lakini magari mengi yanaagizwa kutoka Dubai. Pia, kuwa kituo kikubwa cha biashara na huduma kwenye Ukanda wetu wa *East Africa* pamoja na *SADC*. Nini tumekifanya tunapozungumza? Kwa mfano *Air Tanzania* ilikuwa haifanyi safari zake upande wa Congo ambapo karibu Wabunge wengi hapa sana wamezungumza na yupo Mbunge mmoja ameenda mbele zaidi akasema pengine hatupo *serious.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza tumefungua *Air Tanzania* na inafanya safari zake Lubumbashi, Ndola na tunakwenda kufungua Goma, pamoja na Kinshasa. Hivi

ninavyozungumza tunajenga reli ndefu kuliko zote Barani Afrika yenye urefu wa kilometa zaidi 25,000. Hili halikuwahi kufanyika na reli hii inakwenda mpaka Kigoma kama tulivyosema wakati wote. Ikifika Kigoma tunaweka meli za kutosha katika Ziwa Tanganyika lengo twende Congo. Kwa hiyo Serikali ipo *serious* kuliko wakati mwingine wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapounganisha reli yetu inayotoka pale Uvinza – Gitega - Msongati inakwenda mpaka Congo, yote hiyo maana yake tunaiwinda Congo tuweze kuifikia vizuri zaidi na tayari tupo kwenye hatua za manunuzi kwenye eneo hilo. Kama haitoshi kwenye eneo la reli, *TAZARA* inakwenda kufumuliwa na kuboreshwa upya. Ilipotengenezwa miaka hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya kubeba mzigo wa tani 5,000,000 leo tunakwenda kuongeza uwezo wa reli yetu ili iende mpaka Piliposhi ifike Kolwezi na Lubumbashi, kote huko ni Congo. Kwa hiyo bado tupo *serious* kama Serikali na maono ya Mheshimiwa Rais wetu ni juu kabisa katika Ukanda wetu wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi tunafahamu huwezi kufanya biashara bila kuwa na miundombinu imara, haiwezekani. Ndiyo maana kwenye meli, Serikali hii imewekeza takribani shilingi trilioni moja, haikuwahi kutokea. Moja, kujenga kiwanda kikubwa cha kutengeneza meli pale Tanganyika; mbili kujenga meli kubwa kuliko zote ya tani 3,500 katika Ziwa Tanganyika; kujenga meli kubwa kuliko zote Ziwa Victoria; na kukarabati meli mbalimbali zilizopo katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa. Hapo sikuzungumza kwenye kazi kubwa ya upande wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaboresha bandari zetu, tumefanya uboreshaji mkubwa kule Ujiji, tunafanya uboreshaji mkubwa Kemondo, Bukoba na North Mwanza. Sasa hivi wakandarasi wapo *site* kwenye Bandari ya *Mbamba Bay* lakini kama haitoshi tunafanya maboresho makubwa kwenye Bandari ya Dar es salaam na kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam miaka ya baadaye hatutoweza kuongeza zaidi, tutakwenda kujenga bandari ya Bagamoyo, tunakwenda kujenga Bandari ya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** …yote hii ni kuhakikisha lazima tuwe na miundombinu mizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya, wajiandae Mheshimiwa Profesa Kitila, Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba nianze kuunga mkono hoja. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya. Kwanza ya kuweka uwekezaji mkubwa sana kwenye hii sekta lakini pia kwenye sekta ya miundombinu. Vilevile, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa hotuba nzuri, lakini pia na mipango mizuri sana ambayo ameiainisha kwenye hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita tu kwenye sekta moja tu ya miundombinu na hasa barabara. Nimewasikia wachangiaji wengi wakiwa wanaunganisha biashara na usafirishaji. Ni zaidi ya 70% ya bidhaa zote hupita kwenye barabara na *World Bank* wanasema kama ingekuwa ni mwanadamu barabara ndiyo mirija ya damu. Kwa hiyo ili ufanye biashara yoyote lazima uwe na miundombinu bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la uzalishaji ambako kunazalishwa ili ufike kwenye soko unahitaji Barabara n ani barabara ambazo ni imara iwe ni soko la ndani ama la nje. Ukiwa na miundombinu mizuri unavutia wawekezaji lakini unapunguza muda wa usafiri na usafirishaji, unapunguza gharama za bidhaa kwa sababu kama kuna miundombinu migumu hata gharama za bidhaa unakopeleka huko zitakuwa ngumu. Pia zinapunguza matumizi ya mafuta kwa watu wenye magari. Barabara

zinaunganisha vijiji na wilaya lakini zinaunganisha miji na majiji; na majiji na majiji. Pia ndiyo zinazotoa mazao shambani na kuyafikisha viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulifahamu hili Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuifungua nchi na kuiunganisha Tanzania na nchi zinazotuzunguka kwa kujenga miundombinu bora kabisa ili Tanzania ifanye biashara na mataifa hayo lakini pia kutumia faida ya eneo letu kijiografia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kujenga na ina mipango ya kujenga barabara za kiuchumi na za kimkakati kwa kiwango cha lami. Tunavyoongea sasa hivi tumejenga barabara ya Sumbawanga - *Kasanga Port* kwenda DRC, Sumbawanga – Matai - Kasesya kwenda Zambia ambayo itapunguza sana foleni ya wafanyabiashara pale Tunduma. Mpanda – Ikora - Karema kutoka Mpanda tupo kwenye mpango. Muda wowote tunaanza kuijenga Nyakanazi – Kakonko - Kibondo hadi Kasulu kwenda Burundi tupo kwenye ujenzi. Vilevile, tuna Kibondo - Mabamba kwenda Gitega kwa Makao Makuu ya Burundi; Lusahunga - Rusumo tunarekebisha hiyo barabara. Kuna Murongo kutoka Uganda kwenda Kayanga ambayo itaunganisha na upande wa Burundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mpango wetu ni kujenga barabara kutoka Songea - Likufusi kwenda Mkenda kwa ajili ya kuunganisha na Msumbiji Kaskazini. Pia tuna barabara ya Tunduma - Mpemba kwenda Malawi ambayo tayari imeshakamilika. Tunachofanya ili kurahisisha biashara, Wizara ya Ujenzi imepunguza vituo vingi sana vya yale magari yanayosafirisha, kwa sababu ilikuwa ni kikwazo kikubwa kwa wafanyabiashara zile *transit goods.* Kwa hiyo sasa hivi vipimo vimepunguzwa pia tunajenga miundombinu ambayo ni rafiki sana kwa wafanyabiashara ambayo tunasema ni *way in motion,* mizani ambayo wakati gari inapotembea ndiyo inapopima na hiyo ndiyo ilikuwa kikwazo kikubwa sana kwa wafanyabiashara. Kwa hiyo ni mizani ya kisasa ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia ameamua kuijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto kubwa ya wafanyabiashara ambao wengi wanacheza na muda, kwa mfanyabiashara muda ni mali, ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuboresha majiji yetu na wewe ni shahidi. Pale Jiji la Dar es Salaam anajenga miundombinu mingi sana ili kupunguza muda wa wafanyabiashara…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** … *two* mpaka *three*. *By pass* na *outering* za hapa zinaendelea kujengwa…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitila, Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Mwigulu mjiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imeakisi kikamilifu kabisa vipaumbele vitano ambavyo vipo katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021 – 2025). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie nafasi hii kujibu baadhi ya maoni na hoja za Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni ushauri ni ushauri, tumepokea ushauri wa kuongeza jitihada katika kuvutia uwekezaji kwenye eneo la viwanda na niwatoe tu wasiwasa Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwa sasa kwa kweli miradi mingi ambayo

inasajiliwa na *TIC* ni kwenye eneo la viwanda. Mfano, mwaka jana miradi 506 iliyosajiliwa na *TIC*, miradi 237 ambayo ni asilimia 45 ni kwenye sekta ya viwanda, kwa hiyo sekta ya viwanda ndiyo inaongoza katika kuvutia eneo hili la uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kutaka kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge na wafanyabiashara ambao wamewasilisha hisia zao kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala la uwekezaji pale Ubungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na wafanyabiashara wameonesha hofu kuhusu uwepo wa mradi huu kwamba, unakwenda kuua soko letu la Kariakoo, kwa hiyo ni mradi ambao una changamoto hiyo. Niwatoe hofu kwamba kwanza mimi mwenyewe ni Mbunge wa Jimbo la Ubungo, kwa hiyo mradi huu naufahamu vizuri na ni mradi muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe unafahamu vizuri kwamba Soko la Kariakoo kwa kweli lilianzishwa mwaka 1913 na likawa rasmi 1923 wakati huo Gavana akiwa ni Horace Byatt, Gavana wa kwanza kabisa wa kikoloni, kwa hivyo ni soko la siku nyingi. Serikali ililifanyia maboresho maalum mwaka 1970, ndiyo likawa katika *structure* ambayo tunaiona leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo idadi ya watu Dar es Salaam ilikuwa 357,000, leo tunazungumzia Dar es Salaam watu zaidi ya milioni sita, sasa haiwezekani Soko la Kariakoo likabaki kama lilivyo au likabaki soko moja. Tunatarajia kipindi hiki, tuwe na Kariakoo nyingine nyingi, ziwepo kule Mbagala, Kigoma na maeneo mengine katika nchi hii, kwa hiyo, hilo ni eneo muhimu sana ambalo lazima tulizungumzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunavyozungumza ikikamilika *SGR,* Mji wa Kigoma unatarajiwa kuwa *a trading hub*, inamaanisha kwamba, badala watu wa *DRC* na nchi zingine za jirani kwenda Dar es Salaam kuchuka mzigo, watachukulia pale Kigoma. Sasa mtaanza tena kusema mtaua Kariakoo kwa sababu

ya kuweka *trading hub* pale Kigoma? Kwa hiyo, hiyo haipaswi kuwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, pale tuna nini? Tuna mambo matatu, kwanza tutakuwa na maduka ya jumla na rejareja, tunazungumzia maduka 1,860 na tunavyozungumza tayari maduka 985 yameshachukuliwa na wafanyabishara, nitaeleza baadaye wafanyabiashara gani. Kutakuwa na maonesho ya biashara lakini pia kutakuwa na sehemu ya maghala ya kuhifadhi mizigo pale na forodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumechukua hatua gani? Kwanza, tunapovutia uwekezaji katika nchi hii, tuzingatie mambo mawili ya msingi, moja, hatuwezi kubagua mataifa tukasema taifa hili lije, taifa hili hapana. Pili, lazima tulinde maslahi ya Watanzania. Katika uwekezaji huu pia tumelinda maslahi ya wafanyabiashara wa Tanzania. Juzi tulikuwa nao tulikaa na kuzungumza nao vizuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu kwamba pale maduka yatakayochukuliwa asilimia isiyopungua 95, lazima maduka yale yachukuliwe na Watanzania. Huu utaratibu umewekwa kimkataba na mwekezaji anafahamu, ndiyo maana tunavyozungumza leo, katika maduka 985 ambayo yamechukuliwa na wawekezaji na wafanyabiashara mbalimbali, wale wageni ni watu 15 peke yao, watu 965 ni Watanzania waliobaki ni hao wageni ambao hawazidi 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu mzuri, wafanyabiashara wanafahamu na mimi natoa wito na kuwahamasisha wafanyabiashara wa Kitanzania waende pale wakachukue nafasi za kufanya biashara, wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanafanya biashara, pale kuna fursa kubwa ambayo tunaweza tukafanya biashara, kwa hiyo nawatoa wasiwasi Watanzania kwamba ni muhimu sana iwe katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu, ni suala la *export*. Mheshimiwa Mbunge mmoja ameeleza hapa nadhani ni

Mheshimiwa Luhaga Mpina, kwamba *export* zimeshuka. Tunaposoma takwimu tuzisome takwimu vizuri na tusizisome kwa ujumla wake. Takwimu ambazo tunazo Serikali, *World Bank* na mashirika mengine mbalimbali, mwaka 2002 mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 935, miaka 20 baadaye tulikwenda bilioni 6.4 mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za mwaka jana, mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi yana thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 8.2. Sasa unaposema yameshuka, yameshuka kivipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mauzo haya, bidhaa za kilimo zinachukua nafasi muhimu sana katika mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge tunapotoa takwimu tuzitoe vizuri na kama inakuwa kidogo changamoto, kuna wataalam humu waulize watakusaidia kuchambua ili u-*present* takwimu vizuri. Kwa hiyo, niseme wazi kwamba takwimu ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitoa siyo sahihi. Sahihi ni hizi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho...

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Askofu, Mbunge wa Kawe kwamba, Dira ya Taifa ya Maendeleo ambayo tunaiandaa kwa sasa kuelekea mwaka 2050 itazingatia yote ambayo mmeyasema na itakiwa ni dira yenye maono kamili. Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, kabla Bunge hili halijaisha kutakuwa na semina ama mkutano wa pamoja ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kutoa maoni yao katika Dira hii kabla ya uiingiza humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kutoa ufafanuzi huo, naomba nami niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Mwigulu ujiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, pili nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo imekuwa na *clarity* na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nianze kwanza kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa maoni yao na yale ya ushauri tutayachukua *especially* kwenye eneo la *coordination,* tunaendelea kujenga msingi imara kati ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara katika eneo la ushirikiano. Hata hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha, mfano eneo la viwanda vidogo, Wabunge wameona tunavyoshirikiana, watu wa *TEMDO*, watu wa Bodi ya Sukari, Wizara ya Kilimo inatoa fedha tunashirikiana pamoja kuzalisha hivi viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo muda mrefu naamini kwamba mwekezaji aliyeko Simiyu atapata kile kiwanda kidogo na tutam-*support*. Tumekubaliana ndani ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda kwamba, tutam-*support* mwekezaji huyu kuwa *modal farmer* ambaye ana-*process* sukari mwenyewe kutoka miwa, kuzalisha sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, kuna hoja ya viwanda vya chai. Kwanza, chai tunayo changamoto ni *global case*, ni *issue* ya dunia lakini Serikali inachukua hatua zingine. Kati ya viwanda 24 tulivyonavyo katika nchi, viwanda saba vimefungwa na viwanda hivi saba vitatu ni vya Mohamed *Enterprises*, viwili ni vya *DL Group*, kimoja tuna ki-*unlock*, tunamshukuru Mbunge wa Lupembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, dhana ya kuamini kwamba wakulima wetu wadogo hawawezi ku-*run* viwanda imeweza kuwa *proven wrong* katika eneo la Lupembe. Mkulima mdogo aliyekuwa napeleka chai kiwandani na kutokulipwa, alituomba tumpe leseni ya yeye kuendesha kiwanda. Mwanzo alianza kuchakata chai

yake na ya wakulima wadogo wenzie na alikuwa anaifunga kwenye mifuko ya kilo 50, leo anafanya *proper branding* na chai yake inaitwa Chai Imara na ameshaanza kuuza vizuri, Serikali tutam-*support* ku-*run* kiwanda chake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutamlipa *Dhow Mercantile Investment* aliyofanya ili aondoke kwenye kile kiwanda na kile kiwanda kishikiliwe na wakulima wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe alitaka kujua tunajenga viwanda vingapi. Mpango wa Serikali ni kujenga viwanda saba na mwaka ujao wa fedha tunaanza na viwanda viwili. Tumeanza kufufua shamba la chai la Kilolo ambalo liko katika Mkoa wa Iringa, tumeshatoa fedha ya kufufua na sasa tumefunga *weathering machine* tukishirikiana na *development partner* na Julai tutanunua Kiwanda cha CTC na Kiwanda cha Orthodox *Tea* ili wakulima wa pale waweze ku-*export* chai na kuuza *black tea* wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, nataka nichangie kwenye eneo la *export*, amesema Mheshimiwa Kitila. Ni vizuri tukiwa tunachukua takwimu tuchukue 360. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda kwenye kitabu chake hiki amefanya *selected market*, amechagua masoko matano tu kuyaoneshea takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amechagua Soko la *AGOA*, Soko la *Free Trade Africa*, Soko la *EU* na Soko la *UAE*. Ni *selected market* na anapo-*report* export, ana-*report export* kwa ujumla lakini hapa kachukua mifano ya masoko matano ambayo kati ya matano, masoko manne tumeanguka *export* yetu, haina maana kwamba *export docket* yote imeanguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapochukua *data* za kuangalia *export* ni vizuri uchukue *data* za *source* kwa maana ya eneo ambalo *export* ina-*originate*, chukua *data* za *TRA*, chukua *data* za *Central Bank* na *data* za *National Bureau of Statistics* ili uweze ku-*inform* umma juu ya takwimu sahihi za *data*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo nataka niongelee ni kuhusu alizeti. Ni kweli tuna-*import* mafuta ya kula na ni *disincentives* kwa wakulima wetu, tunachukua hatua gani kwa mwaka ujao wa fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kwanza tunayochukua ni kwamba kama Serikali..

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina nakuomba ukae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumepeleka mapendekezo Wizara ya Fedha, kuchua *measure* mbili. *Measure* ya kwanza tunataka tuanze utaratibu wa *quoter importation*. Kwamba mafuta yatakayoingia ndani ya nchi ni *gap* tu uki-*compare* na kile ambacho viwanda vyetu vya ndani vinazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tumepeleka mapendekezo tunajadiliana na Wizara ya Fedha, tutaongeza kodi na Bunge lako Tukufu likipitisha kwenye *crude oil*, *semi refined oil* na *refined oil* ya *pam oil* inayotoka nje ili kuwalinda wakulima wetu wa ndani waweze kuzalisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wetu wa alizeti sasa umeongezeka. Mwaka jana wakulima wamezalisha sana alizeti, mwaka huu kidogo wamepata *disincentives* kwa sababu ya bei ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo nataka niongelee ni eneo la mbolea.  Naomba tu niijibu hii hoja *specific* kwa Mheshimiwa Mpina, amelia mara mbili ndani ya Bunge lako Tukufu. Ni hivi, ruzuku ya mbolea anachukua *absolute number*, kwamba mfumo wa usajili umesajili wakulima milioni tatu, waliofaidika na mbolea ya ruzuku ni 25% tu ni *wrong analysis*, kwa sababu mfumo wa ruzuku hu-*focus* mbolea *selected DAP, Urea, CAN, SA* na *NPK*, kwa ajili ya mazao ya mahindi na mazao ya chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *data base* ya usajili wa wakulima, tumesajili wakulima wa korosho hawatumii *urea* wala *DAP*. Kwa hiyo, unapoenda kuchukua *data* hiyo unaupotosha umma.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, nimekuomba ukae na hayo ndiyo maelekezo ya Kiti.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, unapoenda kuchukua *data* za ruzuku ya mbolea ya tumbaku haimo. Unapoenda kuchukua *data* ya ruzuku ya pamba, *data* za usajili wa wakulima tunasajili wakulima wote lakini siyo kila mkulima anafaidika na *measure* ya ruzuku iliyotolewa na Serikali, kwa hiyo, 25% anaowaona ni wakulima wa mazao ya chakula na utumiaji wetu wa mbolea, ukichukua kwa takwimu za miaka mitatu, umetoka wastani wa tani 350,000 mwaka huu Juni, tutafika tani 900,000, lengo letu ni kufika tani 1,000,000 ya matumizi ya mbolea ili *per hector* tuweze kufika kilo 50 kwa wakulima wa mahindi, mpunga na mazao ya chakula, hilo ndiyo lengo la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali inatoa ruzuku? Inatoa ruzuku kwa sababu tatu, matumizi ya mbolea yana mambo matatu, yana *affordability, availability* na suala la *knowledge*. *Affordability* ndiyo Serikali inachokichukua sasa inapunguza bei. *Availability* ndiyo tunaongeza mtandao wa wasambazaji na suala linalofuatia ni suala la uelewa. Leo ukija kwangu Nzega, hawatumii mbolea ya kemikali, wanataka watumie mbolea ya samadi. Kwa hiyo, ni vizuri hili jambo tukalitazama kwa mtazamo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa chakula kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, tumefika tani milioni 20 ya chakula katika nchi yetu. Msimu huu wa kilimo tunatarajia tutafika tani milioni 24 ambayo *it is a record* hatujawahi kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tumeanza kuuza mazao. Hivi sasa tumeanza kuuza unga, *WFP* wametaka mahindi, tumewaambia chakula mnachopeleka Malawi, pelekeni unga. Sasa hivi tunasaga unga kwenye viwanda vyetu. Jana tumesaini makubaliano na *DRC* Congo, kupeleka mahindi zaidi ya *metric tons* laki tano na tunauza kwa dola siyo shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaombe wakulima, nimeanza kupokea meseji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, siyo muda mrefu tutatangaza bei elekezi ya mahindi na wakulima kuanza kuuza kupitia *NFRA*. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mwigulu, wajiandae Mheshimiwa Naibu Waziri Kigahe na mtoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia maeneo ambayo yamejitokeza. Kwanza, naunga mkono hoja na jambo la pili, tumezipokea hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge zile hoja zote ambazo zinahusisha masuala ya hatua za kikodi, waridhie kwamba tumeyapokea na tarehe 25 na tarehe 26 tutakuwa na kikao cha wadau wote kwa ajili ya kujadili hatua mpya za kikodi na tutazileta Bunge hapa kwa ajili ya mjadala kabla hazijapitishwa kwa ajili ya kutumika kama sheria mpya za kikodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema katika kipindi ambacho nilikuwa najibu maswali narudia tena, masuala haya ya kikodi ni masuala ya kisheria na kila hatua ambayo tunaipitisha kama Bunge, inapokwenda kwenye hatua za kutekelezwa ni sheria ambayo kila mtu anatakiwa aifuate.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na taasisi zingine zote hapa nchini zinazokusanya kodi, hazitungi sheria, zenyewe zinatekeleza sheria. Kwa hiyo, tunapojadili muda huu na tunaelekea kwenye kujadili sheria ya fedha ambayo itakuwa na hatua za kikodi, itakuwa ni muda muafaka sana wa kujadili sheria zote zile ambazo tunaona zina ukakasi ili kuweza kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la msingi pia hilo tukakubaliana na tunandaa sisi kama watu wa Wizara ya Fedha kuanzia tarehe moja tutakuwa na semina ambazo zitafanywa kwa Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kuelewana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye haya masuala ya kodi, tuna aina nyingi za kodi, mojawapo bila kutaja kwa mtiririko wake, tukitaja kwa makundi ya walipakodi. Tunalo kundi la walipa kodi linaitwa wafanyakazi wanakatwa kwenye mishahara yao. Hili ni kundi ambalo ulipaji wake hauna kelele, pale anapopokea inakuwa imekatwa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wamegawanyika kwenye makundi mengi tu, kuna wafanyakazi ambao kipato chao ni kidogo sana, wanalipa kodi 100%. Kuna wakati na kuna ambao kipato chao ni cha wastani na kuna wale ambao kipato chao kina unafuu wanalipa kodi 100%. Hizo kodi zinakwenda kwenye shughuli za maendeleo, hazifanyi kazi za familia za *TRA*, inakwenda kufanya kazi za maendeleo ya nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna walipakodi wadogo, wapo wanalipa kodi vizuri kabisa, tunalo kundi la walipakodi wakubwa na tuna kundi la walipakodi wanaokusanya kodi kwa niaba ya Serikali wale waliosajiliwa *VAT,* kodi siyo ya kwake, siyo yeye anayelipwa, yeye anatumika kama mkusanyaji wa kodi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inatokea mtu ambaye amekusanya kodi ya Serikali, anatakiwa aiwasilishe, siyo yeye aliyelipa, amekusanya kodi za walipakodi wengine, yeye amekusanya kama wakala wa kukusanya, anatakiwa aiwasilishe

Serikalini. Inatokea mwezi wa kwanza hajawasilisha, mwezi wa pili hajawasilisha, mwezi wa tatu hajawasilisha, mwaka hajawasilisha, mwaka wa pili hajawasilisha na mwaka wa tatu hajawasilisha. Ametumia kodi ya walipakodi wengine, kaichukua, anatembea anaonekana tajiri kumbe kachukua kodi ambayo walipakodi wamelipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa aina hii hata ipite miaka mingapi, huyu ni mwizi kama mwizi mwingine na mimi nikiwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hawa lazima walipe kodi ili watoto wa maskini waweze kusoma. Hatutawaacha kwa sababu imepita miaka. Lieleweke vizuri hili, mtu ambaye amekusanya kodi kwa niaba ya Serikali, anatakiwa aiwasilishe kodi hiyo Serikalini, hii haina mwezi, haina mwaka, anatakiwa aiwasilishe kodi Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Mheshimiwa Rais aliposema akiwa Kagera alikuwa anaongelea walipa kodi hawa wadogo wadogo. Wanasumbuliwa walipa kodi wadogo wadogo ambao hawajui hata kutunza takwimu lakini mtu ambaye ni mlipakodi mkubwa amesajiliwa *VAT,* amekusanya kodi ya Serikali kwa niaba ya Serikali, amechukua fedha ya Watanzania ambayo inatakiwa ikajenge madarasa, ikatoe dawa mahospitalini, ikasomeshe watoto wa maskini, ikajenge barabara hawezi kuigeuza hiyo kuwa fedha yake. Tutaenda naye sambamba hata kama imepita miaka ya kutosha ni lazima ailipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuelewane vizuri, hii ni Sheria. Sheria inasema mtu yeyote akikusanya kodi ya Serikali anatakiwa aifikishe Serikalini. Hawezi akawa mjanja kwa sababu amekwepa miaka miwili au mitatu kwamba yeye fedha ya Serikali anaifanya iwe ya kwake na tumuangalie tu kwamba ni mjanja, hatuwezi tukafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutamkamata hatuwezi tukamuacha. Mheshimiwa Mbunge alichangia kwamba tunapofanya hivi mimi nichongewe. Nasema wakati mimi nikiwa Waziri wa Fedha, mtu yeyote anayekusanya fedha ya Serikali ni lazima aifikishe Serikalini. Hatuwezi mtu mmoja akaonekana tajiri

kwa kuchukua fedha za Watanzania na kujigeuza yeye ni Benki Kuu. Akachukua fedha ya Watanzania halafu mama wajawazito kule wakose dawa hospitalini na wanafunzi wa vyuo vikuu wakose fedha tumuachie yeye aonekane ni tajiri kwa kukusanya fedha ya Serikali. Amekwepa kwepa miaka miwili imeshapita kwa hiyo asamehewe. Nikiwa Waziri wa Fedha msamaha huo haupo. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca kaa chini tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukaendelea kuwaonea wafanyabiashara wadogo wadogo, tukaendelea na Watanzania maskini kwa sababu hawawezi kukwepa halafu wengine wakakusanya fedha ya Serikali tukawaachia, hilo halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yeyote ambaye anakusanya fedha ya Serikali lazima ifike Serikalini. Ninachokisema hiki kwenye wakusanyaji nasema na kwa watumiaji. Hatuwezi tukakusanya fedha ya Watanzania maskini maskini hawa ikawa kubwa halafu mtu mwingine ajichotee, hilo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kundi hili ninalosema lipo na la wale ambao wanakata rufaa kupinga maamuzi. Kuna wengine wapo kwenye bodi ya zabuni. Hawa ambao wapo kwenye bodi za zabuni kwa ajili ya utawala bora tunawasikiliza. Wanapata kusikilizwa hatua zote zile lakini na jambo lile lina kodi takribani shilingi trilioni 6.5 ambao kesi zao zimeenda kwenye bodi ya zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wapo kwenye bodi za zabuni shilingi trilioni 6.5, shilingi trilioni 3.2 uamuzi umeshafanyika. Kuna walioshinda na kuna wale ambao bodi ya zabuni imeelekeza wanatakiwa walipe. Wanatakiwa walipe kodi ya Serikali ili tuweze kukamilisha miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili bajeti katika kipindi ambacho nchi yetu inajenga reli yenye urefu mkubwa kwenye nchi tano duniani. Tanzania inaingia kwenye nchi tano duniani zenye urefu mkubwa zaidi wa reli. Tanzania tunajadili bajeti katika kipindi ambacho tunatekeleza Mradi wa Bwawa la Umeme ambao utakuwa na *megawatt* za kutosha kwenye miradi ya mara moja. Ni mojawapo ya mradi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga katika kipindi ambacho nchi yetu ina idadi kubwa zaidi ya wanafunzi wa vyuo vikuu ambao wanasoma kwa fedha za Serikali. Tunajadili bajeti katika kipindi ambacho nchi yetu inatekeleza miradi mikubwa zaidi ya umwagiliaji kwa ajili ya kubadilisha maisha ya Watanzania walio chini. Tunapeleka zaidi ya shilingi bilioni 50 kwenye vijiji kubadilisha maisha ya Watanzania waliopo vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukatokea wale ambao walishapata neema ya kuchuma wakawa matajiri halafu tukawaacha tukimbizane na wafanyakazi, walimu wa shule ya msingi, nesi na wafanyabiashara wadogo wadogo huku wale wakubwa wakiwa wanakusanya fedha ya Serikali na kukaa nayo. Hili halikubaliki na niwaelekeze Mamlaka ya Mapato Tanzania wakati mimi nikiwa Waziri wala wasicheke na mtu yeyote anayekusanya fedha ya Serikali na kuigeuza ni fedha yake binafsi. Lazima fedha hiyo iende kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao wapo kwenye Baraza la Rufani za Kodi ni takribani shilingi trilioni mbili, tunawapa fursa hiyo ya kusikilizwa. Suala la kulipa kodi ni wajibu, hii siyo ombi...

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii wala siyo hisani. Mtu yeyote ambaye anatakiwa kulipa kodi ni wajibu anatakiwa alipe kodi. Hata nchi zilizoendelea wanaweza wakacheka kwenye mambo mengine yote, wakachekeana

kwenye siasa lakini linapofika jambo la kujenga nchi hapo halina mzaha na hili hata sisi hatutafanya mzaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naunga mkono katika vipindi vyote ambavyo mimi nimekuwa na akili timamu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Serikali ambayo imesikiliza Sekta Binafsi na kuwafanyia *fair* kama Serikali ya Awamu ya Sita. Inawafanyia *fair* kwa kiwango ambacho hata mtu ambaye fedha yake nyingi imekusanywa zaidi Mheshimiwa Rais anaelekeza arudishiwe. Utapata wapi mamlaka ambayo inalinda Sekta Binafsi kama hiyo? Hii hai... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umeshaeleweka. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri umeshaeleweka na muda wako umekwisha. Kitu cha msingi hizo shilingi trilioni tatu mliyokubaliana zilipwe, ahsante.

Sasa namwita Mheshimiwa Kigahe. Mheshimiwa Mpina nakuomba ukae.

Mheshimiwa Kigahe, mtoa hoja jiandae.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia katika kujadili bajeti hii muhimu siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii muhimu ya Viwanda na Biashara. Pia, kwa namna ya pekee nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa

kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha anavutia wawekezaji katika Sekta ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu mahiri Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji ambaye kwa kweli ni daktari wa kweli, mwalimu wangu na dada yangu kwa kuendelea kunielekeza na kunifundisha kazi ili niweze kumsaidia katika nafasi hii ya Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kulishukuru Bunge lako, kumshukuru Mheshimiwa Spika wetu kwa kutuendesha vizuri katika shughuli mbalimbali hapa Bungeni. Pia, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wenyeviti wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuendelea kufanya kazi nasi kwa weledi mkubwa na kutuelekeza katika shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayofanya, lakini mahususi leo hii wanapochangia katika Wizara hii muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwapa pole Watanzania wenzangu kuhusiana na mvua kubwa zilizonyesha mwaka huu. Maeneo mengi kumetokewa na maafa na uharibifu wa miundombinu. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa ametoa fedha nyingi

kurekebisha miundombinu hiyo lakini pia na wale ambao wamepata maafa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru kwa sababu nami katika jimbo langu la Mufindi Kaskazini tulipata changamoto katika miundombinu ya barabara lakini Mheshimiwa Rais ametusaidia na kutupa uwezo wa kurekebisha maeneo ambayo yalikuwa yameharibika. Kwa hiyo niwahakikishie wananchi wenzangu na wapiga kura wangu wa Jimbo la Mufundi Kaskazini kwamba nawawakilisha vizuri na changamoto hizi tutaendelea kuzitatua kadri ambavyo zinatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nishukuru familia yangu kwa kuwa wamekuwa bega kwa bega nami katika kuhakikisha natimiza wajibu wangu katika majukumu yangu kama Naibu Waziri katika Sekta hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nichukue sasa nafasi hii na mimi kuchangia hoja hii muhimu ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara mahususi kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge katika mjadala huu wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba katika hoja nyingi zilizotolewa nyingi zimelenga katika kuhakikisha tunaimarisha sekta ndogo kwa maana kuhakikisha wajasiriamali *(SME*'s) wanakua na kufanikiwa. Historia inatuambia maendeleo yote duniani yametokana na kukuza sekta ndogo (biashara ndogo na viwanda vidogo).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu zetu hapa Tanzania zaidi ya 95% ya biashara zote ni ndogo sana. Mchango wa *GDP* wa sekta hii au wa biashara hizi ndogo sana ni zaidi ya 35%. Zaidi ya 54% ya *SME* hizi ambazo ndiyo zinachangia maendeleo makubwa katika nchi hii zinafanywa au shughuli zake zinafanywa na kina mama na hasa kwenye eneo la shughuli za kilimo pamoja na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana leo hii Waheshimiwa Wabunge wengi wanachangia kuhusiana na kuhakikisha tunaimarisha uongezaji wa thamani kwa kuwa na viwanda vidogo na kuboresha biashara ndogo kwenye maeneo mbalimbali. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge na ndiyo maana sisi kama Wizara tumeanza kupitia sera yetu ya *SME* ambayo tunataka sasa iendane na mahitaji halisi ya sasa kwenye Sekta hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunajua umuhimu wa usalama na afya ya wananchi tunapozalisha bidhaa hizi katika viwanda vyetu vidogo. Mahususi sasa nianze kuchangia kwenye hoja mbalimbali ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge. Moja ni hii ambayo Mheshimiwa Sichalwe ameisema na wengine wameisema kwenye maeneo mbalimbali kuhusu bidhaa mbalimbali ikiwemo pombe kali na pombe nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, atakuwa shahidi na yeye kwamba tayari timu yetu ya viwanda na biashara kwa maana *SIDO* na *TBS* wameshatembelea maeneo mbalimbali ikiwemo Mkoa wa Songwe na kule Momba wameenda. Moja ya kazi tuliyokuwa tunafanya ni kuhakikisha tunaaza kuwasaidia wazalishaji wadogo kuwa na maeneo sahihi ya uzalishaji kwa maana ya majengo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuwapa elimu ya kuzalisha kwa ubora. Sasa tumeshatenga zaidi ya shilingi milioni 300 zinatumika kwa ajili hii, si tu katika bidhaa hizi za pombe na vinywaji vikali lakini pia katika bidhaa zote kwa wajasiriamali wadogo. Kwa hiyo *SIDO* na *TBS* wanashirikiana na Serikali imetoa fedha zaidi ya shilingi milioni 300 ambazo zinalipiwa kupata nembo ya ubora kwa wazalishaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoenda kufuata sasa ni hizi teknolojia sahihi na rahisi ambazo kupitia Shirika letu la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda *(TIRDO)* tutaenda sasa kuwapa wale ambao watakuwa tumewafundisha namna ya kuzalisha ili wawe na mitambo midogo midogo ya kuweza kufanya *distillation* ya hizi

pombe kali ili kulinda usalama wa wanywaji au watumiaji wa bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya tathmini hizi lengo kubwa litakuwa sasa kusaidia au kubuni mitambo midogo ambayo itawasaidia wazalishaji wa pombe pale Momba na maeneo mengine ili waweze kuzalisha vinjwaji hivi vikali kwa usalama. Pia, tunazingatia ubora na usalama wa afya za walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi katika eneo hili Wizara inahakikisha tunaenda kuwasaidia vifungashio. Ndiyo maana ili waweze kuingia kweye Soko la Afrika Mashariki na Soko la Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na eneo la biashara la Afrika lazima tuwe na vifungashio vizuri na vya kisasa ambavyo bidhaa hizo zitakazozalishwa vitaweza kufungashwa ili tuweze kuuza katika masoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kuna wazalishaji wengi wa pombe kali ambao wameshasajiliwa na wanazalisha vizuri. Kwa hiyo tutaendelea kuwasaidia na wengine ambao wanazalisha vinywaji katika nchi yetu. Pia, kumeongelewa kuhusiana na uongezaji thamani kwenye mazao yetu ya kilimo ikiwemo parachichi na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mipango yetu kupitia *SIDO* na taasisi zetu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema. Tunabuni teknolojia mbalimbali za kuchakata mazao mbalimbali. Wamesema wenyewe Wabunge hapa kama Mheshimiwa Waziri alivyosema kwenye bajeti kuna ile *mini plant* ya kuzalisha sukari ambapo mitambo hii midogo itawawezesha wazalishaji wadogo wadogo ambao watalima miwa na mazao mengine kuweza kuongeza thamani ili tuweze kupata thamani ya uwekezaji katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwa sababu najua upotevu baada ya uzalishaji *(post harvest losses)* katika maeneo mengi ikiwemo alichosema Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe kuhusu parachichi na

maeneo mengine. Tunajua baada ya Mheshimiwa Rais kuweka fedha nyingi sana kwenye Sekta ya Kilimo maana yake uzalishaji utakuwa mkubwa. Kwa hiyo kutoka pale sisi lazima tuchukue na wamesema vizuri sana kwamba kuwe na *BBT* ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndilo linalokwenda ili tuwe na mitaa au majengo ya viwanda *(industrial parks)* ambapo humo sasa wajasiriamali wetu wengi ambao hawana uwezo wa kujenga majengo ya viwanda waweze kuleta mashine zao kwa kusaidiwa na *SIDO* na wengine kuingiza kutoka nje wakaweka mle na kuweza kuongeza thamani mazao yetu. Kwa hiyo kule Lupembe na maeneo mengine nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge waandae maeneo ambapo sisi tukishapata bajeti sasa tueze kujenga majengo haya ya viwanda ambapo humo wawekezaji au wajasiriamali wengi wataweka mashine na kuongeza thamani mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba katika maeneo ambayo yameongelewa na Waheshimiwa Wabunge, moja; waliongelea kuhusiana na changamoto ya lumbesa. Kupitia wakala wa vipimo *(WMA)* tumeendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusiana na changamoto ya lumbesa. Lumbesa ni neno maarufu ambalo linahusisha ufungashaji usiokuwa rasmi kwenye magunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo haya yamekuwa na maneno tofauti tofauti. Kuna lumbesa, kangomba, ndonya na kadhalika. Hii maana yake ni nini? Ni mauzo ya mazao ya kilimo kwa kutokufuata vipimo vya uzito kutumia mizani. Tumekuwa tukishughulikia tatizo hili kwa muda mrefu, lakini sasa Serikali kupitia Wizara yetu tumeshachukua hatua mahususi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumeunda kikosi kazi mahususi ambacho kinasimamiwa na Wizara yetu kwa kuhusisha Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo na kwa kupitia wakala wa vipimo ambao moja ya kazi yake ni kuhakikisha tunaendelea kutoa elimu. Tunatoa elimu kwa wakulima, wafanyabiashara na zaidi tunataka wenzetu wa

TAMISEMI waweze kuweka maeneo ya kuuzia *(collection centres)* ambapo hapo sisi kupitia wakala wa vipimo tutapeleka mizani ili wakulima waweze kuuza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumeshaanza kulifanya na tayari sasa tumepita katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Manyara, Mbeya, Iringa na Njombe. Tunafanya hivyo kwa kushirikiana pia na *TBS* ili kutoa elimu ya kutunza ubora wa mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mazao ya nafaka tunawapa elimu wakulima kuhusiana na sumu kuvu kwamba namna ya kuvuna, namna ya kutunza, kuanika na kuweza kuyapaki ili yaweze kuingia sokoni yakiwa na ubora. Hali kadhalika na mazao mengine ambayo ni kama viazi na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi kama Wizara tutahakikisha tunaendelea kusimamia hili. Tayari tulishaanza *operation* maalum kupitia wakala wa vipimo katika mikoa tisa kwa maana ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Iringa na Njombe. Zoezi hili kwa taarifa yako, zaidi ya magari 2,500 yaliyokuwa yanasafirisha mazao yalikaguliwa na kati ya magari hayo, magari 2,419 yalikutwa na mazao yaliyofungashwa kwa uzito unaoruhusiwa yaani usiozidi kilogramu 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari 81 yalikutwa na makosa kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, Sura 340 ambapo hatua mbalimbali stahiki zilichukuliwa. Zoezi hili linaendelea na tutahakikisha wale wote ambao wanaleta shida na hasa kuwapa hasara wakulima wanachukuliwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo kuhusiana na umuhimu wa Shirika letu la Kuendeleza Viwanda Vidogo Tanzania *(SIDO)*. Shirika hili ni muhimu sana na limekuwa likisaidia wajasiriamali wengi. Moja, kwa kuwapa teknolojia rahisi ambazo zinawasaidia kuongeza thamani; na pili, kutoa mitaji, kwa maana ya mikopo nafuu kwa wajasiriamali hao wadogo ambao kwa

wakati mwingine hawawezi kukopesheka kwenye taasisi zetu za fedha na pia ambazo zinatoa riba kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* tunatoa mikopo kwa asilimia tisa, huwezi kuipata hii kwenye maeneo mengine kote ambako wanatoa mikopo hiyo; na wengine ukienda kwenye benki, kama nilivyosema, hawakopesheki.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi tumeanzisha mafunzo atamizi kwa kupitia Chuo chetu cha Elimu ya Biashara *(CBE)*. Tunafanya hivi ili kuwawezesha vijana wetu wengi waweze kujiajiri kwa kuanzisha biashara mbalimbali. Pia kuwawezesha kupata mikopo kupitia *SIDO;* na zaidi sasa kuwawezesha kupata teknolojia rahisi ambazo zinabuniwa na Shirika letu la *TEMDO* na kuzalishwa na shirika hilo kwa kushirikiana na *SIDO* na wajasiriamali wengine ambao wanachukua teknolojia hizo na kuzizalisha na kuwagawia wajasiriamali hao ili kuweza kufanya kazi ya kuzalisha na kuongeza thamani mazao yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuipitishe ili mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri wangu ameyasema hapa yaweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 34(2) tunaendelea na kazi yetu mpaka shughuli yetu ya leo iishe. Mheshimiwa Ashatu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amefanikisha majadiliano haya, kwenye sekta hii ya viwanda na biashara ndani ya siku hizi mbili ambazo tumekaa hapa ili kujadili yale yote yanayoendelea kwenye sekta hii muhimu kwa ujenzi wa Taifa letu na uchumi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa jinsi ulivyoendesha mjadala huu tangu jana tulipowasilisha hotuba yetu na hadi muda huu tunapoelekea kuhitimisha majadiliano haya. Pia, niruhusu niwashukuru sana Kamati ya Bunge ya Viwanda, Kilimo, Biashara na Mifugo kwa kazi nzuri waliyoifanya tulipowasilisha taarifa yetu kwenye Kamati na taarifa yao waliyoiwasilisha hapa. Naomba kumwambia Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwamba tumepokea pongezi walizotupatia sisi tunaofanya kazi kwenye Wizara hii. Pia tumepokea ushauri na maelekezo waliyotupatia kwa ajili ya kuiboresha Sekta hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi nzuri waliyoifanya kuanzia jana ya kujadili kwa kina kuhusu sekta yetu hii, fursa tulizonazo na changamoto ambazo wafanyabiashara wetu wanapitia kwa pamoja. Nikisema wafanyabiashara, hata wenye viwanda ni wafanyabiashara, kwa hiyo nikisema wafanyabiashara naomba ijulikane hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Bunge lako Tukufu kwamba tumepokea maoni, maelekezo na ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Pia, tumepokea pongezi, ahsanteni sana sana, kiukweli tulikoanzia na tulipo hapafanani, tunapiga hatua, nawashukuruni sana. Mijadala yenu imeonesha umuhimu wa sekta yetu hii kwenye uchumi wa Taifa letu kama ambavyo Serikali yetu ya Awamu ya Sita inavyoweka msukumo mkubwa kwenye eneo hili. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka msisitizo mkubwa kuhakikisha malighafi zinazozalishwa hapa nchini zinachakatwa, zinaongezwa thamani kabla hazijapelekwa nje ya mipaka ya Taifa letu. Niwashukuru sana kwa uelekeo huo ambao ni maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo nasi tumeanza kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu pamoja na Naibu Mawaziri

ambao wamejibu hoja hizi na kutoa ufafanuzi wa maeneo yale ambayo yapo kwenye sekta zao wanazozisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Exaud Kigahe kwa kazi nzuri anayoifanya pale Wizarani na Jimboni kwake pale Mufindi Kaskazini. Naomba niwaambie wapiga kura wake na wajumbe, hasa wajumbe wanaye Mbunge makini sana, wanaye mchapa kazi anayefanya kazi nzuri sana. Wandelee kumuunga mkono. Kwa kuwa kule Kondoa wameamua kuniachia lile jimbo basi muda ukifika nitahamia Mufindi Kaskazini ili nimsaidie kule kwa wajumbe. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kutuletea kiongozi makini na mahiri anayeifanya kazi yake vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naomba tena nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utayari wake wa kuona malighafi za Watanzania zinachakatwa ndani ya Taifa letu, tunaongeza thamani, zaidi kwa kufungua mipaka ya Taifa letu na sasa tunapeleka bidhaa zetu kwenye masoko mbalimbali, nje ya mipaka ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri walioongelea kuhusu utofauti wa takwimu. Ni kwamba takwimu zilizotolewa na Waziri wa Kilimo ni takwimu za mazao ya kilimo hivyo haziwezi kufanana na takwimu ninazozitoa mimi Waziri wa Biashara. Kwa hiyo kwa hilo naomba nimwombe sana ndugu yangu Mheshimiwa Mpina, asiwe ana-*focus* sana kwenye kutafuta makosa ataishia kuonekana makosa kwake mwenyewe. Kwa hili nimwombe sana kaka yangu, ni muhimu sana akaangalia yale mema mazuri ambayo yanafanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita, ili tuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais kwenye huduma anazozifanya na utumishi wake mwema kwa wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, nitasema machache sana kwenye hoja ambazo nyingi zimesemwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwenye eneo letu...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuwe na utulivu, tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** ... kwenye eneo hili la Viwanda na Biashara. Naomba nianze kwenye Mradi wetu wa Mchuchuma na Liganga. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwama kama ilivyo kawaida wameendelea kuusemea mradi huu kwa nguvu kubwa na maono makubwa waliyokuwa nayo viongozi wetu tangu Awamu ya Kwanza mpaka Awamu ya Sita. Sisi ambao tumepewa dhamana ya kusimamia eneo hili, kama nilivyoeleza jana kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara yetu; moja, naendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kutoa bilioni 15.42 za ulipaji wa fidia. Hakutoa bilioni 15 tu, alitoa na maelekezo fedha hizi tunazozipeleka kwa wananchi, wananchi hawa wakapewe elimu ili wanapopokea fedha hizi ziweze kubadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliifanya kazi hii kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ludewa, nimpongeze sana kaka yangu, kazi yake ni njema na ameleta mrejesho, kwamba zile fedha na elimu iliyotolewa kwa niaba ya mama mpenda watoto wake wa Kitanzania imefanya kazi. Moja ya kijiji wameweza kuwekeza kwenye *bond*. Tulikwenda na taasisi zetu za kifedha tukatoa elimu na elimu imefanya kazi. Naomba niendelee kumshawishi Mheshimiwa Mbunge, aendelee na vile vijiji vingine, wafanye hivyo ili maisha yao yaboreke kupitia fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemaliza kulipa fidia, wamebaki hao wachache ambao hawajaonekana. Hatua ya pili inayofuata ni kutwaa lile eneo kama nilivyosema jana. Namshukuru kaka yangu Mheshimiwa Jerry Silaa tumeweza kufanya kazi vizuri, sasa hivi tunahitimisha mchakato wa utwaaji wa lile eneo ili sasa iwe ni mali ya Serikali baada ya kuwa tumeshalipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishamaliza hapo sasa tuna bidhaa ya kuipeleka sokoni. Bidhaa yetu ni eneo letu lenye rasilimali ya makaa ya mawe pamoja na chuma cha Liganga. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais wiki moja iliyopita, sasa tunakwenda kuhitimisha majadiliano na huyu mwekezaji wetu ili

kazi iendelee. Hayo ndiyo maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pamoja na Mawaziri wenzangu, Waziri wa Mambo ya Nje anayeshughulika na diplomasia nje ya mipaka ya Taifa letu tunaendelea kukaa na watu hawa. Waziri wetu wa Madini, Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Waziri wa Fedha pamoja na Mwanasheria wetu Mkuu wa Serikali. Kama nilivyosema mwaka jana, tunachokihitaji ni kuhakikisha kwamba Taifa letu haliingii kwenye mgogoro mwingine ili tuweze kuanza utekelezaji wa mradi huo. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba hicho ndicho ninachokisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini wengi wananifahamu, huu ni mwaka wangu wa tisa hapa Bungeni; nasimamia haki na uadilifu ambavyo kwangu ni kitu cha kwanza. Naomba niwahakikishie kuwa mradi wetu huu tunakwenda kuuhitimisha vizuri, Taifa letu libaki salama. Mwekezaji kama anawekeza yeye awekeze, lakini kama hawezi akae pembeni tupate mwekezaji mwingine ili aweze kuifanya kazi hii na Taifa letu linufaike na madini haya tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda, wanatushauri vizuri, wana wataalam wazuri ndani ya Kamati, tunakwenda nao hatua kwa hatua na tutaleta mrejesho juu ya eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ya kielelezo, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, ndicho kipaumbele chetu cha kwanza kuhakikisha inaanza utekelezaji. Mradi mwingine wa pili ambao aliusema Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa ni Mradi wa Maganga Matitu. Serikali imeshafanya kazi yake, tumeshamaliza majadiliano na mwekezaji wetu, ndani ya miezi miwili ijayo tunasaini mkataba ili aendelee kufanya kazi yake nasi tuendelee kuvuna madini yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema jana, kwa kuliangalia eneo lote, kwa ukubwa wa eneo lile la Liganga na

Mchuchuma, eneo hili ni robo tu ambalo tuna mkataba na mwekezaji wa eneo zima la Liganga na Mchuchuma. Kama Serikali tulichoamua kukifanya ni eneo hili linalobaki 75% tumeweza kutengeneza sehemu yake, tumepata vitalu 48 ambavyo tayari tuna Watanzania wanaofanya utafiti wa kijiolojia na kampuni mbili zimefanikiwa kupata madini ya makaa ya mawe mazuri sana na wanaanza uchimbaji muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini tunafanya? Tunachotaka kufanya ni kuhakikisha dhamira ya Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi ya kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 - 2025 juu ya miradi hii ya kielelezo iweze kutekelezwa na athari chanya zipatikane kwa wananchi wetu na uchumi wetu kwa ujumla. Kwa hiyo, nalihakikishia Bunge lako Tukufu, mradi wenu uko mikono salama na tunakwenda kuutekeleza vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la pili, nilimsikiliza Mheshimiwa kaka yangu Askofu Gwajima wakati anaongelea Kiwanda cha *Kioo Limited;* kwamba wanaagiza kila kitu nje nikapata tabu kidogo, kwa sababu mmoja wa wakandarasi au wazabuni wanao-*supply feldspar* pale *Kioo Limited* ni mmoja wa Wabunge wenzetu hapa Bungeni. Kwa hiyo, niliposikia wanaagiza kutoka nje nilishtuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshakaa na *Kioo Limited* tukaelewana, malighafi zote na kama nilivyoandika kwenye kitabu changu cha hotuba, kwamba malighafi zote za viwanda vya vioo vilivyopo hapa nchini zinazopatikana hapa nchini 80% zinachukuliwa hapa nchini kwetu. Kama nilivyosema mmoja wa wazabuni anaye-*supply feldspar* ni Mbunge mwezetu, yumo humu, namjua. Sasa hili nitalifanyia kazi, lakini huo ndio ukweli na naomba Watanzania waamini hivyo. Sisi tuko hapa kulinda rasilimali zao na kulinda maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze *Kioo Limited* kwa sababu nimewataja. Juzi tukiwa kwenye Mkutano wa *CEO Forum* pale Kigali Rwanda, wameweza kusaini mkataba mwingine, wamepata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 45 kwa ajili ya kuendeleza kupanua na kuongeza uzalishaji kwenye kiwanda

chao. Ni kwa sababu ya mazingira mazuri ya uwekezaji pamoja na biashara yaliyowekwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wanatuletea zile fedha zinakuja ndani, tunakuja kuendelea kuongeza uzalishaji kwa sababu wanauza kwenye nchi zote za *SADC,* chupa zote wanazozalisha wanauza kwenye nchi zote za Ulaya, bidhaa zao wanazozizalisha. Soko lipo, mazingira ya uwekezaji, mazingira ya biashara ni mazuri. Naomba tuendelee kuwaunga mkono ndugu zetu wawekezaji wetu wanaokuja kuwekeza nasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwingine wa kielelezo ambao pia mama mpenda watoto wake Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuandika historia nyingine ni Mradi wa Magadi Soda Engaruka, huyo ndiye mama. Mpaka hapa tunapoongea namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutupatia shilingi bilioni 5.4 twende tukalipe fidia kwenye Mradi wa Magadi Soda Engaruka ili tuanze utekelezaji wa mradi huu. Mama anaiandika historia ambayo haikuandikwa miaka 60. Tuna sababu ya kumpongeza, Watanzania tuna sababu ya kumuunga mkono ili aendele kuchapa kazi yake na kutuhudumia sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara tuliyopewa dhamana hii tunawahakikishia kuwa tunakwenda kuusimamia tena mradi huu. Tulipe fidia watu wetu. Tutaanza na elimu kama kawaida ili pesa zao watakazozipata ziweze kutumika vizuri. Pili, naomba kulipa taarifa Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali ilishapeleka Wizara zote za Kisekta kule kwenye eneo letu la Magadi Soda Engaruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti za Wizara za Kisekta ambazo mmeshapitisha na nyingine mtapitisha, tukianzia ujenzi, nishati na maji; kwenye bajeti zile wana bajeti ya kuweka miundombinu kwenye eneo la Engaruka ili mradi huu tunapomaliza tu kulipa fidia tuanze utekelezaji. Kama ilivyosemwa hapa, uhitaji wa magadi soda ndani ya Taifa letu na duniani ni mkubwa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linajibu hoja ya kwamba Serikali yetu hii haifanyi kazi kwa pamoja. Si kweli, tunafanya kazi kwa pamoja, tunaratibiwa vizuri na mwanamama mahiri sana mwanangu Jenista Mhagama; tunamshukuru sana kwa kuturatibu. Tunakaa kwa pamoja kuongea na ndiyo maana wizara zingine zote tayari zimekwishafika Engaruka na tunakwenda kuanza utekelezaji kwa kuweka miundombinu yote muhimu ili wawekezaji watakapofika wawekeze bila kusema kwamba eneo hili linawakwamisha kwa sababu ya kukosa miundombinu inayowa-*support* kufanya uwekezaji wao. Kwa hiyo, ndugu zangu naomba niwahakikishie kuwa tuko tayari na tuko salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilitamani nalo kulizungumzia lilianzishwa mwaka jana kwenye Bunge letu la Bajeti wakati wa mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu mradi wetu wa *Ursus,* hasa kipande cha matrekta. Mdogo wangu Mheshimiwa Asia Halamga alisema vizuri wakati anatoa hoja zake kipindi cha mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwaambia Watanzania na wote waliokopeshwa matrekta yale mnaye mama mlezi, mnaye mama anayejua nini Watanzania wanahitaji. Nimshukuru Mheshimiwa Asia jana alisema kuwa tayari kuna utulivu mkubwa kwenye eneo lile, hakuna mwananchi aliyekopeshwa anayedaiwa kwa sasa kama ilivyokuwa kabla. Hayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwaambia Watanzania na wote waliokopeshwa matrekta yale, mnaye mama mlezi, mnaye mama anayejua nini Watanzania wanahitaji. Nikushukuru Mheshimiwa Asia jana ulisema tayari kuna utulivu mkubwa kwenye eneo lile, hakuna mwananchi aliyekopeshwa na anayedaiwa kwa sasa kama ilivyokuwa kabla, hayo ni maelekezo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari timu yetu ya Serikali imekwishamaliza kazi yake kwa 90% na sasa tunakwenda

kuhitimisha kwa sababu athari za matrekta yale hazifanani kwa wananchi wote 800 waliokopeshwa yale matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari zinatofautiana tunataka kuelewa kila mmoja aliathirika kwa kiasi gani na anastahili aidha kurejeshewa kiasi gani au kulipa kiasi gani kwa Serikali yetu, hiyo ndiyo kazi ndogo iliyobaki ambayo vijana wetu (timu yetu ya Serikali) inahitimisha na tukishahitimisha kwa sababu tuliahidi na tulielekezwa na Bunge kuhitimisha jambo hili, tutaileta taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, naomba hilo nalo niliweke hivyo, Mama amekwishafanya kazi yake nzuri ili tufanye kazi sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuhusu ufanyaji kazi wetu wa *SIDO* na hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao wamekuja na *BBT* viwanda, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaona mbali zaidi alikwishaelekeza. Tayari jambo hili na kwenye bajeti hii wanayotupitishia tunakuja na mtaa mmoja wa viwanda kwenye kila wilaya yetu ili tuchakate malighafi zinazozalishwa kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili naomba sana niendelee kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini niwashukuru wadhamini wetu na wadau wetu tunaofanya nao kazi kwa karibu sana, kwenye eneo hili, *USAID* kupitia mkataba wa kibiashara tuliosainiana nao wanatu-*support* kwenye eno hili na tutapita kwenye majimbo ya Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane ni wapi tutaweka mtaa huo wa viwanda ili kila wilaya iweze kuchakata malighafi zinazopatikana kwa wingi kwenye wilaya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mlivyosema sisi ni Wizara ya uratibu na narudia kile ambacho alikisema Mheshimiwa Dada yangu Jesca na ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe, wamelisema vema. Ni kweli kwenye ukurasa wa sita nimesema sisi ni waratibu, sisi tuna sera na tunafanya kazi na sekta nyingine. Kwa hiyo, hata hii mitaa ya viwanda tunafanya kazi kwa

pamoja na sekta nyingine za uzalishaji ili tuweze kuwahudumia Watanzania kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema jana, lakini Waheshimiwa Wabunge nao walisema kuhusu kulinda uwekezaji huu wa uzalishaji viwandani ambao Taifa letu linanufaika nao kama takwimu zinavyosema. Serikali yetu iko tayari kuwalinda wawekezaji wetu na tutawalinda wenye viwanda na kwenye maeneo yao wanayofanya kazi. Tunapokwenda kuwalinda, tunakwenda pia kuongea nao kuhusu hali ya watumishi wetu (watoto wetu wa kitanzania) wanaofanya kazi kwenye maeneo haya, waboreshe mazingira ya ufanyaji kazi kwenye viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishaanza na kama nilivyotoa taarifa tumekwishapita kwenye mikoa 10 na tukifika tunapita kwenye viwanda kuangalia mazingira ya biashara, mazingira ya ufanyaji kazi ndani ya kiwanda hicho kabla hatujakaa na mwekezaji yule.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatoe hofu, wengi wanasema kwamba, tunatoa taarifa wanajiandaa, siyo kweli, hatutoi taarifa. Taarifa tunayotoa ni kwa Mkuu wa Mkoa husika tunaokwenda kwamba, tunakuja kukutana na wafanyabiashara; wafanyabiashara wanapewa taarifa, wenye viwanda hatuwapi taarifa ili Serikali tujifunze mazingira ya kazi ya vijana wetu waliopo kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie kwamba, kwenye viwanda vyote tulivyopita zaidi ya 22, tulikutana na changamoto ya mazingira ya kazi kwenye eneo moja tu la kiwanda kimoja ambacho kipo Wilaya ya Temeke ambacho nacho nilikwishaikabidhi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu ili washughulike na kiwanda kile. Vijana wetu walipiwe *NSSF* zao, mikataba yao ya kazi isainiwe na mazingira ya kazi yaboreshwe. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, tumeamua kufanya kazi na tumeamua kuisimamia Sekta ya Viwanda na biashara. Naomba Wabunge watuamini kwenye eneo hilo na tuwaunge mkono wafanyabiashara wetu kwenye eneo hili la viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilisemwa kwenye eneo hili kwamba tukae na wafanyabiashara wazawa, hatutofautishi wewe ni mgeni au ni mzawa, tunakwenda kwenye viwanda vyote ambavyo viko ndani ya Taifa letu na kuongea nao ili kujua changamoto wanazokumbana nazo. Ndani ya Wizara yetu sisi tuna *slogan* moja, tukiwa ndani ya Serikali sisi ni sekta binafsi (sisi ni wafanyabiashara). Ndiyo maana hata jana nilipokuwa nawasilisha nilikuwa nawaita wafanyabiashara wenzangu, kwa sababu nikiwa Serikalini, ni sauti ya wafanyabiashara na hilo nalifanya kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, najua kuna sehemu tunapeana lugha ngumu kwa sababu mazingira mengine ninayokutana nayo huko siyo mazuri. Mheshimiwa Jesca, nikuhakikishie dada yangu upole wangu huu ni kwenye mambo mengine na siyo kazi, kwenye kazi mimi siyo mpole na Bunge hili linanifahamu vizuri, kwa hiyo, hilo nikutoe shaka, kwa hiyo, tunaongea sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alinipa funguo ya kuongea na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato moja kwa moja bila kupita kwake. Katika mtu ninayewasiliana naye sana ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, yaani kwa siku moja naongea naye zaidi ya mara kumi kwa sababu ya changamoto za wafanyabiashara kwenye maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa tu ninachokiomba ni wafanyabiashara wetu kuwa waadilifu na kufuata sheria. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema vizuri kwamba, kodi hukusanywa kwa sheria. Kwa hiyo, kama kuna sehemu kumevunjwa sheria hatuwezi kukubaliana na jambo hilo, lakini kwenye maeneo yote ambayo wanashughulika nayo Mamlaka ya Mapato Tanzania na siku hizi sasa huwa wananipigia simu wanasema Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara tunakwenda Kariakoo. Wananipigia simu ili nijue na niwaambie wafanyabiashara kwamba leo Mamlaka ya Mapato Tanzania wanakuja kufanya kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza pia Kliniki ya Biashara pale Kariakoo. Tuko pamoja, wakala wa usajili leo hii tunapoongea ana wiki nzima yuko Kariakoo pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuhakikisha kodi ya Serikali inalipwa, lakini tunaongeza *tax base* (wigo wa walipaji kodi). Tunawasajili wale ambao hawajasajiliwa ili tuongeze walipaji wa kodi ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, niwahakikishie kwenye eneo hilo nafanya kazi kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo hili aniruhusu tu niseme. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amezuia mahindi yetu yasiuzwe nje ya nchi, nilikuwa nampigia simu mpaka saa nane za usiku, kwa sababu, magari yamepanga foleni kule Namanga, hayapiti. Aliniruhusu na tukaweza. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo nikushukuru sana, tuliweza kutatua lile jambo usiku saa tisa, magari yakaanza kupita kwenda Namanga, lakini tunafuata sheria za nchi yetu. Kufuata sheria ndugu zangu, kunawalinda hata wafanyabiashara wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkikumbuka ile kesi iliyotokea Zambia. Hao hao wafanyabiashara wetu wamekwenda kununua mahindi Zambia na hawana vibali, wamezuiwa kule zaidi ya mwezi. Tunashirikiana kwa pamoja na wenzangu kutatua changamoto hizi ili tuweze kuwahudumia vizuri. Kaka yangu Mheshimiwa Kapufi, nimupe pole sana na sasa hivi tumeimarisha sana katika eneo hili. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuanzisha Idara ya Viwanda na Biashara kwenye halmashauri zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema jana, tumemaliza kufanya semina na hawa ndugu zetu wanaoshughulika na viwanda na biashara kwenye halmashauri zetu zote. Pia moja ya jambo ambalo tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, watu hawa ni walezi wa wafanyabiashara, waondolewe kwenda kukusanya tozo na ushuru, kwa sababu huwezi kukusanya tozo halafu ukamlea unayemkusanyia tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo tumekubaliana nalo kwamba, sasa hawa waendelee na semina na warsha kwenye maeneo yao. Tumewapa *target* kwa kila mwaka kwamba, kila Afisa Biashara aliyepo kwenye halmashauri lazima atengeneze wafanyabiashara 15 kwenye halmashauri yake, kwa sababu kazi yake yeye ni kuwatengeneza na kuwalea, lazima tuifanye hiyo kazi ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, hilo naomba sana tuwape *support* Maafisa Biashara wetu kwenye halmashauri zetu zote 185 ili waweze kutulelea wafanyabiashara wetu. Hawa ndiyo watakaoanzisha hata michakato ya mitaa ya viwanda tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili pia imesemwa kuhusu *issue* ya leseni moja. Ni kweli Serikali imeunda timu, inalifanyia kazi jambo hili ili kuondokana na changamoto kama tulivyosema awali. Kwa hiyo, naomba niwaombe sana, Mheshimiwa Kunti, mdogo wangu naona dalili za kukamata shilingi yangu, aniachie shilingi yangu ili nihitimishe hili jambo na tukalihitimishe jambo hili ndani ya Serikali halafu tukirudi hapa nitamwambia nini kimefanyika na atasikia, kwa sababu yeye ni Mjumbe wa Kamati asishike shilingi yangu, kazi inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili nimhakikishie, mjadala unaoendelea ni mzuri na kwa sababu ya mifumo ambayo imeboreshwa ndani ya Serikali yetu, *single window* tunakwenda vizuri na tunakwenda kuwahudumia wananchi wetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, imesemwa pia hoja ya kiwanda cha Viuadudu, Viuatilifu Kibaha, wapi tumefika? Kamati yetu inatusimamia vizuri sana. Sisi kama Serikali tayari Makatibu Wakuu, wamekwishakutana na sasa wanakwenda kusaini Mkataba wa kuweza kununua viuatilifu hivi kutoka kwenye Kiwanda chetu cha Viuadudu Kibaha, kazi inafanyika vema naomba watuunge mkono ili tuhitimishe jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema kama nilivyosema tumeanza pia kuzalisha *Biopesticides*. Ni dawa nzuri ya kuzuia wadudu waharibifu kwenye mashamba yetu. Profesa Ndakidemi amekwishai-*test* ile dawa na sasa tunaisambaza nchi nzima ili

tukipatie uhai Kiwanda chetu cha Viuadudu Kibaha na kiweze kutengeneza pesa vizuri na kufikia ile dhamira ya kuanzishwa kwa kiwanda chetu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge jambo moja. Serikali yetu haijawahi kuwa na dhamira mbaya kwa wananchi wake. Kumekuwa na mjadala hapa kwamba, yawezekana dhamira haikuwa nzuri au ilikuwa nzuri, Serikali haijawahi kuwa na dhamira ovu kwa wananchi wake. Kilichofanyika wakati inahamishwa Chakula na Dawa kutoka *TFDA* kuja *TBS* yalikuwa ni maamuzi makini ambayo wataalam waliyafanyia kazi na mambo yote yakakubalika. Kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge juzi tukiwa kwenye semina, kilichofanyika, *TBS* walipelekewa watumishi wote 81 pamoja na vifaa vyao walivyokuwa wakifanyia kazi vya kimaabara. Sijapata malalamiko popote kwamba, *TBS* hawafanyi kazi yao sawasawa,. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuendelee kusimamia maamuzi tunayoyafanya wenyewe, wataalam ni wale wale, maabara ni ile ile. Ni kipi kinacholeta hoja ya kwamba kazi haifanyiki sawasawa? Kwa sababu nikiwa Waziri wa Viwanda na Biashara naifanya kazi yangu sawasawa. Nikipelekwa kuwa Waziri wa Uchukuzi, siamini kama kazi yangu haiwezi kuwa sawa awa, kwa sababu mtu ni yule yule na uwezo ni ule ule. Kwa hiyo naombeni sana sana, jambo hili limekuja na hoja kwamba tuangalie *best practice,* hivi sisi hatuwezi kuwa *source* ya *best practice* duniani? Inawezekana sana na naomba tusimamie maamuzi yaliyofanyika na Bunge lako Tukufu mwaka 2019 na maamuzi ambayo yanasimamiwa vizuri na vijana wetu ambao wanafanya kazi nzuri. Pia, niendelee kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge tupite pale *TBS,* tuone kazi nzuri inayofanywa na watumishi wetu kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya naomba sasa kusemea suala la bajeti ndogo ya Wizara kama ambavyo imesemwa. Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme bajeti inatutosha, tunakwenda kufanya kazi na niishukuru Kamati

wametuwezesha kuongezewa bajeti kwa 20% ya tulipokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu nimesema sisi ni waratibu, sisi siyo watendaji wa moja kwa moja, sisi hatuwekezi kwenye viwanda. Naomba sana watuunge mkono kutoka kwenye bajeti hii tuliyoongezewa kutoka bilioni 92 mpaka bilioni 110, ni hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha hizi tulizoongezewa naomba niwatoe hofu Wajumbe wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Kilimo, katika pesa tuliyopewa ile bilioni 3.4 ya *KMTC* ni sehemu ya pesa tuliyoongezewa. Kwa hiyo, *KMTC* wanakwenda kupata fedha yao yote ili waendeleze kazi nzuri ambayo wanaifanya. Naomba sana watuunge mkono ili tuendelee kufanya kazi hii nzuri ambayo tumeianza pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naomba sasa kuliomba Bunge lako Tukufu kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba Bunge lako liidhinishe jumla shilingi 110, 899,722,000 kwa Fungu 44. Kati ya fedha hizo shilingi 81,115,206,000 ni matumizi ya kawaida na shilingi 29,784,516,000 ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINABU ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 44- Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kifungu 1001 – *Admininstration and Human Resources Management*...................................Sh.18,403,443,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuna mshahara hapa, Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKF. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina lengo la kumshikia Mheshimiwa Waziri shilingi yake lakini wakati nazungumza nilisema kwamba, kuna baadhi ya *element* nne ambazo ndiyo *raw materials* ya chupa hizi. Mojawapo ni *feldspar, silica sand, limestone* na *soda ash*. Pia, nikasema kwamba *soda ash* tuna *import* kutoka nje mpaka leo. Vilevile, *feldspar* pia tuna *import* mpaka leo kwa *data* ya kutokea Wizarani kwake, lakini yeye amesema kwamba hawa-*import* chochote. Naomba maelezo na kama hana maelezo ya sasa hivi, kama anahitaji ku-*verify* na Wizara yake itakuwa vizuri kwa ajili ya kutunza rekodi. Vinginevyo sina haja ya kushika shilingi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimshukuru Mheshimiwa Askofu Gwajima kwa hoja yake hii. Kama nilivyosema wakati natoa ufafanuzi, sijapingana na hoja yake, nimesema katika moja ya viwanda ninavyofanya navyo kazi kwa karibu ni kiwanda hiki cha *Kioo Limited*. Nikasema nimeipokea taarifa yake kwa sababu taarifa tulizonazo sisi ni kwamba wana *import soda ash* tu na *raw materials* nyingine wanachukua kutoka hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama alivyosema hana haja ya kushika shilingi yangu, nimwombe tu, nakwenda kulifanyia

kazi jambo hili ili kuhakikisha na lengo ni lile lile la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha malighafi zote zinazopatikana hapa nchini zinachakatwa na viwanda vyetu tulivyonavyo. Nakushukuru sana

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINABU ISSA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..................Sh.632,380,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....................Sh.1,798,644,000
Kifungu 1004 – *Government and Communication Unit*..........................................................Sh.391,176,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*.................................Sh.372,875,000
Kifungu 1006 – *Legal Services Unit*................................Sh.439,837,000
Kifungu 1007 – *Management Information System*.......Sh.498,368,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*.........Sh.476,364,250
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh.565,444,000
Kifungu 2001 - *Industry*..............................................Sh.12,805,693,750
Kifungu 2002 - *Small and Medium Enterprises Division*..................................................Sh.7,367,165,000
Kifungu 3001 – *Trade Integration Unit*.........................Sh.1,910,537,000
Kifungu 4002 – *Commodity Market Development*………………………..Sh.35,453,279,000
Kifungu 5001 - *Investment Development Division*..........................*Sh.0*
Kifungu 5002 – *Economic Empowerment and Private Sector Development*................................Sh. 0
Kifungu 5003 – *Business Environment Unit*……………………………Sh. 0
Kifungu 6001 – *Research and Innovation Unit*……………..………Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINABU ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 44- Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*......................................Sh.1,150,000,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....................Sh.7,897,860,000
Kifungu 2001 - *Industry*...........................................Sh.17,736,656,000
Kifungu 2002 - *Small and Medium Enterprises Division*...............................................Sh. 3,000,000,000
Kifungu 4002 – *Commodity Market Development*………………...Sh. 0
Kifungu 5002 – *Economic Empowerment and Private Sector Development*................................Sh. 0
Kifungu 5003 – *Business Environment Unit*…………………………Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINABU ISSA – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**NAIBU SPIKA:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Wote mmeafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hongera sana, bajeti yako sasa imepita rasmi, nendeni mkafanye kazi mliyoagizwa na Bunge hili, Serikali na wananchi kwa ujumla. Nawapongeza watendaji wote wa taasisi zako, lakini niwapongeze Wabunge kwa michango mizuri ambayo imeonesha uelewa na maelekezo na ushauri walioutoa, basi mzingatie.

Baada ya hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.25 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 23 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*